BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	Mhe.	Zubeir Ali Maulid	-	SPIKA
2.	Mhe.	Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
3.	Mhe.	Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4.	Mhe.	Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
5.	Mhe.	Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
6.	Mhe.	Issa Haji Ussi Gavu	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
7.	Mhe.	Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
8.	Mhe.	Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
9.	Mhe.	Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais
10.	Mhe.	Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
11.	Mhe.	Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	Mhe.	Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
13.	Mhe.	Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais
14.	Mhe.	Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais
15.	Mhe.	Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani

16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**

34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
36.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
37.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
38.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
39.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**

85.	**Mhe. Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe. Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
	Ndg. Raya Issa Msellem	**-**	**Katibu**

Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 28 Juni, 2018

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Mezani Ripoti ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Mhe. Ali Khamis Bakari (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuweka Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Mhe. Naibu Spika naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa sana naomba kuweka Mezani Hoja ya Mjumbe kuhusu kuchukuliwa hatuwa stahiki dhidi ya kadhia ya Timu ya Taifa ya Vijana ya Zanzibar kufutwa katka mashindano ya *CECAFA Under Seventeen* na kupewa adhabu kutokana na madai ya kudanganya umri wa wachezaji. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 205

Ufinyu wa Bajeti ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kumekuwa na kilio cha ufinyu wa bajeti ya matumizi mengineyo katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba (*DPP*), ambapo kwa mwezi wanaingiziwa shilingi 3,000,000/= kufanya kazi za ofisi na hazitoshelezi.

(a) Je, kwa nini ofisi hii nyeti sana katika kuchunga haki jinai kisiwani Pemba inapewa fedha chache sana za matumizi ya kila mwezi.

(b) Je, kuwapa fedha kidogo kama hizo hatuoni kwamba Ofisi ya *DPP* Pemba inakwama kufanya majukumu yake kwa ufanisi na badala yake wanabeba mzigo mkubwa kutoa huduma.

(c) Ni hatua gani zitachukuliwa kuhakikisha Ofisi ya *DPP* kisiwani Pemba inapata fedha za *Other Charges (OC)* za kutosha kufanya majukumu yake kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 205 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, serikali inakiri kwamba ni kweli kulikuwa na tatizo la kiufundi katika sehemu ya hesabu kulikopelekea muingizo mdogo wa kifedha katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba. Kwa sasa tatizo hilo limeshatatuliwa na Afisi ya Pemba inapokea fedha za matumizi ya kawaiida kwa mujibu wa bajeti ilivyopangwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika majibu yake alisema kuna neno kiufundi naomba atueleze neno kiufundi lina maana pana, je anaweza kutufahamisha kwa faida ya Baraza hili, ili tuweze kuelewa kwa nini wakashindwa kujipangia bajeti yao ni sawa mtu kukataa kula chakula wakati chakula anacho.

(b) Kwa nini ofisi za Pemba haiwezekani kupelekewa bajeti yao moja kwa moja, ili kuondosha utaratibu huu ili wananchi wapate kutumikiwa vizuri katka kusimamia haki na wajibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye kifunge (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku anataka kujuwa tatizo la kiufundi ni lipi kiufupi ni kwamba hili ni tatizo la *system*, *system* ndio chanzo cha tatizo hili lakini ofisi baada ya kugundua lile tatizo kiasi cha fedha ambacho kilichopelekwa kule ni kidogo ofisi ilichukuwa jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba kile kiwango ambacho hakikufika au hakikuingizwa kwenye *system*. Kwa kweli, kiwango kile kilipelekwa na fedha karibu zote waliweza kuzipata na matumizi yao wakawa wanayafanya kama kawaida.

(b) Mhe. Naibu Spika, ni kwamba ofisi za Pemba fedha zao wanapata moja kwa moja kwa sababu wana *sub vote* kule. Kwa hiyo, fedha mara tu zinapoingizwa basi huwa zinakwenda moja moja na kiufupi wao wanapokea asilimia 25 kule kwa hivyo mara tu

bajeti ya mwaka inapokamilika fedha zao 25% wanapelekewa na wanafanya matumizi yao bila ya wasi wasi wowote. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: kuhusu utaratibu

Mhe. Naibu Spika: kuhusu utaratibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, 63, 37 Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi Wa Umma na Utawala Bora nafikiri hakunifahamu nimwambie katika majibu yake alisema neno kiufundi nikamwambia lina maanda pana je unaweza kutufahamisha kwa faida ya Baraza hili, hili neno fundi lina maana gani ili Baraza lipate kujuwa maana yake ni sawa sawa na mtu kuwa na chakula akashindwa kukila baadae.

Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni kwamba Mhe. Jaku Hashim Ayoub anaposema na *microphone* na anajuwa kuna tatizo la *echo* inabidi aeleze vizuri jambo lake ili Mhe. Naibu Waziri asikie na Waheshimiwa Mawaziri wasikie na Wajumbe wengine wasikie anaposema kwanza anasema kwa haraka halafu hasemi na *microphone* kwa hivyo hatumsikii kwa hiyo chochote alichokisema hata Makati Mezani hawakumsikia. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika tunaomba yeye ajibidiishe kusema vizuri anaposema, ili tumsikie tunaomba arejee tumsikilize alichokisema. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub rejea swali lako taratibu ni kweli kwamba mara nyingi sana unasema haraka, husikilikani, lakini vile vile unapozunguma *concentrate* kwenye kipaza sauti ambacho ulichonacho hapo, naomba urejee swali lako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na uzuri Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndie mwenye dhamana wachombo na anajuwa hizi ndude muda mrufu zina matatizo na Mhe. Waziri tumepitisha bajeti juzi na naona kwa nini hutaki kuzishughulikia mpaka muda huu jitahidi kufanya jitihada hizo Mhe. Waziri hili jambo liko mikononi mwako na uzuri umesimama mwenyewe umejihukumu mwenyewe umejiengezea sheria mwenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora alipokuwa akijibu alisema neno kiufundi lina maana pana, je anaweza kutufafanulia kwa faida ya Baraza hili, ili tuweze kuelewa kwa nini wakashindwa kujipangia bajeti yao ni sawa na mtu kukataa chakula wakati chakula anacho hilo (a) sijui na la pili nirejee

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub ulilokuwa hujajibiwa ni lipi si ndio hilo moja tu jengine ulishajibiwa, haya mjibu swali hilo linohusiana na ufundi

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi Wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali la nyongeza ambalo anataka kujuwa maana ya kiufundi ilokusudiwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli katika Kamusi ya Kiswahili inawezekana ukaliona neno moja linamaana zaidi ya moja ya matumizi lakini hapa kilichokusudiwa kwamba kiufundi kwa maana

ya neno kiutaalam kwa hivyo palikuwa pana makosa ya kiutaalam na katika jawabu langu mama nilisema kulikuwa matatizo ya kiufundi katika masuala *system* nashukuru sana ahsante.

Nam. 138

Uwekaji Mbaya wa Majina ya Mitaa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Hivi karibuni kumekuwa na utaratibu wa kuweka majina ya mitaa mbali mbali ya Unguja na Pemba kwa kuweka vipati kwenye nguzo vikiwa na majina hayo. Jambo la kushangaza baadhi ya majina mengi yaliyowekwa hayaendani na uhalisia wa pahala panapohusika, majina yamebuniwa wala hayana uhalisia wa eneo husika.

(a) Je, utaratibu gani umewekwa wa kuita maeneo yetu majina bila kuharibu uasili wa eneo husika.

(b) Wapo masheikh, wanasiasa wa Kamati ya Mapinduzi ya watu 14, wanamichezo, wasanii na kadhalika kwa nini majina yao hayaenziwi kwa kuitwa mitaa yetu na badala yake tunatumia majina ya mashujaa wa nje ya Zanzibar kuwaenzi.

(c) Kwa nini majina ya mitaa ya asili ya Zanzibar inapotezwa na badala yake tunaagiza majina kutoka nje ya Zanzibar au Tanzania Bara kama vile Kiboje Manzese, Nyarugusu na kadhalika huku yale ya kwetu yakiachwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 138 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003, ilianzisha kwa majaribio (*pilot*) mfumo wa anuani zinazoendana na majina ya mitaa ambapo watu binafsi na maeneo ya biashara yatatambuliwa kwa kutumia majina ya maeneo yaliyopo pamoja na postikodi zao. Katika majaribio hayo mfumo huu wa Anuani za Mkaazi na Postikodi umeanza katika Shehia za Chukwani na Mombasa kwa Unguja na Limbani na Selem kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Muongozo wa Mfumo wa Anuani za Makaazi wa mwaka 2016, zoezi la uundaji wa majina ya mitaa linatakiwa kuzingatia pamoja na mambo mengine vigezo vifuatavyo:- historia ya mtaa husika, majina ya watu, matamshi ya majina, kuzingatia sheria na jinsi kuepuka kuleta mgawanyiko katika jamii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ tayari imeandaa rasimu ya muongozo unaozingatia mazingira ya Zanzibar na Mfumo wa Anuani wa Makaazi kwa kuzingatia vigezo nilivyovitaja katika maelezo yangu hapo juu. Muongozo huo utakaotumika katika kupendekeza majina ya mitaa na barabara baada ya kupitishwa rasmi.

(b) Mhe. Naibu Spika, watu mashuhuri wakiwemo Masheikh, Wanasiasa, Wanamichezo na Wasanii wanayo nafasi ya majina yao kuenziwa kwa kuyatumia majina hayo katika mitaa na barabara kama ilivyoainishwa katika vigezo nilivyovitaja hapo juu.

(c) Mhe. Naibu Spika, sina jibu la moja kwa moja kuhusu sababu zinazosababisha majina ya mitaa ya asili ya Zanzibar kupotea na badala yake kutumika majina kutoka nje ya Zanzibar. Suala hili linahitaji kufanyiwa utafiti wa kina ili kupata sababu zinazopelekea suala hili. Hata hivyo, mfumo huu mpya wa anuani za makaazi unayo nafasi kubwa ya kuyarejesha majina ya asili kwa vile upatikanaji wa majina ya mitaa utakuwa shirikishi katika ngazi mbali mbali za jamii. Naomba nichukue fursa hii adhimu kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kutoa majina ya mitaa yanayozingatia hulka, utamaduni, maadili na silka za kizanzibari. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya kumuuliza maswala madogo ya nyongeza Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ nimpe pole yeye na Mhe. Waziri na Watendaji wake, Mkuu wa Mkowa, Mkuu wa Wilaya jinsi walivyotembelea masoko na wakaona hali ilivyo masoko yale yalivyo, nikupongezeni kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na Naibu Waziri, Wakuu wa Mikowa, Wakurugenzi na pale mlipochukuwa hatuwa ya kumsimamisha mfanyakazi mmoja wa Manispaa katika Soko la Samaki la Darajani. Baada ya pongezi hizo naomba kumuuliza swali moja la nyogeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, majina ya mitaa huzingatia mambo muhimu ya historia na majina ya watu maarufu yenye mchango mkubwa katika taifa, hayo majina tunayoyaona yamepatika kwa utaratibu gani.

(b) Kwa nini Zanzibar ina mambo ya kihistoria yangeweza kutowa majina yakiwemo hata matunda, Tofaa *street*, Doriani *street*, Shokishoki *street*, majina ya wasanii na viongozi wa dini maarufu kwa nini tusichukuwe hatua hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa majibu ya ziada Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wakati nilivyokuwa nikijibu katika jibu langu la msingi nimeeleza bayana kwamba kwa namna gani ambavyo shughuli hii ambavyo inatarajiwa na kwa namna changamoto hizi ambazo zimekuwepo zikijitokeza katika mitaa yetu katika majina hayo ambayo yamekuwa yakijitokeza. Vile vile, nimesema tu kwamba umuhimu wa kuwaenzi viongozi pamoja na masheikh na wanasiana kama ambavyo nimeelezea ni kwamba iko haja na uko umuhimu wa kufanya hivyo.

Lakini nataka niseme tu Mhe. Naibu Spika, kwamba kazi hii pamoja na ushauri Mhe. Mwakilishi ambao ameutoa tunaopokea, pia naomba tu aendelee kwanza kutustahamilia katika kazi hii kwa sababu hii inafanyika kwa mashirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na Ofisi inayoshughulikia masuala ya miundombinu. Kwa hiyo, pale muda utakapofika ni dhahiri kwamba yale yote ambayo ameyaelezea na yale ambayo ameyashauri Mhe. Mwakilishi, naomba niseme Mhe. Naibu Spika, tutayazingatia tutaweza kuyafanyia kazi, ili kufikia kupata lile lengo ambalo tumekusudia kupata mitaa ambayo haina majina yale ambayo hayaendani na silka za Kizanzibar.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, maeneo mbali mbali yanayopewa majina ili kurahisisha mtu yeyote akifahamishwa njia namba fulani, jina fulani inakuwa rahisi na mtu kuelewa kwa haraka, lakini kwa kuwa majina hayo hutolewa na Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ametwambia kwamba Wizara yake na Wizara ya Miundombinu zinahusika kukaa pamoja na kutowa majina hayo. Je, kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo wapo mashuhuri na wapo wanaojuwa zaidi kuliko wao hawaoni ni vyema kukaa na wananchi hao kwa kuwapa historia kamili ya maeneo hayo na kupata majina sahihi bila usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba naomba nikubaliane na Mhe. Ali Suleiman Ali kwamba wananchi wanahitaji kupatiwa taaluma ya mara kwa mara kuhusiana na mambo tofauti likiwemo hili ambalo tumelizungumzia kwa sasa hivi la kuweka majina ya mitaa na mengine kama hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuhakikishie tu Mhe. Ali Suleiman Ali kwamba zoezi hili hata huko ambako tumelifanya katika lile la majaribio katika Shehia zile tumezitaja Unguja na Pemba tulifanya kwa mashiriano au kuwashirikisha wananchi katika maeneo husika. Lakini katika zoezi hili zilikuwepo changamoto nyingi lakini hata hivyo tuliweza kushirikiana na wananchi na ndio mana zoezi hilo ambalo la majaribio likaweza kufanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimwambie tu Mhe. Ali Suleiman Ali kwamba pale muda utakapofika wa kuliendeleza zoezi hili basi kama vile ambavyo tumefanya tutaendelea kuwashirikisha wananchi wetu pamoja sambamba na kuwapatia taaluma waweze kufahamu

namna na yale malengo ya makusudio ya zoezi hilo, ili kusudi kurahisha shughuli za wananchi pale ambapo mtu anataka kwenda mtaa fulani basi aweze kufika kwa urahisi zaidi.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza pamoja na majibu matamu kabisa na mwanana ya Mhe. Naibu Waziri. Napenda kujua na ukilingania na malalamiko wanayotoa Waheshimiwa Wawakilishi kuhusu hiyo mitaa. Je, hiyo mitaa hapo zamani ilikuwa haipo na kama ilikuwa haipo sasa mnaunda mipya. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba katika maeneo ambayo sasa hivi tunaendelea kufanya zoezi au tuliofanya katika zoezi hilo la majaribio lazima tukubali kwamba mitaa imeongezeka katika ujenzi umekuwa mkubwa na vile vile wananchi wanahitaji kupata majina katika yale ambayo wanajenga majengo yao. Lakini kwa mitaa ambayo vile vile kuna mitaa mengine majina ilikuwepo lakini mengine pia inaendelea watu kutaka kubadilisha majina kwa ile *interest* ambazo wanaziona wao wenyewe zionaona kwamba wanataka kufanya hivyo.

Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi ni kwamba mitaa hii ilikuwepo mengine na majina ilikuwepo lakini mengine ni mitaa mipya ambayo ndio hasa kwa uzoefu unavyoonekana kama majina haya mengi yamekuwa yakishamiri. Kwa hivyo, nilitaka kutoza maelezo hayo Mhe. Mwakilishi naomba tulifahamu hilo na ndicho kitu ambacho kimepelekea tuendelee na zoezo hili ili kuweka mambo sawa ili tupate ile mitaa na majina tunayoitaja.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 238

Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:

Kwa bahati mbaya ujenzi wa Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi umechelewa kuanza kwa muda mrefu hadi sasa. Kwa kuwa eneo la ujenzi wa afisi hiyo lipo hapo Amani limezungushwa mabati hadi sasa.

Je, ni lini ujenzi wa Afisi hiyo utaanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake Nam. 238 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi umechelewa kuanza ujenzi wake ambapo kuchelewa kwake kunatokana na Muwekezaji aliyepewa kazi hiyo ya ujenzi kwa njia ya *BOT* kushindwa kupata fedha za ujenzi huo kwa wakati uliokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, jambo ambalo limepelekea kuchelewa utekelezaji wa mradi huo kwa wakati. Hata hivyo, jitihada mbali mbali zinachukuliwa ili kuhakikisha kwamba shughuli za ujenzi zinafanyika kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa jitihada zilizofanyika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Muwekezaji imezungumza na Benki ya *CRDB*, ambapo hatua iliyofikiwa hadi sasa ni Benki hiyo kusaini makubaliano ya awali na Muwekezaji yanayoashiria utayari na muelekeo wa kupatikana kwa fedha hizo ili shughuli iliyokusudiwa iweze kufanyika.

Mhe. Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa endapo taratibu hizo zitaendelea kwa mujibu wa mazungumzo, fedha hizo zinapatikana hivi karibuni na shughuli za ujenzi zitaanza baada ya kupatikana kwa fedha hizo.

Aidha, ikiwa muelekeo huo wa kupatikana kwa fedha hautakuwa na matumaini mazuri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inatarajia kuanza hatua za dharura za kuanza kujenga wenyewe jengo hilo taratibu kutokana na fedha ambazo tutaweza kuzipata.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa kuonesha jitihada kubwa ambazo anakwenda nazo ili kuhakikisha kwamba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inakuwa ya kileo na kutoa huduma zake kwa jamii. Lakini pamoja na hayo Mhe. Naibu Spika niseme tu kwamba Ofisi ya Mhe. Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi ni Ofisi muhimu zote muhimu lakini Mjini kutokana na mandhari yake na Makao Makuu ya Serikali pana haja ya kuonekana ujenzi wake unakwenda haraka pamoja na mazingira yaliokuwepo na kwa kuwa muda mrefu pamebomolewa pahapa pale na mabati yanaibiwa hadi leo hii.

Je, wizara kwa kuhakikisha kwamba kuna maofisi mengi ya serikali mfanoTakwimu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ukienda Waziri wa Katiba, Sheria ni ya kileo imejengwa kwa haraka pana kitu gani serikali yenyewe bila ya kutaka mfadhili ana miradi yake lakini sisi tunamahitaji yetu kuanza kujenga wenyewe na kutafuta miundombinu kama wanataka kukodisha chini wakodishe juu watumie ofisi, ili iwe pato linalopatikana linaingia moja kwa moja katika mkoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuendelea kumjibu naomba nipokee pongezi zile za jitihada ambazo tunaaendelea kuzifanya lakini vile vile naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe.

Mwakilishi kwa namna ambavyo amekuwa akishirikiana nasi katika kuona kwamba shughuli zza ofisi yetu zinafanikiwa na hazikwami katika maeneo yote yale.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo maelezo mafupi naomba nitowe majibu kwa Mhe. Mwakilishi kwamba serikali haijashindwa kwamba kujenga ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kama vile ambavyo imejenga majengo mengine katika maeneo mbali mbali hapa nchini katika ofisi zake. Vile vile, tukumbuke kwamba ambao katika ujenzi huu hii ni mambo ambayo tuliyapanga na haikatazi na wala haipingani kwamba kutafuta watu ambao wanaweza kusaidia miradi mbali mbali hapa nchini, kwa sababu serikali ndio ambyo imefungua milango kwa hiyo kiufupi ni kwamba utaratibu ambao tumeutumia ni huo.

Lakini, kwa sasa vile ambavyo kama nilivyosema pale tutakapoona kwamba tumeshindwa kupata fedha kwa njia hiyo ambayo tumeitaja, ndio nikasema kwamba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa tutalifanyia kazi jambo hili, ili kuona kwamba Mhe. Mkuu wa Mkoa pamoja na Ofisi za Mikoa mengine tunaona kwamba ifikiwe wakati basi na wao wawe na majengo kama vile taasisi nyengine ama ofisi nyengine ambazo tumekuwa nazo. Mhe. Naibu Spika, kiufupi tumefanya mengi na serikali imekuwa ikiya-*support* kwa kiwango kikubwa sana.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na maelezo mengi ya Mhe. Waziri ambayo kwa kweli mimi hayanifurahishi. Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa jengo hili umechukuwa siku nyingi mpaka hayo mabati hivi sasa yaliyozungurushiwa hayapo kwa sehemu kubwa sasa na ninaoneka vile vile pengine uwezo wa huyu mwekezaji sifa zake ni ndogo. Kwa hivyo, naomba kuuliza tu, mwekelezaji huyu ni nani, tuambiwe. Vile vile, ni taratibu gani za tenda na vigezo vya sifa ambazo vilitumika kumpata mwekelezaji huyu. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kwanza nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi kwa namna ambavyo kwa kweli amekuwa akiona kwamba kuna umuhimu mkubwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kuamilika kama vile ambavyo au kujengwa ili kuweza kutoa huduma kutokana na umuhimu wake.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba tulipokuwa tukiendelea na mkutano wetu wa bajeti kwa kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa maelezo yakina sana Mhe. Waziri wa ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa aliweza kuyatoa na akatoa ufafanuzi wa kina juu ya jambo hili. Kwa hiyo kwa sasa hivi naomba Mhe. Mwakilishi kwa kuwa majibu yameshatolewa sina majibu mengine ya ziada ambayo yatakuwa tofauti na yale ambayo Mhe. Waziri aliweza kuyatoa wakati akitowa ufafanuzi. Kwa hiyo, naomba tu turejee tena kwamba Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe watuamini juhudi tunayoifanya ni kubwa na serikali haipendi kuona kwamba yale mipango yake au majengo yake imekusudia kwamba ofisi zifanye kazi nzuri basi kuona kwamba tunafanya katika mazingira ambayo hayako vizuri.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika kwa kutumia fursa hii naomba Mhe. Mjumbe turudi kwenye *hansard* angalie maelezo yale ambayo Mhe. Waziri aliyatoa na mimi sitakuwa na majibu mengine ya ziada tukiachana na majibu ambao Mhe. Waziri aliyatoa katika kipindi cha bajeti.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kutokana na dharura aliyonayo Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifungo na Uvuvi ameomba swali lake lisigezwe mbele hivyo basi tutakwenda katika swali la 71 pamoja na swali ya 213 halafu tutarudi kwenye maswali mengine kama mpangilio unavyotuekeza katika *'Order Paper'*; yetu ahsante.

Nam. 71

Mgawanyo wa Matrekta Unguja na Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Hivi karibuni kiasi cha matrekta 47 yamepatikana na kugaiwa kwa upande wa Unguja, hata hivyo, mgawanyo huo hauna mgawanyo kwa upande wa kisiwa cha Pemba.

Je, kwa nini matrekta hayo hayajagawanywa kwa upande wa kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 71 kama ifuatavyo:

Kwanza nampongeza sana Mhe. Mwakilishi kwa kutaka kwamba na matreka yaapelekwa Pemba anataka kuona matreka yanapelekwa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, matrekta yamepelekwa Pemba matrekta 47 yamefikiwa baada ya kupokea matrekta mapya 20 (10 aina ya *New Holland* na 10 aina ya *Mahindra*), na matrekta 10 aina ya *Massey Ferguson* kutoka Ubalozi wa Libya - Dar-es-Salaam. Kabla ya hapo, wizara ilikuwa na matrekta 17.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inapenda kulithibitishia Baraza lako Tukufu kuwa mgawanyo sahihi wa matreka mapya na makongwe kama ifuatavyo:

1. Matrekta mapya ya *"New Holland"* - Unguja 7 na Pemba 3.
2. Matrekta mapya *ya "Mahindra"* - Unguja 6 na Pemba 4.
3. Matrekta ya zamani – Unguja 12 na Pemba 5.
4. Matrekta ya *"Massey Ferguson"* kutoka Ubalozi wa Libya – 10 Unguja tu.

Mhe. Naibu Spik, naomba kuwasilisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na nimpongeza Mhe. Naibu Waziri lakini vile nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa juhudi

anazozichukua katika sekta mbali mbali ikiwemo afya, ardhi na kilimo ndio *engine* kuu au ndio uchumi wa nchi yetu, lakini nitakuwa sitamtendea haki kama sikumshukuru Mkurugenzi au Meneja wa fani wa kitengo cha matreka kwa jitihada walizozichukua kwa umakini wake wa hali ya juu.

Je, serikali imejipanga vipi kuhakikisha vipuri vinapatikana kwa wakati matreka yaweze kufanya kazi kwa muda wote na kufanyiwa *service* na matengenezo bila ya kuathiri shughuli za kilimo moja tu hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Katika kuhakikisha kwamba vipuri vinapatikana wizara hivi sasa imeshaorodhesha mahitaji ya *spare* zote ambazo zinatakiwa na tayari tunazifanyia kazi na *Inshaallah spare* hizo zitapatikana na kutakuwa hakuna tatizo la ukosefu wa *spare* hapo baadaye. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 213

Mashamba ya Karafuu Yaliyorejeshwa Serikalini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Hivi karibuni kumekuwa na harakati za kurejesha mashamba ya mikarafuu serikalini, hata hivyo yapo baadhi ya mashamba yanadaiwa kuwa ni ya wananchi na yana hati miliki za wananchi pia yamechukuliwa na kurejeshwa serikalini.

a) Je, serikali imefanya utafiti wa kina kujua mashamba yepi ya wananchi na yepi ya serikali, ili kuondoa malalamiko kwa wale wenye hati miliki za mashamba yao yaliyochukuliwa.

b) Je, serikali ikigunduwa kuna mashamba yamechukuliwa kimakosa ipo tayari kuwarejeshea wenyewe bila kusumbuana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 213 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imepewa jukumu la kuyatafuta na kuyakodisha mashamba yote ya serikali ambayo wamiliki wake hawakupatiwa mikataba ya eka tatu tatu na pia kwa mashamba ambayo wanaostahiki kuyasimamia kwa mujibu wa mikataba ya eka tatu tatu hawapo tena. Kwa awamu ya mwanzo Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ilifanikiwa kuyatambua mashamba 5,822 katika Wilaya zote za Pemba (Wete, Chake, Mkoani na Micheweni).

Mhe. Spika, kufuatia utambuzi wa mashamba hayo katika mwezi wa Oktoba 2016, wizara iliwasilisha serikalini waraka kuhusiana na usimamizi wa mashamba hayo, na hivyo serikali

kuiagiza Wizara ya Kilimo kuendelea kuyatafuta na kuyatambua mashamba ambayo bado yalikuwa hayajatambuliwa. Hadi hivi sasa jumla ya mashamba 5,822 yametambuliwa kiwilaya kama ifuatavyo: Wete – 1,250, Micheweni – 831, Chake – 1,417 na Mkoani – 2,324.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu sasa Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo:-

Serikali imefanya utafiti wa kina kujuwa mashamba yepi ya wananchi na yepi ya serikali kwa lengo la kuondoa malalamiko. Pindipo ikibainika kuna shamba lolote la mwananchi limechukuliwa kimakosa serikali italirejesha kwa muhusika.

Naomba kuwasilisha Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza maswali madogo sana ya nyongeza. Kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko mengi juu ya zoezi lilivyokwenda kwa nini serikali haioni kuna haja ya kuunda kamati ya kuchunguza ili wanaolalamika hawakutendewa haki madai yao yaweze kuchunguzwa na serikali kupata ukweli wa kadhia hiyo. Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwa mashamba haya wengine wana hatimiliki wengine hawana.

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri atakuwa tayari kuunda kamati maalum ya kwenda kuchunguza kule kupata ukweli wananchi wasije wakapata haki zao. Hilo la kwanza.

(b) Kwa kuwa kuna tuhuma za madeni ya mashamba hayo kinyume na utaratibu kuna madeni yamekodishwa mashamba yale pesa zile hazijalipwa mpaka leo. Anaweza kutwambia shilingi ngapi zimelipwa na shilingi ngapi hazijalipwa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Kwanza kuunda kamati napenda kunmhakikishia Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba kamati hiyo ipo na inaendelea kufanya kazi hiyo ya kuyabaini mashamba yote yale ambayo hayajatambuliwa, ambayo yameshatambuliwa, ambayo yana matatizo ya uridhi, yenye matatizo ya uimiliki na kadhalika. Kwa hiyo, kamati ipo na inafanya kazi nadhani hakuna haja tena ya kuunda kamati nyengine kwa sababu hizo kamati zipo.

b) Kuhusu madeni ni kwamba, madeni kwa wale ambao walishughulikia tulijibu swali hili nakumbuka katika Baraza hili hili na kikao hiki kinachoendelea, kwamba wale wanaodai madeni kwa sababu kuna waliokuwa wanahudumia mashamba kwa viwango tofauti, wale kuna baadhi yao wameshalipwa na wengine tupo kwenye mkakati wa kuwatafutia malipo yao wapewe.

Kwa mfano, wale ambao wameyahudumia vizuri sana mashamba yale wanapata asilimia 40 ya pato lilopatikana kwenye shamba hilo. Wale ambao hawakuhudumia vizuri lakini yanaridhisha walipata asilimia 30, na wale ambao hawakuhudumia vizuri

walipata asilimia 20, na wale kabisa kabisa tena ah wanayatumia lakini hawafanyi vizuri nao walipata asilimia 10. Kwa hiyo, viwango hivyo tutaendelea kuvitumia kumaliza kufidia wale wote ambao hawajalipwa mpaka sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, nakuhakikishia kama kuna madeni yoyote basi madeni hayo yatalipwa, kwa sababu lengo la serikali sio kumdhulumu mwananchi wake, lengo la serikali ni kumpa haki yake mwananchi kila ambaye anastahiki kupata haki hiyo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 63 na 37 Mhe. Naibu Waziri nafikiri hakulifahamu swali langu, yale mashamba yamekodishwa kwa wafanyabiashara na wafanyabiashara hao wameingia mitini hawakuonekana. Nimetoa taarifa hapa kuna pesa zinadaiwa nilikuwa namuuliza zile pesa je wameonekana waliokodishwa na shilingi ngapi zimelipwa na ngapi hazijalipwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. *(Makofi)*

Aidha, nimshukuru Mhe. Mwakilishi, kwanza nataka nimuhakikishie kwamba serikali iliunda Kamati Maalum ya Baraza la Mapinduzi wakiwemo mawaziri mbali mbali kusimamia kwa undani juu ya hilo zoezi zima la mashamba ya karafuu ambalo limeanzia Pemba na litaendelea na hapa Unguja.

Nia na madhumuni ni yale yale aliyosema Mhe. Mwakilishi kuhakikisha kwamba mashamba haya yanakuwa katika mikono rasmi kwa utaratibu mzuri uliowekwa na serikali. Hakukuwa na nia hata kidogo ya serikali kuwanyanganya wananchi mashamba, lakini ilikuwa inatafuta utaratibu mzuri wa kuwawezesha wananchi hawa kwa mashamba hayo kwa utaratibu uliopo wa kisheria na waweze kutumia kwa mujibu wa taratibu za kisheria, kwa sababu mbali mbali zilizojitokeza huko nyuma ya kutumika visivyo, hivyo ni dhamira njema ya serikali. Kwa hiyo, tunataka tuwaondoe wananchi wasi wasi na wale wote ambao wana haki zao katika mashamba hayo, serikali inalisimamia vizuri zoezi hili na kila mmoja atapata haki yake.

Kwa hivyo, tuondoe mashamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili na wananchi wote. Vile vile, wale waliokodishwa mashamba hatua mbali mbali zinachukuliwa kuhakikisha wanalipa kodi hizo walizokodishwa. Kwa kweli, hakuna atakayekimbia kulipa kodi hiyo, taratibu za kisheria zitachukuliwa na wote watalipa kodi hiyo. Nataka kumuhakikisha Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi kwamba utaratibu upo na wote watalipa kama ilivyopangwa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naipongeza sana serikali kwa lengo zima la kutaka kuyatambua mashamba haya na kurudi serikalini lakini baadae inakuwa na nia njema kuwarejeshea wananchi. Hilo naunga mkono kwa asilimia mia moja kwa juhudi za serikali kuhakikisha hilo, kwa sababu ilikuwa lengo lake ni kuyatambua na kuwarejeshea wananchi, nina imani watarejeshewa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wale wananchi ambao walikuwa wakishughulikia mashamba yale na tayari waliambiwa kwamba watalipwa ile asilimia yao, nataka kujua watalipwa baada ya kulipwa hizi pesa ambazo zimekopeshwa au watalipwa lini ili wananchi wapate kufahamu na sisi kule majimboni tukienda tuweze kuwafafanulia. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na nimshukuru Mhe. Mwakilishi kwa swali lake la nyongeza. Kama nilivyosema serikali inachukua kila hatua kuhakikisha wananchi hawa wanapata haki zao, wale wote ambao waliyasimamia mashamba haya na wakaahidiwa kwa mujibu wa utaratibu basi wasiwe na wasi wasi wowote utaratibu umeanza na watalipwa fedha zao hata kama hawa ambao wanadaiwa hawajalipa bado serikali italipa fedha hizo. *(Makofi)*

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kuniona tena na kunipa ruhusa ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo inaongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuwa na uhakika wa kutokutaka kuwanyanganya wananchi wake mashamba haya ya mikarafuu.

Mhe. Waziri kwa kuwa umetupa takwimu mzuri za idadi ya mashamba ambayo yanajuulikana katika kisiwa cha Pemba. Je, kwa sababu Unguja kuna mashamba ya mikarafuu tupe takwimu za Wilaya za Unguja ni mashamba mangapi yamejuulikana ya serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, namuomba arudie swali lake kwa sababu sikumsikia vizuri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa swali la Mhe. Mwakilishi linahusu takwimu ningeomba atupe nafasi swali hili lijibiwe kwa maandishi na takwimu zote ataletewa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 146

Mpango wa Kugawa Maduka ya Biashara Jumba la Treni Darajani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Wakati wafanyabiashara wa muda wa Jumba la Treni Darajani wanahamishwa, ili kupisha ujenzi wa jengo jipya la biashara walipewa ahadi kuwa watarejeshwa katika sehemu zao ujenzi

utakapokamilika. Hata hivyo, ujenzi unaonesha kuwa idadi ya maduka imepungua kuliko ile ya awali na kuna hofu kuwa wengine wanaweza kukosa nafasi zao.

(a) Je, serikali itafanya utaratibu gani kuhakikisha wafanyabiashara wale wanapata haki zao za kurejeshwa kwenye maduka yao bila kukosa.

(b) Kuna taarifa kuwa baadhi ya vigogo wameshafanya mipango ya kujipatia sehemu za biashara wakati hawakuwamo tangu mwanzo. Je, hili likoje.

(c) Endapo walengwa watakosa kurejeshwa pale hatua gani zitafuata kuwapatia haki zao.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu swali Nam.146 la Mhe. Mwakilishi lenye vifungu (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo ya jumla kama ifuatayo:-

Mhe. Spika, ili kulinusuru jengo la Jumba la Treni (*Chawl Building*) ambalo lilikuwa katika hali mbaya sana, serikali ilifanya maamuzi kuwa jengo hilo lenye hadhi ya kihistoria ya daraja A lifanyiwe matengenezo makubwa ili kulihami. Kazi hiyo ilikabidhiwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) kwa makubaliano kuwa baada ya matengenezo itakodisha sehemu zake za biashara ili *ZSSF* iweze kurejesha fedha zake ambazo ni fedha za wanachama. Serikali pia iliamua kuwa baada ya matengenezo hayo, fursa ya kwanza ya kutumia maeneo hayo itatolewa kwa wafanyabiashara waliokuwepo awali pindi wakikubaliana na masharti mapya ya *ZSSF*. Wakati matengenezo hayo yanakaribia kukamilika, viongozi mbali mbali wa serikali na *ZSSF* walikutana na wafanyabiashara hao na mkutano huo ulifanyika tarehe 8 Machi, 2018 na kuwahakikishia kwamba bado serikali ina dhamira ya kutekeleza ahadi yake kwao, kupitia masharti mapya.

Naomba nisisitize kuwa hii ni fursa, na sio haki kama alivyoisema Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nijibu swali lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali itatangaza ukodishwaji wa maeneo yote ya biashara katika jengo hilo, na wafanyabiashara waliokuwepo awali ndio watakaopewa kipaumbele.

(b) Hakuna mtu yeyote aliyepatiwa eneo katika jengo hilo hadi sasa, kwa hivyo taarifa kuwa kuna wakubwa wamefanya mipango ya kupata maeneo sio sahihi na yeyote atakayehitaji atapaswa kufuata utaratibu wakati utakapofika.

(c) Kwa mujibu wa maelezo niliyokwisha kuyatoa hakuna mlengwa ambaye atakosa eneo la biashara iwapo atakubaliana na masharti na taratibu zitakazopangwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri niipongeze sana serikali kwa juhudi iliyochukua kunusuru jengo lile kwa dhati kabisa.

(Mhe. Waziri, michoro imezingatia vipi uhalisia wa jengo hilo, kuna sehemu hazikurudi katika ujenzi ule. Kuna kipenu njia ya Msikiti wa Darajani hakikurudi na kipenu kile kilikuwepo mwanzo kabla ya Mji Mkongwe kuanza. Kipenu cha mbele kule Marikiti kimerudishwa na kuna sehemu pale wafanyabiashara wamekosa maduka yao na milango imepungua.

(a) Je, watapelekwa sehemu gani katika jengo lile na katika milango sita mpaka minane ina upungufu, watapelekwa sehemu gani na lile jengo sababu gani hakikurudishwa kipenu kile, kimoja kimerudishwa na kimoja hakijarudishwa. Utaratibu gani ulizingatiwa au mchoro wa aina gani.

(b) Mhe. Naibu Spika, nataka kujua gharama halisi ya jengo lile Kampuni ya *CRJE* imejenga kwa gharama ya kiasi gani. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, hili swali tayari nimeshalitolea maelezo katika kikao hiki. Ni kwamba jengo halikubadilika lakini kuna kipenu ambacho ni sehemu ndogo sana ambacho kilifanyiwa marekebisho na marekebisho yaliyofanywa ni kwamba katika eneo la upande wa Kaskazini ya jengo kulikuwa na duka la Calipso, lakini pia kulikuwa na dula la *perfume*. Kwa hiyo, nilisema hapa kwamba eneo hilo la duka la *perfume* liliondolewa ili kuweza kupisha ujenzi wa ngazi ya kwendea kwenye *apartment* za juu. Hayo ndio mabadiliko yaliyofanyika lakini pia upande wa Marikiti kuna mlango mmoja ulitolewa kwa ajili ya kuweka sehemu ya *ATM*. Maelezo hayo nilikwisha kuyatoa lakini maeneo mengine yote yamebaki kama lilivyokuwa jengo lile, na huo ujenzi uliofanyiwa mabadiliko ulikuwa lazima ufanyiwe ili kuweka haiba nzuri ya jengo hilo. Vile vile liweze kufikika kirahisi katika sehemu za kati na sehemu za juu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na gharama nalo pia nishawahi kulitolea maelezo kwamba gharama kamili za ujenzi wote ni bilioni 11,242,489,155,000/- hizo ni gharama kamili za ujenzi huo na zinahusisha matengenezo kwa maana ya *main contract* lakini pia zinahusisha sehemu *services* zilizofanywa pamoja na kuweka *lift* mbili gharama za umeme na gharama za *plug***.**

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 63 na 37 kama kawaida. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alisema watapatiwa sehemu lakini wenyewe wamekuwa na wasi wasi na hivi sasa wamenunua redio kusikiliza jawabu hili na betri wametia mpya kupata jawabu. Hebu tuwekee sawa Kiswahili hiki watakwenda sehemu gani katika jengo lile lile ama juu au kati kati maana ni mwakilishi wa wananchi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza pale ndani kuna wamiliki watano hawa wana utaratibu wao, na mazungumzo yanaendelea jinsi ya kufidiana wamiliki watano. Kuna wamiliki wawili wanamiliki maduka peke yake, watatu wanamiliki maduka na

apartment hawa wana mazungumzo yao. Lakini wale walikuwa na maduka wao watapewa kipaumbele cha kwanza ndivyo nilivyojibu, na milango hivi sasa ya maduka jumla ni 53 kwa hivyo ukitoa milango 5 tutabaki na milango 48 itatosheleza kwa hao waliokuwepo na wengine watakaohitaji.

Nam. 97

Ajira za Ualimu

Mhe. Ali Khamis Bakar (Kny: Mhe. Omar Seif Abeid) – Aliuliza:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iliajiri walimu mwezi wa Februari, 2018 kutokana na kuwepo kwa tatizo kubwa la upungufu wa walimu.

(a) Je, kwa upande wa Pemba wizara imepanga kupeleka walimu wangapi kwenye kipindi hiki, ili kupunguza tatizo kubwa la walimu na kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wetu.

(b) Je, kwenye uajiri uliopita wizara iliajiri walimu wangapi kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 97 lenye vifungu (a) na (b) kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa wizara imefanya uajiri wa walimu katika vipindi mbali mbali katika mwaka wa fedha wa 2017/2018. Uajiri wa walimu umefanyika kwa skuli za Unguja na Pemba kwa mujibu wa taratibu za utumishi ambapo waombaji wa kazi walitakiwa kuwasilisha maombi yao ya kazi na vyeti vya masomo kwa Tume ya Utumishi Serikalini.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Wizara imepokea vibali vya ajira vya walimu na wafanyakazi wengine 1,112, kati yao Unguja ni 858 na Pemba ni 254. Hivyo, wizara imewaajiri na kuwapangia kazi walimu 247 kwa skuli za Pemba kwa mchanganuo ufuatao:-

Walimu wa cheti 94, Walimu Stashahada Sanaa 48, Stashahada Sayansi 25, Shahada ya Kwanza Sanaa 74 Shahada ya Kwanza Sayansi 4 na Kidato cha Sita 2.

(b) Katika kipindi cha Januari hadi Disemba, 2017 wizara iliajiri jumla ya walimu 66 kwa skuli za Pemba. Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikalini itaendelea na zoezi la uajiri wa walimu wengine kwa skuli za Unguja na Pemba kutokana na baadhi ya walimu kutimiza muda wao wa kustaafu. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini vile vile niipongeze Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutoa idadi hii ya walimu ambao wamepata uajiri na Mwenyezi Mungu ataijaalia kwamba skuli zetu hizi *inshaallah* zitapata walimu hawa ambao wameshapelekwa ili kuweza kupunguza yale mahitaji ambayo yanatakiwa katika skuli zetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Waziri Wilaya ya Micheweni ni miongoni mwa wilaya ambazo zina upungufu mkubwa wa walimu, na mara nyingi hutokea matangazo kama haya na vijana kuweza kuomba nafasi hizi za ualimu, lakini tu vijana pale ambapo wanaomba wanakuwa wanaanishwa kwamba ajira hizi zimetolewa kwa Wilaya ya Micheweni kwa mfano, lakini vijana wanakwenda kuomba nafasi zile na badala yake wakishakupata baada ya kama wiki au wiki mbili huhama. Je, wizara yako ina mpango gani wakuona kwamba suala hili inalisimamia ili kuweza kukidhi zile nafasi ambazo Wilaya husika imekusudia ili kupunguza mrundikano ule.

b) Katika kipindi hiki ambacho wameajiri. Je, Wilaya ya Micheweni imepata walimu wangapi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

(a) Kuhusu Wilaya ya Micheweni na wilaya nyengine yoyote, kwa sasa hatujaweka mgao maalum kiwilaya kwamba ajira hizi zinakusudia Wilaya ya Micheweni, hii Wilaya ya Mkoani zinakusudia wilaya nyengine. Lakini hata kama utakuweko utaratibu huo ajira katika Zanzibar haina mipaka mtu yeyote anaweza kuomba. Kwa maana hiyo basi, popote mtu inapotangazwa ajira na anatimiza sifa zinazotakiwa basi anaweza kuomba.

(b) Katika wakati huo Wilaya ya Micheweni tumeweza kuwapatia walimu 37. Lakini wakati mwengine kuanzia sasa wakati wowote kibali cha ajira kimeshatolewa tumepata ajira kama 71 juzi, nazo pia tukipata mgao Wilaya ya Micheweni itahusika. Ahsante.

Nam. 24

Utafiti wa Kuimarisha Shirika la *ZSTC* kwa Upande wa Tanzania Bara

Mhe. Mussa Foum Mussa – Aliuliza:

Shirika la *ZSTC* katika malengo yake ya mwaka 2017/2018 ni kufanya utafiti wa kupanuwa wigo wa biashara ikiwemo kuimarisha kituo cha *ZSTC* Dar-es-Salaam kwa biashara na Tanzania Bara.

(a) Je, Mhe. Waziri utafiti huo umefikia wapi.

(b) Je, kuna faida gani ya utafiti huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Shirika liliwapatia Chuo cha Usimamizi wa Fedha Chwaka kazi ya utafiti wa njia bora ya kuliendeleza Tawi la Shirika la *ZSTC* Dar-es-Salaam na tayari limeshawasilisha mapendekezo yake kwa shirika, na shirika limeshaanza kuyafanyia kazi mapendekezo hayo.

(b) Utafiti huo umeleta faida ya kugundua maeneo ambayo shirika linaweza kuyafanyia kazi mfano asali na bidhaa nyengine za kilimo kama kunde yanaweza kuleta tija kubwa kwa shirika ikiwemo kupeleka bidhaa zake inazozalisha kama mafuta ya mimea kuweza kuuzika kwa kiwango kikubwa. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kituo hiki cha Dar-es-Salaam kimefunguliwa kwa muda mkubwa sana kipo, na kwa kuwa kituo kinahitaji gharama kubwa ili kukiendesha.

Je, ni faida ipi nyengine iliyopatikana ukiacha hiyo ya utafiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe kwamba, kituo hiki pale Dar-es-Salaam kwa kweli ni kituo muhimu kwa sababu kama wizara tuna mkakati wa kukiendeleza. Faida kubwa iliyopatikana kwenye utafiti huu tumegundua kwamba utafiti umesema kuna mambo mengi ambayo kama kituo kinaweza kikafanya na yakaleta tija kwa maendeleo ya Zanzibar na wananchi wa Zanzibar.

Kwa mfano, utafiti umegundua uzalishaji wa maziwa kwa wananchi ambayo yanaweza yakauzwa katika viwanda inaweza ikaleta tija. Lakini kadhalika kule Shengejuu utafiti umegundua kwamba kunaweza kukaendelezwa kuzalishwa ile chumvi inayozalishwa na kupelekewa katika viwanda. Lakini tumegundua tunaweza tukazalisha asali kunde, chooko kama dengu na bidhaa mbali mbali za kilimo. Kama vile, *agroprocessing product* ambazo pia zinaweza zikazalishwa na yote haya yamesemwa na utafiti uliofanyika ahsante. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali sasa hivi alitaja viwanda Shengejuu na viwanda vyengine. Juzi aliulizwa swali kuhusu Kiwanda cha Soda cha Maruhubi. Je, bado kiwanda kile kinaendelea kufanya kazi hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali hilo siliruhusu, tayari maelekezo nimeshatoa na Mhe. Waziri alilitolea maelekezo vizuri. Tunaendelea.

Nam. 160

Taa za Kuongozea Ndege Usiku Uwanja wa Ndege Pemba

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Kwa kuwa Uwanja wa Ndege wa Pemba bado unahitaji kuendelezwa kwa kuboreshwa kwa miundombinu ya kufanyakazi usiku, lakini tayari umeshawekwa taa za kuongozea ndege usiku ingawa taa hizo haziwashwi na huenda siku ikitokea dharura taa hizo, pengine zisiwake au kutokea kwa changamoto nyengine.

(a) Je, taa hizo za kuongozea ndege tokea siku ya kuwashwa kwa majaribio zimeshawashwa mara ngapi usiku mzima ili kuona kuwa hakuna matatizo.

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kuziwasha taa hizo, ili zisije zikaharibika bila kutumiwa.

(c) Je, wizara imejipanga vipi kwa sehemu za nje ya uwanja kwa kuwekwa mataa na mambo mengine yanayohitajika, ili uwanja uwe uko tayari kwa wakati wowote.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 160 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, taa za kuongozea ndege zilizopo Kiwanja cha Ndege cha Pemba zinatoa huduma kuanzia saa 12:30 asubuhi hadi 12:30 jioni pale zinapohitajika na kwa hivi sasa taa hizo zinatumika nyakati za usiku panapotokea dharura.

(b) Mhe. Naibu Spika, utaratibu uliopo kwa mujibu wa miongozo, taa hizo huwashwa kwa majaribio kila siku mara mbili (asubuhi mapema kabla kufunguliwa kiwanja na jioni), kwa kupitia muongoza ndege na mafundi umeme waliopo zamu (*remote and local*).

Kuhusu kufanya kazi nyakati za usiku katika kiwanja hicho Mamlaka Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania zinaendelea na taratibu za kufanikisha huduma za usiku kwa kuazia kufikia saa nne.

(c) Mhe. Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kupitia wizara tayari imeweka taa katika maeneo ya nje ya kiwanja cha Pemba.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nimshukuru waziri kwa majibu yake mazuri. Mimi nina swali ya kwamba, nafahamu habari ya kiwanja cha ndege cha Pemba kwamba hakifanyi kazi usiku, lakini taa zake ni kwamba nazo zinazimwa.

(a) Naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba pamoja na kuwa uwanja haufanyi kazi lakini ni kwa nini taa zile zisingewashwa tu zikawaka kwa vile ni uwanja wa ndege ambapo

moja ni kwamba tunazijaribu kuwa zina uwezo wa kuwaka muda wote bila ya tatizo lolote.

(b) Naomba nimwambie Mhe. Waziri kwamba ukiachia umeme pale pana jenereta. Je, hili jenereta limeshafanyiwa uchambuzi ya kwamba lina uwezo wa ku-*operate* kiwanja kizima kile hasa kwa sehemu za *running way* kwa muda wa siku nzima bila ya kuwa na tatizo lolote.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mhe. Suleiman Sarahan Said kama ifuatavyo.

(a) Umeme ni kitu ambacho kinalipiwa na huwa kinatumika pale panapokuwa na mahitaji. Kuwasha taa usiku kucha wakati tuna uhakika hakuna ndege itakayokuja hayo ni matumizi mabaya ya fedha za serikali na pia hakutaleta tija katika kiwanja hicho. Tuna uhakika wa kwamba taa zinafanya kazi na pale pindipo itahitajika basi zitawashwa.

(b) Kuna jenereta, ambalo lililonunuliwa linalingana na mahitaji ya uwanja wa ndege husika, kila jenereta linanunuliwa kwa ukubwa wa sehemu na *kilowatt* ambazo zinatakiwa kutumika, lilioko kwenye kiwanja cha Pemba limenunuliwa na linajulikana kwamba litakidhi mahitaji pindipo patahitajika kuwashwa taa usiku.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na nampongeza sana Mhe. waziri kwa majibu yake ya msingi. Lakini haoni haja kwamba angefanya *rehearsal* kila baada ya mwezi mmoja angalau zile taa zikawa zinawaka, kusudi mambo ya *electronics* haya na mambo ya umeme ni mambo ya kuwasha kila siku, pengine siku ya haja ya kuwashwa mtambo umekataa na pengine kutokana na muda mrefu kuwa hazijawashwa. Je, atakubali kupokea ushauri huo awe anafanya hata baada ya mwezi mmoja kuwashwa na kuhakikisha kwamba jambo lile linafanya kazi sawasawa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, uwanja wa ndege una mafundi wa kuwasha taa na kuzima na wanaelewa taratibu za kuwasha taa na kuzima na kuzifanyia majaribio kila yanapotakiwa na ndio maana wako pale asubuhi na usiku kufanya majaribio hayo.

Suala la kuwasha taa usiku kucha pale itakapobidi uwanja wa ndege utumike usiku kucha hayo yatafanyika, lakini kwamba taa zinafanya kazi kwa kipindi ambacho zinafanyiwa majaribio mpaka dakika hii hatujapata taarifa ya kwamba uwanja una matatizo.

Nam. 182

Matatizo ya Mawasiliano ya Simu Kisiwani Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, lakini nimuombe Mhe. Naibu Waziri anapojibu sauti yake kidogo iwe kubwa hatusikii humu ndani, ainamie *microphone* hiyo. Naomba majibu ya swali Nam. 182.

Makampuni ya simu yanayofanya kazi Tanzania moja ya masharti waliyopewa ni kufikisha huduma kwa wananchi maeneo yote, kinyume chake wananchi wa Pemba hasa maeneo ya Wesha wamekuwa wakipata tatizo la mawasiliano ya simu kila mara.

Je, hatua gani zitachukuliwa na serikali kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano ya simu zinapatikana katika kisiwa cha Pemba bila matatizo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub abadilishe kauli yake mimi ni waziri kamili na si Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliyesimama mbele yetu ni Mhe. Waziri na sio Naibu Waziri. Kwa hivyo, naomba ufute kauli yako na kusema Mhe. Waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nafikiri Mhe. Waziri hakusikia hizi *microphone* zina mataitzo tukafuate *hansard*, namuheshimu sana mimi sikumwambia Naibu Waziri, hakusikia.

Mhe. Naibu Spika: Na wewe hukusikia aa! Hata na mimi nimesikia umesema Naibu Waziri. Kwa hivyo, naomba ubadilishe tu hiyo kauli useme waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Basi namuombea dua afike mpaka Makamu wa Pili wa Rais Mungu akipenda *Insha Allah*.

Mhe. Naibu Spika: Ninachokisema useme waziri hayo mengine ni ya kwako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Narekebisha kauli.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, kawaida unasema ni waziri ndio kawaida. Mhe. Jaku Hashim Ayoub wewe ndiye unaezitumia sana kanuni humu ndani na unazifahamu vizuri sana, lakini likija kwa upande wako huwa hutaki kuzitumia kanuni. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Waziri, Dkt. Sira Ubwa Mamboya. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante namshukuru kwa kunitambua kwa jina na kwa nafasi yangu. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 182 kama ifuatavyo:-

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri azidishe sauti kidogo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, tunaomba sauti kidogo usogee karibu ya kipaza sauti.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, matatizo ya mawasiliano katika kisiwa cha Pemba yanafahamika na serikali zetu zote mbili, ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kutokana na hali hiyo, ndipo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imeanza kufanya ukaguzi kwa Mikoa yote ya Pemba na kugundua maeneo kadhaa ambayo yana matatizo ya mtandao ya simu (*Mobile Signal Status*).

Mhe. Naibu Spika, kufuatia ukaguzi huo pia kumegundulika kuwa yapo maeneo ambayo hayana mawasiliano kabisa na yanahitaji kujengewa minara.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kuyataja maeneo hayo. Maeneo hayo ni Ngomeni na Mgelema katika Wilaya ya Mkoani, Mzambarao Takao, Tungamaa, Weni, Limbani, *Sea View Street*, Kisiwani kwa Bint Abeid na Maziwani kwa Wilaya ya Wete. Maeneo mengine ni Mjananza, *Ngezi Forest*, Makangale, Tondooni – Makangale, Kilindini, Shumba Viamboni, Sizini, Kinazini, Wingwi kwa Zakuani na Njuguni katika Wilaya ya Micheweni na maeneo ya Wesha na Tumbatu – Gombani kwa Wilaya ya Chake Chake.

Aidha, baadhi ya maeneo yameonekana yana mawasiliano mabaya (*weak signal*). Mawasiliano yapo lakini hayana nguvu ya kustosha. Maeneo hayo ni Chokochoko, Temi, Kalani, Makhudusi, Kengeja na Ukutini katika Wilaya ya Mkoani, Makongeni, Kinazini – Mtambwe, Gando, Shengejuu na Kiungoni katika Wilaya ya Wete. Maeneo mengine ni Kipange, Kiuyu Mbuyuni, Tumbe na Dodeani katika Wilaya ya Micheweni na eneo la Mkanjuni katika Wilaya ya Chake Chake.

Mhe. Naibu Spika, katika kutatua matatizo hayo wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa *UCSAF* pamoja na *TCRA* itashirikiana na wataalamu kutoka makampuni ya simu, ili kujenga minara ya mawasiliano katika sehemu zinazostahiki na kuongeza vifaa kwa sehemu zenye mawasiliano dhaifu (*weak signal)*. Katika kuhakikisha hayo yanafanyika tayari baadhi ya makampuni ya simu wameshapewa kazi ya ujenzi wa miundombinu ya minara ya mawasiliano na *UCSAF*. Aidha, wizara imeshapokea maombi hayo ya ujenzi na inaendelea kuratibu suala hilo ili kuondoa matatizo ya mawasiliano kwa wananchi wa kisiwa cha Pemba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana tena Mhe. Waziri, nimwite tena kwa mara ya pili Mhe. Waziri Dokta Sira Ubwa Mamboya wa Jimbo la Ikulu kwa kukiri kuna matatizo katika sehemu za Pemba na huu ndio ukweli ulivyo.

(a) Je, kampuni zinazotoa huduma kwa wananchi wanaomiliki mitandao yao wanafidiwa vipi kwa kukosa huduma bora kama wateja.

(b) Pemba ni sehemu ya Zanzibar *TCRA* inasimamia vipi kuwepo uwiyano wa huduma bora baina ya visiwa viwili hasa kwa kuzingatia huduma za mawasiliano ni huduma muhimu kwa wananchi na kwa maendeleo ya nchi.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, athari za kutokupata mawasiliano zinafahamika kwa sababu sasa hivi katika kitu muhimu ulimwengu wa leo ni

mawasiliano na kwa kulitambua hilo ndio maana pakafanyika huo ufumbuzi wa kuweza kutambua. Kwa sababu wananchi walilalamika na kazi ikafanyika ili kuweza kuyatambua hayo maeneo. Baada ya kuyatambua maeneo hayo ndio hiyo kazi inayoendelea sasa hivi ya kutaka kujenga minara. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba minara itakapojengwa na kwa sababu maeneo yanafahamika tutaweza kusahihisha yale matatizo yaliopo na wananchi wote watapata mawasiliano kama wanavyostahiki. Kwa hivyo, naomba tu Mhe. Mwakilishi awe na imani kwamba yatakapofanywa matengenezo na wale ambao wamekosa mawasiliano wastahamili kidogo matengenezo yatengenezwe, minara ijengwe na baada ya hapo mawasiliano yatapatikana. Hilo la kwanza.

La pili, *TCRA* inafanya kazi kwa karibu tena nchi nzima Zanzibar, Unguja na Pemba na Tanzania kwa ujumla. Vile vile, wao pia ndio mmoja katika watu waliokuwepo hapa katika kikao chetu tukakubaliana. Kwa hivyo, *TCRA* pamoja na huyo *UCSAF* ni watu ambao wamefanya kazi kwa pamoja na tatizo hilo wanalitambua. Katika kutengeneza hiyo minara mashirikiano baina ya *UCSAF* na *TCRA* yatakuwepo na watahakikisha kwamba jambo hilo linafanikiwa.

Nam. 81

Nyumba za Wizara ya Afya

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kumekuwa na madai kuwa Wizara ya Afya wanamiliki nyumba za wafanyakazi zilizopo Micheweni na Mombasa Unguja.

(a) Je, Wizara ya Afya wanazitambuwa nyumba hizo.

(b) Je, nani wanaishi katika nyumba hizo.

(c) Zipo nyumba za Wizara ya Afya Wete na Chake Chake zinadaiwa kukaliwa na Wizara inayohusika ya Ardhi. Je, kwa nini nyumba hizo hazirejeshwi Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Afya inamiliki nyumba za wafanyakazi na ni katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba ikiwemo Micheweni na Mombasa Unguja.

(a) Mhe. Naibu Spika, napenda kulithibitishia Baraza lako tukufu kwamba wizara yangu inazitambua nyumba hizo na katika jitihada za kudhibiti rasilimali zake hivi sasa inaendelea kufanya zoezi la uhakiki wa mali za wizara ikiwemo nyumba hizi.

(b) Katika uhakiki huo, wizara ilibaini kwamba kuna baadhi ya watu ambao wanaishi katika nyumba hizo sio madaktari wala wafanyakazi wa Wizara ya Afya. Aidha, uhakiki umebaini kuwa baadhi yao wamethubutu kubadilisha umiliki kutoka ule wa wizara wa awali na kuwa wao binafsi.

(c) Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la nyumba zinazodaiwa kukaliwa au kuchukuliwa na wizara nyengine ikiwemo Wizara ya Ardhi kama alivyouliza Mhe. Mwakilishi. Wizara yangu tayari imeshawasiliana na Shirika la Nyumba kwa madhumuni ya kuzifatilia na kufanya utaratibu wa kuzirejesha nyumba hizo, ili ziendelee kuwa na umiliki wa Wizara ya Afya. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutokidhi suala la msingi kama nilivyouliza naomba kumuuliza maswala madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Naibu Waziri umekiri kwa baadhi ya watu wanaishi katika nyumba hizo sio madaktari waliingia vipi katika nyumba hizo na lini wataondoka.

(b) Idadi ya watu waliovamia nyumba hizo sio madaktari wako wangapi Unguja na Pemba wako wangapi. Jumla zote nyumba ngapi za Unguja na Pemba na wanalipa wapi fedha za kodi katika nyumba hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu wameingi vipi Mhe. Naibu Spika, na lini wataondoka. Hawa waliingia kutoka na baadhi yao wengine hatujajua utaratibu wameingiaje. Lakini baadhi yao tumegundua kwamba ni familia za waliokuwa madaktari baada ya madaktari wale kustaafu nyumba zile hawakuzirudisha wengine wazee wao wameshakufa wanaoishi humu ni watoto.

Lakini lini watatoka katika nyumba hizo nimekwambiwa katika jibu langu la msingi kwamba utafiti huu unaendelea kuchukuliwa na baada ya kufanya utafiti tutafanya maamuzi. Kwa hiyo, nakuhakikishia kwamba lengo la Wizara ya Afya na serikali kwa pamoja ni kuhakikisha nyumba hizi tunazimiliki wenyewe na zitumike kwa manufaa ya madaktari pamoja na wafanyakazi wa wizara.

(b) Mhe. Naibu Spika, kuhusu idadi yao utafiti bado unaendelea. Kwa hiyo, utakapomaliza utafiti huu ndio tutajua idadi yao hasa ni wangapi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu kuuliza swali dogo sana la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Spika, serikali ina tatizo la upotevu wa mali za umma, lakini vile vile kuna tatizo kubwa sana la makabidhiano ya mali kutoka utawala mmoja kwenda utawala mwengine. Vile vile kuna tatizo la Hatimiliki za Mali za Serikali, pia kuna tatizo la mali kutoingizwa katika *asset*

register yaani Kumbukumbu za Mali ya Serikali. Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri.

(a) Je, walipoingia madarakani katika Wizara hii ya Afya walipata kukabidhiwa kwa uhalali nyumba hizi.

(b) Nyumba hizi zinahatimiliki na zimo katika *asset register*. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli alivyosema Mhe. Mjumbe kwamba kuna tatizo katika makabidhiano ya hati na baadhi ya vifaa au mali za wizara wakati unapomaliza utawala mmoja kuna utawala mwengine. Hili serikali imeliona na katika hii hatua ambayo nimeieleza katika jawabu langu la mwanzo la kufanya uhakiki wa mali ni baada ya kugundua kwamba kuna tatizo hilo na sasa inabidi tujirekebishe.

Kwa hiyo, napenda kukueleza kwamba hili tatizo kweli tumelibaini na tumeliona kwamba ni tatizo wenzetu wa mfumo uliopita walikuwa wanakabidhiana mambo yote sisi tunakabidhiana tu baadhi ya mambo na baadhi ya mambo ukishakuingia wewe mwenyewe unayatafuta kama kiongozi na kuyabaini na kuyatambua na kuyatumia. Kwa hiyo, hili ni tatizo tumeliona na tunalifanyia ufumbuzi kwa kufanya uhakiki wa mali zetu mbali mbali.

(b) Lakini kuhusu la pili Mhe. Naibu Spika namuomba Mhe. Mjumbe anikumbushe kidogo swali la pili limenipita.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, swali la pili nilikuwa naulizia kwamba nyumba hizi zina hatimiliki na je, zimo ndani ya *asset register* la Wizara ya Afya. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, kwamba nyumba hizi zina hatimiliki na zimo ndani ya *asset register* na ndio itakayotuongoza na kuweza kuzibaini na kuzifahamu, ili tuweze kuzirudisha tena katika umiliki wetu.

Nam. 126

Matibabu kupitia Madaktari wanaotoka Nje kwa Muda Mfupi

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Kny. Mhe. Suleiman Sarahan Said) - Aliuliza**:**

Kumekuwa na utaratibu wa madaktari wanaotoka nje kuja kutibu kwa muda mfupi hasa opresheni na madaktari hao huondoka baada ya muda mfupi.

(a) Je, mgonjwa aliyefanyiwa operesheni na madaktari hao wa muda mfupi, ikitokezea tatizo baada ya daktari kuondoka Wizara inafanyaje. Hasa kwa kuzingatia kuwa daktari huyo aliyefanya operesheni, ndiye anayejua vizuri zaidi tatizo la mgonjwa.

(b) Je, kama mgonjwa ana "*special*" operesheni kwa daktari maalum na hayupo tena, Wizara inamsafirisha mgonjwa kwenda kwa daktari au daktari analetwa.

(c) Je, yameshawahi kutokea matatizo kwa madaktari hao katika kufanya opersheni kama kulitokea ni operesheni ngapi na vipi wizara ilizimaliza.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 126 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Afya Zanzibar tunao utaratibu maalum wa kupokea madaktari kutoka nje ya nchi kuja kushirikiana na madaktari wetu kwa ajili ya kutoa matibabu ya muda mfupi yaani (kambi) ikiwemo operesheni.

(a) Kikawaida huduma hizi za matibabu ya kambi za muda mfupi huratibiwa na madaktari wetu kabla ya kuwasili kwa madaktari wa kigeni na matibabu hutolewa kwa ushirikiano mkubwa kati ya madaktari wetu na wageni. Aidha, mratibu huandaa mpango wote wa kambi na ufuatiliaji wa wagonjwa kabla ya kufika kwa madaktari wa kigeni. Hivyo, madaktari wenyeji na wasaidi wao walioshiriki katika matibabu na operesheni hizo wanao uwezo mkubwa wa kufuatilia wagonjwa hao hadi kupona kwao.

(b) Kwa vile operesheni zinafanywa kwa mashirikiano baina ya madaktari wa kigeni na wenyeji na endapo litajitokeza tatizo wakati madaktari wa kigeni wameshaodoka, madaktari wenyeji wanao uwezo mzuri wa kutatua tatizo hilo kwa vile walishirikiana katika kufanya operesheni hizo kuanzia mwanzo hadi mwisho.

(c) Katika miaka ya mwanzo ya kambi za operesheni ya ubongo, iliwahi kutokezea kwa mgonjwa mmoja ambae alikuwa na uvimbe mkubwa sana ambapo madaktari wetu waliwasiliana na madaktari wa kigeni na kwa pamoja walikubaliana namna ya kumpatia matibabu na hatimae mgonjwa huyo alipona. Aidha, wizara imechukua hatua za ziada kwa kusomesha madaktari katika fani hiyo na kujenga jengo maalum kwa ajili ya huduma za matatizo ya ubongo na mgongo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa uchambuzi nzuri wa maelezo yake.

Naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba tuna madaktari bingwa lakini bado kila kukicha na hata sisi tuliokuwa tuna uwezo wetu mdogo mdogo ni kwamba lazima tunakwenda kuanzia Dar-es-Salaam kwa matibabu au tunakwenda nje nchi ikiwemo kama India na hapa tuna madaktari bingwa.

Lakini cha msingi ni kwamba tumezungumzia suala la operesheni zinazofanyika katika hospitali zetu.

(a) Je, serikali kutokana na matatizo haya yanayojitokeza na kuona kuna kasoro ya madaktari wetu kwamba bado hawajafikia viwango vya uhakika katika kubitu mradhi sugu au maradhi makubwa sana. Serikali ina mpango wa kila sekta fulani kuleta daktari bingwa ili kuja kusaidiana na madaktari wetu.

(b) Kutokana na changamoto hizo ulizozisema za kwamba madaktari wale wanaopita kwenye *camp* ya kufanya operesheni mara moja umenitolea mfano kwa mtu aliepona. Je, hakuna mtu aliepata matatizo au aliekufa katika hoja ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nikiri kwenye Baraza letu tukufu hili kwamba ni kweli tunao madaktari bingwa na ni madaktari bingwa kweli kweli na licha ya nguvu za madaktari hawa wenyeji ambao tunao. Lakini pia tuna madaktari bingwa kutoka kwa nchi za wenzetu ambao wanatuunga mkono kwa mfano Cuba na China wanatuunga mkono vya kutosha na operesheni nyingi zinafanyika. *(Makofi)*

Nilikuwa naomba tu kueleza Baraza lako kwamba ile kuja madaktari wakapiga kambi hapa wakafanya utibabu pamoja na uperesheni mbali mbali si kama kwamba madaktari wetu hawawezi, isipokuwa ni mpango maalum ambao wameuandaa madaktari wa nchi mbali mbali kutoa misaada kwa baadhi nchi zikiwemo nchi zetu hasa kutokana na kwamba nchi yetu ina mahusiano mazuri na nchi nyingi. *(Makofi)*

Sasa madaktari wale wanapokuja hapa operesheni zile ambazo wanazifanya hapa madaktari wetu pia wanaweza na ndio maana wanashirikiana nao kuanzia mwanzo hadi mwisho. Baadhi ya madaktari wetu niwathibitishie kwamba wamesoma pamoja na hao madaktari ambao wanakuja na kufanya na matibabu hapa. Kwa hiyo, wanaweza kabisa na hichi kitendo cha kwamba wa hapa wagonjwa wanatoka kwenda Dar-es-Salaam lakini hata sisi tunapokea wagonjwa kutoka Kenya, Dar-es-Salaam kutoka nchi nyengine wanakuja hapa na wanafanyiwa operesheni na madaktari wetu Wazalendo wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba mjenge imani kwamba madaktari tunao lakini huu ni utaratibu maalum. Wakati wengine huwa mgonjwa mwenyewe huwa haridhiki kufanyiwa hapa katika tatizo lile anataka atoke nje ende katika sehemu nyengine. Kwa hiyo, akiomba vile anapatiwa nafasi au pengine huwa kuna kifaa ambacho kule wanakifata ni urahisi zaidi kukipa kukalimisha operesheni ile kwa hiyo wanamuandikia ili aende kule kufanyiwa operesheni.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu swali (b) naomba arejee Mhe. Mjumbe.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nilimuuliza kwamba amenitolea mfano kutokana na operesheni zilizofanyika kulikuwa na mmoja alikuwa na matatizo ya ubongo, lakini baadae yile mtu

akafanyiwa matibabu fulani mpaka akapona. Nikamuuliza amenipa mfano wa mtu aliepona katika operesheni zinazofanyika hakuna mtu aliekufa au aliepata matatizo kama hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Naibu Spika, kufa ni wajibu, kwa hiyo nakuthibitishia kwamba wapo ambao wamefanyiwa operesheni na wengine ahadi yao Mwenyezi Mungu siku zimeshafika wakafariki wapo.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona tena na kunipa nafasi hii ya kuuliza suala dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri pamoja na majibu mazuri uliyoyatoa marudia tena kuipongeza Wizara ya Afya kwa huduma zake nzuri ambazo inaendelea kuhakikisha kwamba wananchi wetu wa visiwa hivi viwili wanapata matibabu mazuri.

(a) Lakini kwa kuwa operesheni hizi zinafanywa na madaktari wa kienyeji na waganga hawa wa kigeni wanaokuja nchi kwetu nataka nijue ni vipi Wizara ya Afya imejipanga kuhakikisha kwamba huduma baada ya upasuaji yaani *Post Operative Management* zinapatikana sahihi kwa wagonjwa wetu hawa ukilinganisha kwamba tuna upungufu mkubwa wa wauguzi wa uhakika ambao wamesoma fani hiyo ya kuuguza wagonjwa hawa ambao wanafanyiwa matibabu baada ya operesheni.

(b) Hata vifaa vyenyewe vya upasuaji vinakuwa ni tabu mfano hata katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja hapana kitu kinachoitwa *Sterilization Unit* ni kitengo ambacho kinapika vile vyombo vya kufanyia *dressing* baada ya kufanyiwa operesheni.

Je, wizara yako imejipanga vipi kuhakikisha *unit* ile ya Hospitali ya Mnazi Mmoja inafanyakazi kisawa sawa pamoja na vituo vyengine vya afya au hospitali nyengine ndogo ndogo, ili kuboresha huduma hizi za upasuaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Hamad Abdalla Rashis kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, huduma hizi baada ya operesheni huwa zinafanyika na zinafanyika vizuri sana na kwamba pamoja na uhaba wa wafanyakazi alioutaja, lakini huwa wanashirikiana kwa kiasi kikubwa na madaktari waliopo kuwashughulikia wagonjwa wale mpaka kuhakikisha kwamba wamepona vizuri.

Kwa hiyo, naomba uondoe wasi wasi kwamba wale wagonjwa watakuwa hawapati huduma baada ya kufanyiwa operesheni. Huduma zinapatikana vizuri kwa mashirikiano na madaktari wote.

Kuhusu swali b Mhe. Naibu Spika alilizungusha sana naomba anisaidie kidogo kulirudia.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, naomba urudie swali lako la b.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ukizingatia na majibu yako mazuri Mhe. Naibu Waziri narudia swali la b.

(b) Ni namna gani wizara imjipanga katika kuhakikisha kwamba vile vifaa vya kufanyia *dressing* katika mahospitali yetu kunakuwa na kitu kinaitwa *Sterilization Unit* ni kitengo cha kupika vile vifaa vya kufanyia *dressing* ili mgonjwa asipate uambukuzi kutoka kwenye vyombo ambavyo sio visafi na nikatoa mfano hata Hospitali ya Mnazi Mmoja ile *unit* ya kitengo kile haifanyi kazi kwa sasa na ni muda mrefu tu.

Vile vile, na hospitali nyengine ndogo ndogo za wilaya ni vipi wizara yako imejipanga kuhakikisha kitengo kile kinafanyakazi vizuri ili vile vifaa basi vinavyotumika kwa kuwatibu wagonjwa hawa baada ya upasuaji hawapati maambuzi ya maradhi mengine katika kufanyiwa *dressing*.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Hamad Abdalla Rashid swali lake la b kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi kikubwa kweli tulikuwa na upungufu mkubwa wa vifaa ikiwemo hizo *Sterilization machine.* Lakini sasa hivi tunazo ingawaje hazitoshelezi hata hapo unapopasema Mnazi Mmoja zipo lakini hazitioshelezi. Hata hivyo, tunategemea kupata mashine hizi kupitia bajeti yetu, tunategemea sana kununua mashine za kutosha za kupeleka Mnazi Mmoja Hospitali ya Wete, Chake pamoja na hospitali nyengine zote. Kwa hiyo, tatizo hili huenda likaishi muda si mrefu. (*Makofi*)

Hata hivyo, madaktari wetu kwa sababu ya kufahamu jinsi ya kutumia vifaa ambavyo wamevichemsha basi kuna mbinu mbadala wanazitumia kuhakikisha vifaa vile zinafanyiwa *sterilization* kabla ya kufanyiwa operesheni na baada ya kufanyiwa operesheni. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea na utaratibu mwengine ambao tumeupanga kwa siku ya leo nilikuwa nataka kutoa taarifa kuhusiana na uchaguzi mlioufanya jana wa kamati mbali mbali ambao ulitolewa taarifa yake hapo jana na Mhe. Spika, kwa ajili ya kuchagua wenyeviti pamoja na makamu wenyeviti.

Kwa hiyo, nitataja orodha ya wenyeviti na makamu wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ambazo zitaanza kufanyakazi rasmi kuanzia Juni 2018 hadi Juni 2020.

Kamati ya kwanza kabisa:

Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:
Mhe. Panya Ali Abdalla - Mwenyekiti
Mhe. Ali Suleiman Ali - Makamu

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:
Mhe. Machano Othman Said - Mwenyekiti
Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Makamu

Kamati ya Ardhi na Mawasiliano:

Mhe. Hamaza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Makamu

Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti
Mhe. Nassor Salim Ali	-	Makamu

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali *PAC:*

Mhe. Miraj Khamis Mussa	-	Mwenyekiti
Mhe. Shaib Said Ali	-	Makamu

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Mwenyekiti
Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Makamu

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii:

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Mwenyekiti
Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Makamu

Kamati ya Bajeti:

Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Mwenyekiri
Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Makamu

Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe:

Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Mwenyekiti
Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Makamu

Kamati ya Sheria Ndogo Ndogo:

Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Mwenyekiti
Mwanaasha Khamis Juma	-	Makamu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, nichukue fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa wote wajumbe wa kamati hizi kwanza kwa kufanya uchaguzi kwa utulivu kabisa na mashirikiano mazuri, lakini vile vile nichukue fursa hii adhimu kuwapongeza wale wote ambao wamepata nafasi ya kuwa wenyeviti pamoja na makamo wenyeviti. Kwa hivyo, niwaombe sana wote wafanye kazi kwa waledi kwa mashirikiano makubwa, ili waweze kutimiza yale malengo yetu ambayo ni kusimimia serikali hususan katika mapato na matumizi ya bajeti ambazo tunazipitisha hapa pamoja na kuishauri serikali na kuiongeza.

Vile vile, nichukue fursa hii Waheshimiwa Wajumbe mimi Mwenyekiti wa UWAWAZA nachukua fursa hii ya kuwapongeza wajumbe wanawake wote ambao wamepata fursa ya kuwa wenyeviti pamoja na kuwa makamo wenyeviti, hii imeweka historia kwamba kama tunakumbuka katika kamati zilizopita hakukuwa na mwenyekiti mmoja mwanamke. Na sasa

tumeona kwamba kwa kweli wanawake wamewiva na wapikika vizuri na wako tayari kufanya kazi kwa ajili ya kulitumikia taifa lao. (*Makofi*)

Ningewaomba wananchi huko nje wauone uwezo mkubwa walionao wanawake katika kufanya majukumu yao. Kwa hivyo, nawaomba hata tunapoingia katika chaguzi hizo watuchague wanawake kwa sababu tunaweza. Baada ya kusema hayo machache Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa nimpishe Mhe. Mwanaasha Khamis Juma aweze kuendelea na shughuli zinazofuata. Ahsanteni sana.

(Mhe. Mwenyekiti, Mwanaasha Khamis Juma hapa alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwengi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana katika Baraza lako hili tukufu tukiwa katika hali ya uzima wa afya na kuweza kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwachukua fursa hii kuwasilisha Ripoti ya Utelekezaji wa Kazi za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi katika kipindi cha Januari hadi Disemba 2017 kama ilivyoainshwa na kifungu Nam. 33 cha Sheria Namba 1 ya mwaka 2012 ya Kuzuia Rushwa Uhujumu Uchumi.

Majukumu na Mamlaka ya Kuzui Rushwa na Uhujumu Uchumi
Mhe. Mwenyekiti Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar imeanzishwa kwa kumujibu wa sheria nam.1 ya mwaka 2012 ambayo kifungu nam.13(1) imeanisha majukumu matatu makuu yafuatayo:-

1. Kufanya uchunguzi dhidi ya vitendo vya rushwa na kuhujumu uchumi.
2. Kushauri taasisi za umma na binafsi juu ya namna ya kudhibiti myanya ya rusha na uhujumu uchumi.
3. Kutoa elimu kwa umma kuhusu rushwa na uhujumu uchumi na atahri zake kwa lengo la kushirikisha jamii katika kuzuia rushwa na kuhujumu uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii inahusisha hatua zilizochukuliwa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi katika kukuza uelewa wa jamii juu ya athari za rushwa na uhujumu wa uchumi, katika kutekeleza jukumu hilo mamlaka imefanikiwa kutoa elimu kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara 24, vipindi vya redio 12, na sita vya *television* vilirushwa hewani kupitia vituo mbali mbali vya Unguja na Pemba. Vile vile, mamlaka imefanikiwa kuandaa machapisho 1,707 kama vipeperushi, mabango, na kalenda.

Sambamba na hilo mamlaka imefanikiwa kufanya mikutano katika skuli za Unguja na Pemba ili kukuza uelewa wa mambo ya rushwa na uhujumu uchumi, mikutano ambayo ilikwenda sambamba na uendeshaji wa klabu za wapinga rushwa katika skuli hizo. Semina mbali mbali kwa taasisi za umma na za binafsi 43 nazo zimetolewa. Vile vile, mamlaka imeshiriki katika

maonesho 18 ya Unguja na Pemba kwa lengo la kutoa elimu juu ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka imeendelea kiufanya udhibiti wa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi katika taasisi na idara mbali mbali za serikali udhibiti huo ulifanyika katika Kombe la Mapinduzi mwaka 2017 Baraza la Miji Wete, Hospitali ya Micheweni, Hospitali ya Wete, egesho la magari Darajani, Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mashamba ya karafuu. Imefanikiwa kuokoa jumla ya shilingi 169,028,120 milioni. Lengo la udhibiti huo ni kuweza kudhibi na kushauri juu ya njia bora ya kuzuia na upotevu wa mapato ya serikali na kupunguza vitendo vya rushwa katika utoaji wa huduma kwa wananchi kupitia hatua hizi kiasi kikubwa cha fedha ambacho kimesaidia kunyanyua uchumi na kuongeza pato zimeokolewa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2017 mamlaka imepokea tuhuma 187 kati ya tuhuma hizo 121 zimefanwa uchuguzi, tuhuma 20 zilifungwa baada ya mamlaka kujiridhisha kuwa tuhuma hizo hazikuwa na hoja za msingi. Majalada 37 yalifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya ushauri na hatua za kimahkama na majalada 5 yamefikishwa mahakamani.

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka imefanikiwa kufunga mitambo kwa ajili ya namba ya bure 113 huduma ambayo ilizinduliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Madhumuni ya huduma hii ni kurahisisha na kuharakisha kuripoti vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Utaratibu huu utaiwezesha mamalaka kuwa karibu zaidi na wananchi samabamba na hilo mamlaka imefanikisha uzinduzi wa mkakati jumuishi wa kitaifa wa kuzuia rushwa na uhujumu uchumi, mkakati huu ulizinduliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein tarehe 15 Machi 2018 ambapo baada ya kupitishwa kwake Mamlaka imeanza kutoa elimu kwa taasisi za serikali na binafsi ikiwa ni hatua ya kwanza kusimamia utekeleji huo.

Mhe. Mwenyekiti, tathmini ya sasa inaonyesha kuwa wananachi wameanza kupata uwelewa na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi lakini pia wananchi wengi wamepata ari na utayari wa kuripoti matokeo ya rushwa na uhujumu uchumi kupitia progamu ya kupiga simu nambari 113. Hata hivyo, mashirikiano yaliyopo baina ya *ZAECA* na taasisi nyengine yemesaidia sana kupunguza vitendo vya ruswha na uhujumu uchumi.

Mhe. Mwenyekiti nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako pamoja na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kupitia Ripoti ya Mamlaka ya Kuzia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ni matumaini yangu kwamba michango, maoni na maelekezo yao ya wawaheshimiwa yatasaidia sana katika kuimarisha utendaji wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi pamoja na kuimarisha misingi ya utawala bora Zanzibar. Wizara iko tayari kupokea ushauri, maelekezo na miongozo hiyo na inaahidi kwamba tutaifanyia kazi kwa nia ya kuifanya mamlaka kutumiza wajibu wake na majukumu yake ipasavyo, Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Waziri. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Utawala Bora na Idara Maalum, nakuona Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha maoni ya kamati kuhusu Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2017.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi, uhai na uzima kwa kutujalia afya njema na taufiki ya kuweza kukutana hapa leo kwa ajili ya muendelezo ya majukumu yetu muhimu ya kuishauri serikali pamoja na kuwakilisha wananachi wa Zanzibar katika kufanya maamuzi muhimu ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, aidha nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kutoa maoni ya Kamati ya Sheria Utawala Bora na Idara Maalum juu uwasilishwaji wa Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2017.

Mhe. Mwenyekiti, pia natumia fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuweza kuwasilisha vyema mbele ya baraza lako tukufu ripoti ya Mamlaka ya Kuzua Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kwa kipindi kifupi cha miezi 12. Ripoti hii inaakisi matokeo ya kazi nzuri zilizofanywa na mamlaka hii katika kukamilisha majukumu yao ya msingi kama Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar Namba 1 ya mwaka 2012 inavyoeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani za dhati kwa wajumbe na makatibu wa Kamati hii ya Sheria Utawala na Idara Maalum kwa Mashirikiano makubwa yanaoendelea katika kamati hii namuonesha ufanisi mkubwa katika kutimiza wajibu wao katika chombo hichi kitukufu katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe.Mwenyekiti, naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje wajumbe wa Kamati hii ya Sheria Utawala Bora na Idara Maalum kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Machano Othman Said - Mwenyekiti
2. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Wanu Hafidh Ameir Mjumbe
4. Mhe. Saada Ramadhani Mwendwa Mjumbe
5. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
6. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf - Mjumbe
7. Mhe. Ali Khamis Bakar - Mjumbe
8. Ndg. Ali Alawy Ali - Katibu
9. Ndg. Haji Jecha Salim - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, aidha nichukue fursa hii kwa kuwapongeza kwa dhati viongozi na watendaji wote wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Unguja na Pemba kwa kazi zao nzuri na ngumu wanazozifanya katika kusimamia haki na wajibu wa wananchi katika kulinda na kusimamia uchumi wa Zanzibar, licha ya changamoto mbali mbali zinazojitokeza na kukabiliana nazo ikizingatiwa kwamba suala la kukabiliana na vitendo vya rushwa ni gumu na linaleta kila aina ya changamoto kwa wahusika wanaopinga vitendo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti baada ya utangulizi huo sasa naomba kukiri kwamba Kamati ya Sheria Utawala Bora na Idara Maalum imeipokea na kuipitia kikamilifu ripoti hii ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi wa Zanzibar na kuweza kuwasilisha maoni yetu mbele ya baraza lako tukufu kwa mujibu wa taarifa zilizomo ndani ya ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika kazi nzuri iliyofanya na taasisi hii ni kudhibiti vitendo vyote vya rushwa na uhujumu uchumi katika nchi yetu. Kamati inashauri *ZAECA* wazidi kutia nguvu na kusimamia vitendo vya rushwa katika zabuni kwani idadi ya kesi hizi ni nyingi na uchunguzi wa kesi zake wa kusuasua ukizingatia kwamba jumla ya kesi 13 zimeripotiwa katika kipindi hichi cha miezi 12 na hadi sasa hakuna kesi yeyote iliyofikishwa mahakamani.

Mhe.Mwenyekiti, vile vile katika jadueli namba moja liliomo katika ripoti hii linaonesha kuwa kuwepo kwa idadi kubwa ya matumizi mabaya ya ofisi ambapo jumla ya taarifa tuhuma 52 zinazohusiana na kesi hizi zimeripotiwa. Hivyo, kamati inaishauri Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais katiba Sheria na Utawala Bora kwa kupitia taasisi zake za Utumishi wa Umma na Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuhakikisha kuwa watumishi wote wa umma wanasimamiwa kufuata miongozo na sheia zilizopo juu ya matumizi sahihi ya ofisi lakini pia na matumizi sahihi ya vifaa vya ofisi vikiwemo vyombo vya usafiri na majengo ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kukuwa kwa maendeleo na sayansi na teknologia nchini kamati yetu inashauri *ZAECA* kufuatilia makosa yanahusiana na uhujumu wa uchumi yanayofanywa kwa njia za mitanado, kwa vile wakati huu miamala mingi ya kifedha inafanyika kwa njia ya mitandao ya simu za mkononi na kumejitokeza wimbi kubwa la wanajamii wanaotapeliwa na kuibiwa kupitia simu zao mkononi. Sasa kwa vile sheria ya *ZAECA* inashughulikia uhujumu wa wa uchumi basi makosa haya wizi wa mitandaoni ni vyema yaakandaliwa utaratibu wa kuingizwa katika orodha ya makosa ya uhujumu ya uchumi.

Aidha, kudhibitiwa kwa changamoto hii kutapelekea hata serikali kupata kodi yake kutoka kwa wafanyabiashara wanaotumia miamala ya fedha katika mitandano na kukwepa kulipa kodi. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa taasisi ya *ZAECA* inamewa jukumu zito la kupambana na vitendo vyote vya rushwa na uhujumu wa uchumi, jukumu ambalo faida yake inaonekana na kila mmoja mioungoni mwetu kamati inazigiazia taasisi zote zenye kufanya kazi kwa mnasaba wa kutafuta haki na kujenga misingi ya utawala bora kwa kulinda uchumi wa nchi, kutoa mashirikiano ya dhati kabisa na yenye kujenga uimara wa tasisi hii ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Vile vile, kamati inataka kuona hukumu za kesi na kupelekwa kwa *DPP* kwa uchunguzi kufika mahakamani na kupata hukumu badala ya kesi hizi kumalizia ofisi ya *DPP* mwaka hadi mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hayo *ZAECA* inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vitendeakazi hususan vyombo vya usafiri katika ofisi za Pemba, jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada zao katika kufanya kazi kwa ufanisi. Aidha, kamati inashauri serikali kulifikiria kwa umakini suala hili la usafiri ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuanzishwa kwa taasisi hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika ripoti hii imelezwa kwamba kuna changamoto juu ya uhaba wa kujengewa uwezo watumishi kuwepo katika tasisi hii ambayo inahitaji kwa kiasi kikubwa kuwa

na wataalamu wa kila fani. Hivyo, kamati inashauri Wizara ya Fedha na Mipango kusaidia taasisi hii katika kuwapatia miradi ambayo itasidia kuwajengea uwezo watumishi wake kulingana na maendeleo ya utandawazi yanavyozidi kuimrika siku hadi siku na hivyo kupelekea kasi kubwa la ongezo la wahujumu uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia kamati pia inashauri *ZAECA* kuangalia marekeboisho kifungu cha sheria yake kinachohusiana na uwezo wa mahakama kusikiliza kesi za aina hii, ambapo kwa sasa kesi hizo hulazimika kufunguliwa katika Mahkama Kuu ya Zanzibar bila ya kuangalia thamani halisi ya kesi, uhalisia unaonesha kuwa kesi nyingi zinazowasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kufunguliwa mahakamani, zina thamani ndogo kiasi ya kwamba huwenda ikawa ndio sababu inayopelekea Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kushindwa kuzipeleka mahakamani. Kwa hivyo, kamati inashauri kuchukuliwa kwa mazingatio hayo ili makosa madogo madogo yaweze kuwasilishwa katika mahakama za chini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kamati inashauri Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu Uchumi kushirikiana kikamilifu na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, katika kuwaibua wahujumu uchumi ambao wanarudisha nyuma juhudi za serikali katika kunyanyua uchumi wa nchi, ambao ndio kikwazo kikubwa katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kuwashukuru kwa dhati kabisa wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii ya maoni ya kamati. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum. Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Sasa mchangiaji wetu wa mwanzo naomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar, atafuatiwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajiandae.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii nichangie kidogo katika ripoti hii ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar *ZAECA.*

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima tukaweza kufika hapa na tukaendelea na ungwe hii iliyobakia ya lalasalama. Nakupongeza sana Mhe. Mwenyekiti, lakini pia naipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuamua kwa makusudi kuanzisha kitengo hiki au mamlaka hii ambayo inafanyakazi ya Mwenyezi Mungu, jambo ambalo hata Mwenyezi Mungu katika Qurani amelikataza la rushwa kwa sababu ni adui wa haki. Lakini na serikali ikaona kwamba jambo hili ilitie katika uongozi wake, ili serikali yetu nayo iwache kufanya kitendo kama hiki iweze kwenda kufanyakazi kwa amani a kila mmoja kupatiwa haki yake. *(Makofi)*

Pia niipongeze mamlaka ambayo kuwa wamepewa majukumu haya kwa kazi kubwa na ngumu ambayo wanaifanya, kazi ambayo inahitaji ujasiri, kazi inayogusa maisha ya mtu na kazi ambayo inagusa mali za watu ni lazima uwe jasiri katika kutekeleza. Inahitaji kwanza wewe mwenywewe

kwanza ukinai katika roho yako usiweze kuhilibiwa kwa kitu chochote, utekelezaji unahita umakini mkubwa na kutenda haki bila ya kuonea, ni lazima wewe mwenyewe uwe umeridhika, hapo ndio utaweza kuifanyakazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana katika kitengo hiki cha mamlaka hii ni lazima waangaliwe ili wawe na uzalendo wao wenyewe kwanza wakubali uzalendo, kwa sababu wanayagusa mambo ya mtu mmoja mmoja, lakini na mali ya nchi. Wakiwa wazalendo ndipo watakapoweza kuifanya kazi hii kwa sababu watakapoona mali ya serikali au mali ya umma inaanza kupotea basi wao ndio wateteaji wa kuona kwamba mali ile haiwezi kuhujumiwa, lakini na wao lazima wawe wazalendo. Lakini ili na wao wawe wazalendo na wao lazima waweze kutunzwa vizuri watu hawa ili na wao waweze kufanyakazi yao, waanze wao kujitosheleza, isiwe mtu anakwenda kuzuwia mali ya mabilioni lakini maslahi yake ni madogo, kwa kweli itakuwa ni rahisi kushawishiwa na kuona kwamba tayari mali ya umma inapotea hivi hivi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ni vyema sana watu hawa na wao watunzwe vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, ili waweze kutekeleza hayo ni lazima pia vile vile waweze kupatiwa vitendea kazi. Mhe. Mwenyekiti, kazi hii ni kubwa sana, ukiona kwamba kila pahali wanahitajika. Niwashukuru kwanza kwa kutangaza mali yao ambayo wameitangaza hapa kitengo hiki ambapo nambari 113 ni sawa sawa na ile ya polisi ukipiga namba 112 unapokewa na Mkoa ulio na polisi. Kwa hivyo, ni jambo zuri sana kuona kwamba nambari hii wameitoa na wananchi waizowee, kwa sababu wakati mwengine kutoka ukasema unakwenda ofisini itakuwa mambo yameharibika. Kwa hivyo, niwapongeze sana kwa kutoa nambari hii ambayo wananchi waizowee ili kuona kwamba inapatikana kwa urahisi sana.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nashauri kwamba wapatiwe na *radio*, hii itasaidia kama vile tulivyozungumza masuala ya kuzuwia magendo. Unapozungumza kitu kile inapopatikana taarifa basi hata yule mkuu wako wakati mwengine anaisikia na atajua kuwa je, hili jambo limefuatiliwa, kuliko hata ile simu kumpigia moja kwa moja wakati mwengine ya mtu yule ambaye umemkusudia na *radio call* naona ni muhimu kwa upande ninavyoona mimi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa upande wa Pemba ndio kabisa hakuna hata usafiri, usafiri ni mmoja Pemba nzima. Tumeshahoji suala hili na kushauri na naendelea kushauri kwamba Pemba waendelee kupatiwa usafiri na usiwe wa gari tu, kwa sababu kuna mwahali mwengine hamuhitaji gari hata vespa zinahitajika, mwahali mwengine ni mwa kupenyapenya wakipata zile taarifa, ama awe amepelekewa au amesikia yeye mwenyewe lazima ajiingize bila ya kujulikana, hivi ni vitu ambavyo vinahitajika sana.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona katika kitabu hiki kwamba miongoni mwa majukumu ni kutoa elimu, niwapongeze sana. Ni kweli kazi yoyote ni lazima itolewe elimu, huwezi kwenda ukamkamata tu mtu moja kwa moja bila ya kumuelimisha akajua haki yake na wajibu wake na nini asifanye. Niwapongeze kwa sababu mimi ni shahidi wameshafika mpaka katika shehia ili kuona kwamba wanatoa taaluma hii ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, lakini waendelee wasiwe tena wamepita ikafika miaka mitano, hii ni elimu inahitajiwa kila siku kuboreshwa mpaka watu wazewee waendee kwa njia moja au nyengine, ile elimu ya ana kwa ana na kutumia mitandano ya kijamii kama vile redio, televisheni na njia nyengine ni vyema sana iendelee huduma hiyo.

Vile vile, miongoni mwa majukumu yake ni kuchunguza kiwango cha uwajibikaji na upotevu wa mali za umma, kuharibu kwa mali za umma, hii ni kazi kubwa sana nayo. Tumeona kwamba kuna taasisi zetu nyengine mali za umma zinapotea hivi hivi, unaweza ukalikuta gari linawekwa pembeni halijakuwa na uharibifu lakini linatengenezewa uharibifu wa makusudi, baadae gari lile linakwenda kwa kiongozi au mtu anayehusika na kitengo kile kwa bei ya chini kabisa, anajitilia bei au anaweza kuzungumza na wahusika wa uondoshaji mali basi ukakuta kitu hiki kinaondolewa, hii inauma sana. Kwa hivyo, naomba sana wawe makini katika kuona kwamba hizi mali za umma haziharibiwi na kwenda kwa mtu mmoja mmoja bila ya sababu za msingi. Hili jambo katika taasisi zetu za serikali linafanyika na wanakazi kubwa ya kulizuwia.

Mhe Mwenyekiti, pia mali za umma zinapohujumiwa ni athari yetu sote inayopatikana. Kwa hivyo, ni lazima zitumiwe vizuri na zidhibitiwe ili faida ipatikane kwa sasa na baadae. Lakini namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho anieleze katika taarifa 187 zilizopokelewa na tuhumu 121 zinaendelea kufanyiwa uchunguzi hadi sasa, lakini tuhuma 20 zimefutwa kwa sababu gani, naomba utueleze kwa nini zikafutwa, ndio ni tuhuma lakini zote zilikuja kama ni tuhuma kwa nini zikafutwa, tuhuma nne zilihamishwa na taasisi husika, zilihamishwa kupelekwa wapi.

Sasa hizi tuhuma 37 uchunguzi wake umekamilika kupelekwa kwa *DPP*, lakini ni kesi tano tu zilizofunguliwa mahakamani kwa nini, nini kimekosekana au wenzetu wameshafanya uchunguzi wamekamilika, *DPP* ni kitu gani kilichosababisha hadi sasa ni kesi tano tu. Kutokana na hali hii ndio hayo watu watarudi nyuma kuona kwamba wanatoa taarifa na jambo liko wazi halafu unakuja kuambiwa ushahidi haupo. Lakini wenzetu wameshakamilisha uchunguzi, *DPP* ni kitu gani kinachosababisha kwamba mpaka leo ni kesi tano tu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anipatie maelezo, ili Baraza lako liweze kupata taarifa na wananchi wanaosikiliza wajuwe hali halisi ya mamlaka yetu inavyofanyakazi. Ahsante nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii, ahsante sana na wewe kwa kuongoza kikao hiki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, atafuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia wasaa huu kuweza kuchangia ripoti hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais anayeshughulikia Sheria, Katiba, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mwalimu Haroun Ali Suleiman, juu ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa kipindi cha Januari hadi Disemba mwaka jana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutimiza majukumu haya au hili kila mwaka nashukuru anatuletea ripoti ya taasisi hii. Mwaka jana nakumbuka alituletea na mwaka huu ametuletea tunampongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, pili naomba kuipongeza taasisi yenyewe kwa kutayarisha ripoti na kutuweka *update* na mambo yao wanayoyafanya tunawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika utangulizi wa ripoti yenyewe Mhe. Waziri ametuambia kwamba mapambano dhidi ya rushwa ni jambo muhimu katika kufikia maendeleo endelevu ya taifa lolote, na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar tumelikubali hili, na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika kusimamia suala zima la utawala bora, amekubali kuundwa Sheria hii ya Udhibiti na Uhujumu Uchumi Namba 1 ya mwaka 2012, na katika kifungu cha 13 imeainisha majukumu makuu matatu yamo hayo majukumu.

Mhe. Mwenyekiti, kubwa sitaki kuchukua muda wako mwingi lakini naomba nijikite kwenye ukurasa wa 6 na 7. Kabla sijasahau niipongeze sana kamati, kwa kweli kamati baadhi ya maoni nayo imeyagusa nawapongeza sana, lakini nitajaribu mimi kuyaleta vyengine hasa nilivyoyakusudia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwenye jadweli namba 6 *ZAECA* wameweza kuweka aina ya tuhuma na idadi ya hizo tuhuma zenyewe na ukitizama hasa hizi tuhuma nyengine ziko wazi, yaani kumkamata mtu ni ushahidi uliowazi kabisa kushawishi, kuomba na kupokea rushwa idadi kiasi 30, rushwa katika zabuni 13, dawa za kulevya 8, kukwepa kulipa kodi 5, kutengeneza nyaraka za uongo. Huyu mtu katengeneza nyaraka za uongo, hilo halitaki tochi liko wazi kabisa, sitaki kutaja nyengine.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kinachonisikitisha ukiangalia ukurasa unaofuata wa 7 uchambuwe. Mimi huwa napenda sana kutafsiri jadweli, maana yake jadweli zina maana yake, uki-*interpret* jadweli unapata picha yote. Jumla ya shutuma zote Mhe. Mwenyekiti ni 187 na zinazoendelea na uchunguzi ziko 121, sijui haikuainishwa kuanzia lini mpaka lini, lakini sasa hivi tokea kuanzishwa taasisi hii ni miaka mitano. Kweli kesi 121 zinaendelea kuchunguzwa tu, uchunguzi huu utakamilika lini.

Mhe. Mwenyekiti, tuna tatizo hapa na ikiwa tunakwenda kwa *speed* hii lile lengo lililowekwa la taasisi hii halitofanikiwa na tutakuwa tunamuangusha sana Mhe. Rais lile lengo lake la utawala bora, uwazi, uwajibikaji, *participatory* ushiriki ule na *openness.* Hili ndio madhumuni makubwa na taasisi hii imeundwa kwa hayo *transparency*, tupige vita rushwa. Sasa Mhe. Mwenyekiti kwa *speed* hii hatwendi, lazima ningemuomba sana Mhe. Waziri ni mwajibikaji mzuri na ni mtendaji mzuri, lazima alisimamie sana hili, kwa *speed* hii hatufiki.

Mhe. Mwenyekiti, sasa twende *column* ya tatu, unasema zilizofungwa kesi 20. Sijui zimefungwa labda unaona hazina maana zimefungwa kesi 20 sawa. Zilizowasilishwa kwa *DPP* kesi 37, kati ya kesi 187 zilizowasilishwa kwa *DPP* ni kesi 37 tu, aa! Lazima tujiulize kuna tatizo gani, wafanyakazi hakuna, wachache au *speed* ya kufanyakazi au kuna vipengele kidogo haviendi, kidogo kuna maswali mengi ya kujiuliza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, sasa inachekesha hiyo *column* inayofuata sasa, zilizofunguliwa mahakamani ni kesi 5 tu ndio zimefunguliwa mahakamani *for 5 years* Mhe. Mwenyekiti, tena zimefunguliwa. Sasa Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri angeongeza *column* nyengine hapa, angeongeza *column* ya mwisho ingetusaidia sana, angesema zilizotolewa hukumu ni ngapi tujuwe ni *conclusive*, hizo kesi zimemalizika zimetolewa hukumu *guilt or not guilt,* katiwa hatia au hakutiwa hatia kesi imalizike. Lakini hata hiyo hukumu haijenda. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunafanya nini, hii inaonesha kuna tatizo ni lazima tuwe wakweli Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri rafiki yangu Mhe. Haroun Ali Suleiman nilikuwa sitaki kumnong'oneza, lakini leo nitamwambia. Tatizo lenyewe tulilolipata tumefanya utafiti, tatizo tulilolipata huo ndio ukweli hatuingilii muhimili mwengine. Lakini tatizo tulilopata ni kwamba kwa mujibu wa sheria hii kesi za uhujumu uchumi zisikilizwe na Majaji wa Mahakama Kuu. Sasa Majaji wa Mahakama Kuu wamesema no, sijui kuna sababu zao za msingi, lakini wamesema hapana wana mtizamo wao mwengine, sasa huo mtizamo wao mwengine mimi siujui lakini sheria haifuatwi kwa sababu hiyo, wanasema wao hapana kesi za uhujumu uchumi ndio maana naona hata moja haijatolewa hukumu, yaani haijakwenda kesi hata moja.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, kama sheria hii tuliyoipitisha hapa kama anaona haifanyikazi basi akarekebishe turekebishe, kama anaona labda Mahakimu wa Mkoa huko au sijui taratibu za kisheria au mahakama za chini, lakini kwa kweli inaelekea kesi Majaji hawazihukumu sijui kwa nini, mimi siingilii huko nasema yale tuliyoyapata tu, tumefanya utafiti kwa nini. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tokea kuanza kama nilivyosema tokea mwaka 2013 kesi 187 mpaka leo hata hukumu kesi moja haijatolewa, lazima ukikaa mwenyewe *simple logic* tu utajiuliza kuna tatizo, tutafute tatizo ni nini.

Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri akae na vyombo vyake tupate *the way forward* mwakani atuletee ripoti basi angalau zimehukumiwa kesi 20, 30 hawa wamekuwa *convited* hawa ameona wako *guilt* au hawako *guilt* basi tutaona kwamba *progress* inaendelea kuliko hivi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hizi kesi nyengine au hizi shtuma nyengine ziko wazi kujifananisha na ofisa wa *ZAECA*, anajifananisha na ofisa wa *ZAECA*. Huyo keshakamatwa halafu anajifananisha na ofisa wa *ZAECA*. Sasa hiyo haitaki tochi, kwa nini lisimalizwe suala kama hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema nichangie hilo kwa nia njema tu ya kutaka mambo yetu yende. Kwa hivyo, naiunga mkono ripoti na namtakia kila la kheri Mhe. Waziri. Ahsante sana na naunga mkono hoja.*(Makofi)*

Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe mchangiaji wetu wa mwisho katika orodha niliyonayo atakuwa Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana. Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuichangia Ripoti hii ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa *ZAECA* ya mwaka huu 2018/2019. Lakini awali nichukue fursa hii nimpongeze sana Waziri katika Ofisi ya Rais Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora, mwalimu wangu Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa kuweza kuwasilisha ripoti hii. Lakini niwapongeze watendaji wote wa mamlaka hii kwa kushirikiana na Mhe. waziri kwa kuendelea kutuletea ripoti hizi mwaka hadi mwaka kwa sababu kuna baadhi ya taasisi ambazo zinapaswa kuleta ripoti na huwa hazileti. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo kwa hili nilichukue fursa hii kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Lakini vile vile nichukue fursa hii kuipongeza kamati, Kamati ya Sheria Utawala Bora, nimpongeze sana muwasilishaji Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis Mwakilishi makini, kwa ripoti yake fupi lakini yenye mantiki kubwa sana. Lakini niwapongeze wenzangu walionitangulia na hususan Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini kwa uwasilishaji wake na niseme kwamba kaninyan'ganya sana suala hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza sana *ZAECA* kwa mafanikio ambayo yametajwa hapa. Taasisi hii ina kazi nzito kwa hivyo tuwapongeze kwa sababu kazi zao zinagusa maslahi ya watu. Lakini ile kuweka nambari sasa ya simu ya bure inaweza kusaidia kurahisisha na kuweka karibu kati ya *ZAECA* na wananchi, ili kuweza kuibua matukio au tuhuma mbali mbali zihusianazo na rushwa na uhujumu wa uchumi, kwahivyo niwapongeze sana. Lakini niwapongeze pia kwa semina mbali mbali na vipindi vya redio na mimi nimsikilizaji mkubwa sana wa vipindi vyao.

Mhe. Mwenyekiti, na niwapongeze vile vile kwa kesi nyingi ambazo za tuhuma ambazo wameziripotia keshi 187 niwapongeze sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi *ZAECA* tumeelezwa kwamba wameokoa mamilioni ya pesa hususan kupitia yale magendo ya karafuu, tuwapongeze sana.

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya jambo ambalo nilitaka nilieleze kwa undani sana lakini Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini ameweza kulifafanua vizuri sana, ni suala la uendeshaji, uchunguzi na umaliziaji wa kesi. Katika ripoti ya aina hii mwaka jana alizungumza hilo na mwaka huu nioneshe wasi wasi wangu wa chombo hichi juu ya tuhuma hizi ambazo zinaripotiwa lakini na uendeshaji, uchunguzi na mwisho umaliziaji wa kesi hizi. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini kanifilisi katika hili. Kwa hivyo yale yote ya Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini namie nayaunga mkono. *(Makofi).*

Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Waziri lazima akae na chombo chake hichi kuweza kuona haiwezekani katika miaka 5 ya uundwaji wa chombo hichi hakuna kesi hata moja ambayo imepatiwa hukumu, hii inatia wasi wasi sana, na hususan ukizitamza, au ukitazama mazingira ya hizi tuhuma, kama alivyotangulia kusema mjumbe mwenzangu.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika suala zima la mahusiano kati ya *ZAECA* na taasisi nyengine. Kwanza niwapongeze sana kwa kuweza umuhimu kwamba *ZAECA* haiwezi kufanyakazi kama *ZAECA* peke yake, *ZAECA* lazima ifanye kazi na taasisi mbali mbali pamoja na jamii, kwa sababu masuala ya rushwa, masuala ya uhujumu uchumi, yamo ndani ya taasisi na pia yamo katika jamii zetu. Kwa hivyo, niwaponge kwa kuweza kuliona hilo.

Lakini katika kitabu chao katika suala zima la mahusiano nimeona taasisi mbili tu ambazo wameziripoti, mahusiano kati yake na Jeshi la Polisi pamoja na waandishi wa habari. Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana *ZAECA* waweze kujipanua zaidi katika kuongeza wigo wa mahusiano kwa sababu majukumu wanayoyafanya bila kuweza kuwa na mahusiano ya karibu na taasisi nyengine basi inawezekana ufanisi ukakosekana.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana kipindi hichi cha bajeti ambacho kinaendelea basi wajaribu kuwa karibu sana na taasisi mbali mbali kwa mfano taasisi kama ya Kikosi cha Kuzuia Magendo

KMKM hawa ni watu wa karibu sana ambao wanapaswa kufanyakazi na *ZAECA*, na wanapaswa vile vile kutowa taaluma katika kikosi hichi kwa sababu wanafanyakazi zinazofanana.

Vile vile, katika ripoti ya wenzetu hawa *ZAECA* haiwezi kuepuka kuwa na mahusiano ya karibu na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za *SMZ*, kwa sababu taasisi hii kazi yake ni kukagua na kuchunguza mahesabu ya serikali, pamoja na mali za serikali. Kwa hivyo ni taasisi moja ambayo inapaswa kuwa na ukaribu mkubwa sana nayo.

Mhe. Mwenyekiti,pia hata ndani ya chombo hichi cha Baraza kuna Kamati ya *PAC* ambayo ni moja kati ya kamati muhimu sana. Kwa kweli, nina imani sana *ZAECA* ikishirikiana *PAC* vile vile na kuipa taaluma basi itasaidia sana kuweza kufanikisha shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, *ZAECA* wameokoa pesa nyingi sana imetajwa na Mhe. Waziri lakini la kujiuliza ni kwamba je, *ZAECA* wametowa elimu kwa wakulima wa zao la karafuu, *ZAECA* wametoa elimu kwa wale wanaokodi mashamba ya karafuu, kwa sababu lengo sio kukamata tuhuma, lakini lengo ni kuweza kwamba zao hili la karafuu wananchi wanaliuza katika vyombo halali. Kwa hiyo kama hawajafanya hivyo nafikiri lengo si kukamata au kuweza kuokoa fedha, lakini lengo ni kuweza tatizo la magendo au tatizo la hujuma katika zao la karafuu linaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana taasisi hii inaulazima wa kufanya semina kwa wakulima wa zao la karafuu lakini hata wale ambao wanakodi mashamba ya karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hii tumeweza kuona changamoto mbili ambazo zimetajwa na wenzetu wa *ZAECA*, moja ni uhaba wa vitendeakazi, na hili nina imani kwamba katika bajeti hii kwa fedha zilizotengwa zinaweza zikawasaidia, lakini jengine ni kujenga uwezo wa watumishi. Sasa mwaka jana katika ripoti ya aina hii kulikuwa kuna tatizo la ufinyu wa nafasi ya kufanyia kazi, lakini vile vile tatizo la kuwa na jengo ambalo linaweza likakidhi haja ya *ZAECA* kufanyakazi zake vyema.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze tu hatua ambazo zinaendelea za kuihakikishia taasisi hii kwamba baada ya kipindi fulani itakuwa na jengo ambalo litakuwa linakidhi haja hasa ya shughuli zake hizi muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ripoti hii ni fupi na mimi nilikuwa sina mengi, isipokuwa niendelee kuiomba *ZAECA* kuweza kusimamia vyema majukumu yake pamoja na kuweza kuwaelimisha watu wake, ili wawe na uwezo ule ambao unaweza kuhakikisha kwamba tuhuma mbali mbali zinafanyiwa kazi na hatima vyombo vinahusikana na sheria vinatoa hukumu ili wananchi waweze kupata imani. Kwa kweli, kama wananchi wale ambao wanapenda maendeleo na kuweza kutoa taarifa za tuhuma hizi hawaoni hukumu kama zinatolewa, sidhani kama itafika wakati waweze kuripotia taarifa hizi.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wananchi watakuwa na imani pale ambapo wanahisi wanaona kwamba kesi zinapelekwa mahakani na hukumu inatolewa vyenginevyo si rahisi sana wananchi wakashajihika kuweza kujuilisha *ZAECA* juu ya tuhuma mbali mbali wakati hawaoni yale matokeo ya matukio ambayo wanayaripotia.

Mhe. Mwenyekiti, baada hayo nikushukuru tena na naunga mkono ripoti hii ya *ZAECA* na nawombea kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe nimemtaja Mhe. Rashid Makame Shamsi mchangiaji wa mwisho lakini nimepata maombi ya Waheshimiwa Wajumbe wawili, ni Mhe. Mohammed Said Mohammed na Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe hawa tumalize nao.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kidogo kuchangia katika ripoti hii fupi sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza tu niseme niwapongeze sana watendaji wa *ZAECA* angalau kwa kukidhi haja ya sharti la kisheria la kuleta kila mwaka ripoti yao hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya sijachangia nilikuwa nina wasi wasi sana na ripoti hii, hii ripoti ni nzuri lakini wasi wangu haikukidhi sheria yote, ipi haikukidhi sheria yote nimkubushe tu Mhe. leo sina nia kabisa ya kuzuia sheria hii isisomwe, lakini kama ningekuwa na nia ya kuzuia sheria isisomwe haikukidhi haja na matakwa ya kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Waziri aelekeze sheria hii aitazame kifungu cha 12. Kifungu cha 12 cha sheria hii inataka iletwe *Auditing and financial Report* lakini humu hamna chochote. Sasa nimuombe Mhe. waziri atakapoleta mwakani atimize haja ya sheria hi ili basi tuweze kuijadili kwa vizuri lakini vile vile tuuoneshe uwajibikaji umetendeka katika serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nichangie katika jaduweli katika ukurasa namba 7 ambapo kuna kesi hapa nyingi kama kesi za kushawishi kuomba nakupokea rushwa umesema kuna kesi 30 zinazoendelea ni 13 zilizofungwa ni 1, zilizowasilishwa kwa *DPP* 13, lakini vile vile kesi ambazo zipo mahakamani ni 3. Sasa Mhe. Mwenyekiti, niseme tu hatukuoneshwa kama kuna kesi zimepungua au vipi, lakini nyengine kuna kesi za kumdanganya muajiri ambao zimefikia 8, na hizo zinaendelea zilishawasilishwa kwa *DPP 5*, sikuweza kufika mahakamani hatujui, lakini vile vile dawa za kulevya kuna hizo 8, lakini hizi hazijapelekwa hata huko kwa *DPP* zinaendelea na uchunguzi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hofu yangu sana kwa *ZAECA* kuendelea na dawa za kulevya uchunguzi wakati mwengine tunaweza kumkamta mtu *red-handed* kwa nini tusipeleke moja moja uchunguzi gani unaweza kufanyika kunawezekana sitaki kusema kitu inawezekana kukawa kuna watendaji waliokuwa sio waaminifu wakaweza kuua kesi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 11 jitihada za wadau katika kupambana na rushwa. Mhe. Mwenyekiti, niungane sana na wenzangu kuwa wapo wadau wengi sana si kuchunguza wanasiasa tu, maana yake *ZAECA* tunaita kuchunguza wana siasa, wanasiasa wenyewe wa CCM wakati ule ambao wa mpapambano wa uchaguzi, lakini hapa wamewataja KMKM, Jeshi la Polisi na wengine Kituo cha Huduma za Sheria, sasa mimi niseme tu hawa ndio

wadau wao na kuweza kuwapa mafunzo lakini kuwapa elimu ya kutosha ili basi waone jinsi tunaweza kupambanana rushwa.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa 12. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amesema matarajio kuendeleza jitihada za kutoa elimu kwa umma kwa kutumia mbinu mbali juu ya athari za rushwa na jinsi ya kushirikiana na mapambano ya vitendo hivyo. Kuwajengea uwezo watumishi wa kupatiwa mafunzo katika fani mbali mbali, kuendelea kuwashirikisha wananchi katika kubaini vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi, kuujenga uwezo wa taasisi mbali mbali kwa ajili ya kufanikisha mpango mkakati, wa kitaifa wa kuzuia rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, hii ripoti sana imeenda kwenye *vision* sana maana nimeiona huu udogo wake halafu hakuna *supporting document* yeyote, Mhe. waziri nikuombe sana utakapokuja utuletee takwimu vizuri na hii ripoti ni ndogo sana na tujuwe jambo hili la kupambana na rushwa ni *very sensitive* sasa tujaribu kuandika kitu ambacho kiko kizuri tuweze kukisoma na iwe faraja kwa wananchi kuona jinsi vitu gani vilivyofanywa.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye changamoto ni uhaba wa vitendeakazi na kujengea uwezo watumishi. Kwa kweli, ni jambo jema sana kuwajengea uwezo watumishi wa eneo lile, lakini imetajwa huku wangapi wamekwenda kozi refu, wangapi kozi fupi, nimwambie Mhe. waziri nijambo jema la kufanya kuwajengea uwezo mara kwa mara ili basi kuwa na wataalamu wazuri na kwa mara chache sana wanapokwenda, au kipindi fupi wanaweza kubaini makosa, lakini jengine uhaba wa vitendea kazi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kupanga ni kuchagua, katika bajeti yao waangalie lile ambalo wataona kwa mwaka huu liko gumu sana kwao ili kulitekeleza. Bajeti zote zinazoletwa bajeti zinalingana basi tuwaombe sana *ZAECA* waangalie kipi kipa umbele watakachokiona lakini vile vile tuwapongeze kwa kuleta ripoti hii lakini tuwapongeze kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya hatuna shaka nao na namuomba Mhe. Waziri sisi ripoti hii tunaiunga mkono kwa asilimia mia, lakini mapungufu ambayo yameonekana mara hii Mhe. waziri atakapokuja mara nyengine yasionekane tena. Mhe. Mwenyekiti nikushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwisho Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sitaki nipoteze muda mkubwa nishukuru Wizara hii ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambayo inaongozwa na kaka yangu mkubwa pamoja na watendaji wake Mwalimu Haroun Ali Suleiman. Vile vile, niipongeze Taasisi hii nzima ya *ZAECA* kwa kazi yao nzuri wanayoifanya niwatakie kheri kwa sababu kazi hii ina mtihani kwa Mungu na majukumu mengi ni majukumu mazito katika taasisi hiyo, lakini ninamuelewa sana Mkurugenzi wa Taasisi hii kwa usikivu wake, busara zake, hekima zake na kazi yake, naona Mhe. Rais wa Zanzibar hakufanya makosa kumchagua kijana huyu ambae kwa kweli ni mwanakindaki ndaki mwenye kuipenda nchi hii.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ni ngumu nzito, lakini niombe Mhe. Mwenyekiti, wiki iliyopita hapa wizara hii kupitia kamati ili tuwasilishia sisi hapa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ripoti ya taasisi ambazo hazikuwa na hati wala hazikuleta hesabu, wizara hii ndani ya katiba na sheria na tunaposema utawala bora, taasisi zikiwemo na *People's Bank of Zanzibar*. Sasa naiomba taasisi hii ya *ZAECA* kufanya kazi yao waende kwenye taasisi ambazo zime *default* na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imo ndani ya katiba.

Kwa hivyo, naiomba basi kwa kuanzia ili sisi Wazanzibari na Wawakilishi kwa sababu imeletwa ndani ya Baraza hili na halikuwa na jawabu. Kutokana na hali hiyo, naiomba taasisi hii sasa ikachunguze ambao wao hawakuleta wame-*default* na tuliwauliza hapa hati wamepata vipi hapakuwa na jibu ndani ya Baraza hili. Vile vile, tunasema kuna utawala bora *good governor*, mimi namshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wamefanya kazi kubwa sana wametuwekea historia. *(Makofi)*

Lakini lazima taasisi hizo, tunaiomba sasa *ZAECA* kwa utawala bora ili Zanzibar ipate jibu, sisi Baraza la Wawakilishi tupate jibu iende ikafanye kazi yake kwa nini hawakuwa na hati, hawajawasilisha ripoti, kamati pamoja na wizara zimezungumza ili tuje tujiridhishe kwa sababu huko kote hizi ni taasisi zipo chini ya serikali. Kwa hivyo, naiomba hilo Mhe. Mwenyekiti changamoto ambayo taasisi hii tuipe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini isitoshe na hapa, hapa juzi tulizungumza sitaki kwenda sana. Vile vile, naiomba taasisi hii sasa ikafanye ukaguzi zile za madawa zilizokuwa zimezungumzwa hapa ya 3.9 bilioni ambazo katika bajeti ya Wizara ya Afya haikuwa imeonesha madeni yale na wanasema wamepokea wakalipa.

Kwa hiyo, naiomba taasisi hii kwa kushirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali waende kwenye bohari watuthibitishie tu kwamba zile dawa zilizokuwa zimelipwa ndizo na zimetumika kwenye taratibu za kupitia tenda au taratibu ambazo zimeitwa kwenye sheria zetu za nchi yetu. Hilo la pili Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naliomba vile vile kwa taasisi hii ili tujiridhishe kwa sababu hili ni Baraza sisi tumekuja hapa kwa niaba ya wananchi, na mimi nimekuja hapa kwa niaba ya Chama Cha Mapinduzi sikuja hapa Raza tu mimi nimekuja hiki kiti si changu cha Chama Cha Mapinduzi. Lakini tumekuja hapa kwa maslahi ya wananchi pesa zetu zionekane wananchi wanazolipa kodi zitumike katika njia ya *sirattilmustaqim* tujiridhishe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, la tatu naiomba vile vile taasisi hii hili suala la dawa za kulevya, naona kama hatukuwa makini hapa Zanzibar tutakuwa na hali mbaya sana. Nilisema kwamba kutokana na mtiririko mzima si kila anaepepesuka mlevi hawa wafanyabiashara baadhi sisemi wote watu wanamiliki nyumba tano tano Mwenyezi Mungu awazidishie lakini je kuna kodi zimelipwa, mtu anatembea na gari la milioni mia mbili je hizi zimepatikana wapi. Tusipige vita siku zote suala la madawa ya kulevya tukawaachia mapapa, kwanza kuna suala la kodi halafu uchunguzi tusije tukaingia katika *money laundry* kuingia katika dawa za kulevya.

Kwa hivyo, narejea tena naiomba taasisi hii Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juzi Iringa kasema na namnukuu kwamba "Iringa tumepata janga kubwa, dawa za kulevya kuanzia watoto miaka 15 mpaka 35". Sasa lazima taasisi hizi tuzipe nguvu tusiwe na

Godfather kwa hivyo mimi naamini taasisi hizi zianze kushirikiana na *ZRB,TRA* kutizama hatutaki kumnyang'anya mtu kwa Mwenyezi Mungu. Mimi nimetoka kwenye umasikini, wazazi wangu wakichunga punda kwa hivyo tutizameni kama mtu ana kodi alipe taratibu zifanywe.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile la nne katika kipindi cha nyuma nataka nitoe tahadhari kama baadhi ya Mawaziri. Mhe. Mwenyekiti, kuna pesa ziliingizwa katika Mfuko wa Wizara ya Habari aliyekuwa Waziri wa Habari wakati ule Mhe. Said Ali Mbarouk hapa tukenda kwenye *hansard* ipo pale, zilitolewa fedha zikaingizwa kwenye mfuko wa serikali baada ya kuingizwa kwenye Mfuko wa Serikali Mwakilishi akahoji, hii ipo kwenye *hansard* anakanusha anasema hajui wala pesa hazikuingia, lakini baada ya tathmini baada ya ule ushahidi kutolewa zilionekana pesa zile zimeingizwa na muhusika mwenyewe akalipwa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninachoomba Baraza hili ni Baraza zito anatoka Waziri halafu asiambiwe chochote mpaka kamaliza muda wake Mhe. Said Ali Mbarouk kathibisha hapa na katibu wake yuko nje, sasa Mhe. Mwenyekiti tusimalize vikao vyetu kama hatujaweza kutizama *hansard* zetu. Kwa hivyo, naomba tukumbushane katika masuala ambayo Wawakilishi wanauliza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache mimi naitakia kila na heri Wizara hii, kwa Mhe. Haroun Ali Suleiman naitakia heri *ZAECA* kwa kazi nzuri nawaombea kwa Mwenyezi Mungu wanachangamoto wasiogope mashetani na kurogwa wao wasimame na Mwenyezi Mungu wafanye kazi yao. Ahsante sana naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Uzini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, nakushukuru Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika wakati huu tukiwa salama salmini. Aidha, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa namna ulivyosimamia majadiliano haya na maoni mbali mbali ambayo Waheshimiwa wametoa. Nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa wote waliochangia hoja muhimu sana, taarifa hii muhimu sana na nikiri kwamba wametusaidia sana kuifanya ripoti yetu kuwa bora zaidi tutakapokuja tena hapa mwakani *inshaallah*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwataje waliochangia ripoti hii. Mwenyekiti kwa niaba yake Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, Mhe. Shehe Hamad Mattar, ndugu yangu rafiki yangu Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini, Mwanafunzi wangu Mhe. Rashid Makame Shamsi, Mwanafunzi wangu mwingine Mhe. Mohammed Said Mohammed, na mdogo wangu Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali, na swahib wangu Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Issa Haji Ussi ambaye kachangia kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii inaonekana ni ndogo kwa maana utaiona ni ndogo lakini kwa tafsiri si ndogo tukiiangalia vizuri tutajikuta kwamba ripoti hii ina mambo mengi sana, lakini

inshaallah tukijaaliwa nawaahidi Waheshimiwa Wajumbe wote kwamba ripoti hii mwakani itakuwa inajieleza vizuri zaidi na takwimu nitazozileta zitatoa tafsiri halisi kabisa ya masuala yenyewe yalivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiri kuna masuala yamezungumzwa kimsingi lakini ukitizama mengi nawashukuru kwamba wote wamepongeza tumepokea pongezi zao na ushauri wao, kwa sababu michango imetolewa leo mingi ni ya ushauri zaidi na sisi tunapokea ushauri wao na tunaahidi kwamba inshallah tutaofaatilia hatua kwa hatua.

Wakati tatizo tunalokuwa nalo wakati mwingine tunaonekana kwa taasisi hii iko *very slow* yaani kesi haziaendi kwa haraka au majibu hayapatikani. Kuna matatizo yanatokezea wakati mwingine ushahidi nao unahitaji busara na hekima siyo kila unachokisikia utachukua hatua hapo hapo tunahitaji kuchukua muda kufatilia kuona ukweli wake. Wakati mwingine basi tu mtu kwa jambo lake au kwa sababu yake anaweza akamtupia dongo mwenzake, ili aadhibiwe apate shida aadhirike, hatuwezi kwenda kwa hivyo, lazima taratibu zifatwe za kisheria na tuangalie njia gani ambazo ni sahihi zaidi ambazo hatuwezi kumtia hatiani mtu ambaye hana kosa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiri inaonekana kwamba labda kwenye taarifa hii kuna mambo kesi nyingi sana lakini bado jawabu halijapatikana, ripoti hii nataka niseme ni kwa ajili ya mwaka 2017 Januari mpaka Disemba, isionekane kwamba ni kesi tano tu hizi ni kwa mwaka huu tu 2017 yaani Januari mpaka Disemba. Vile vile kuna kesi moja ambayo tarehe 5 Januari, 2018 imetolewa uamuzi katika hizo tano, lakini nyingine hazikutolewa uamuzi ama kutokana na kukosekana ushahidi au kutokana na utaratibu uliokuwepo pengine haujakamilika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo siyo kwa sababu taasisi hii haifanyi kazi inafanya kazi vizuri, Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali kachangia suala la mambo ya michezo wakati huo Waziri Mhe. Said Ali Mbarouk kachangia na masuala mengine ya baadhi ya taasisi zimeonekana hazijawasilisha ripoti na kaitaka *ZAECA*. Sasa suala hili lipo katika mamlaka ya *CAG* Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ana taarifa na tunamuomba Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali hizi taarifa alizotutolea hapa basi aziripoti kunakohusika kama ana ushahidi nazo atuletee taarifa kamili na sisi tutachukua hatua. Kama anasema kuna watu wamejenga nyuumba waulizwe kwanza pesa wamezipata wapi kama yeye ana ushahidi wa jambo kama hilo kama kuna pesa zimeibiwa mahali popote basi atuletee hizo taarifa na sisi tutamshukuru sana kuliko kukaa tukaja tukaambizana hapa kwamba kuna taarifa moja, mbili tatu.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunapokea tumetoa nambari 113 wakati wowote dakika yoyote tuletewe taarifa na chombo chetu hiki kitafanya utaratibu japo wana matatizo ya usafiri, lakini nina hakika kwa hili wakipata taarifa watafatilia katika mazingira yoyote, mpaka Mkurugenzi anathubutu kutoa gari yake ili ifanyiwe kazi hiyo vilevile.

Mhe. Mwenyekiti, vitendeakazi bajeti ya mwaka huu tutajitahidi kuimarisha maeneo hayo ili tuweze kupata vitendea kazi vya kutosha, usafiri pemba vile vile tutahakikisha siyo gari siyo piki piki hata baiskeli ikiwezekana na vyombo vya mawasiliano navyo tutajitahidi kuviimarisha, ili wananchi wetu wafaidike. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii inafanyakazi kwa uadilifu mkubwa sana sote tuiunge mkono, tushirikiane jedweli tutakwenda kuziangalia vizuri zaidi na kuona kwa kiasi gani tunaweza kuleta mafanikio mazuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sina haja ya kuzngumza mambo mengi kwa sababu mambo mengi ilikuwa ni ushauri tunapokea ushauri, maoni ya Waheshimiwa na ninaahidi ripoti ya mwakani itakuwa nzuri zaidi zaidi na zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka huu insallah kila la heri naomba kuwasilisha (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa majumuisho yako yenye ufasaha. Waheshimiwa Wajumbe, sasa hoja imetolewa naomba niwahoji wanaokubaliana na ripoti hii ya Mhe. Waziri, wanaokataa. Inavyoonekana waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

HOJA BINAFSI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea sasa naomba nimwite Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana kwa imani yako kwa kunipa nafasi hii ili kuja kueleza hoja ya Wananchi juu ya Chama cha Mpira wa miguu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nimeiomba baada ya Baraza lako tukufu kutoa azimio kuhusu kuchukuliwa hatua stahiki dhidi ya kadhia ya timu ya taifa ya vijana ya Zanzibar kufutwa katika mashindano ya *CECAFA Under Seventeen* na kupewa adhabu kutokana na madai ya kudanganya umri wa wachezaji.

Mhe. Mwenyekiti, hoja hii imefanywa chini ya Kanuni ya 27 fasili ya kwanza fasili ya N na fasili ya 27 fasili ya 3 na vile vile hoja hii katika kifungu cha 49 na kifungu cha 50 ya Kanuni ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi toleo la 2016.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya hoja, kwa kuwa nchi yetu ya Zanzibar kupitia Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar *ZFA* ni Wanachama wa Baraza la Vyama wa Mpira wa Miguu vya Afrika Mashariki na Kati *CECAFA* tukiwa miongoni mwa nchi waanzilishi wa *CECAFA* kuanzia mwaka 1950 na tukiwa ni washiriki wa mashindano ya *CECAFA* katika ngazi mbali mbali na mashindano yanayoandaliwa na Baraza hilo kwa miaka mingi tangu *GOSEGI.*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu pia ni wanachama wa Shirikisho la Vyama vya Mpira wa Miguu la Afrika *CAF* na kushiriki mashindano mbali mbali ya Afrika yanayoandaliwa na *CAF* katika ngazi za vilabu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa katika vyama hivyo vya kimataifa *ZFA* imekubali kufuata masharti ya uanachama kwa kufuata kanuni, miongozo na taratibu mbali mbali za kushikriki mashindano ya mpira wa miguu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda mrefu katika ushiriki wa mashindano ya *CECAFA* Zanzibar imekuwa ikifuata masharti, kanuni, miongozo na taratibu hizo kikamilifu na kwa uadilifu mkubwa sana. Hata wakati wa mashindano ya *CECAFA* yaliyofanyika mwezi wa Novemba mwaka 2017 nchini Kenya na vijana wetu kupata mafanikio ya kuridhisha kwa kupigana kiume na kushika nafasi ya pili nyuma ya wenyeji Kenya. Na kudhihirisha ukanda wote wa Afrika Mashariki na Kati kuwa Zanzibar siyo ya kubezwa katika medani na ushindani wa soka la Afrika. Hii ilikuwa ndiyo timu yetu ya *Zanzibar Heroes*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa mnamo mwezi wa April 2018, Zanzibar ilipata tena fursa ya kushiriki mashindano ya *CECAFA* nchini Burundi ambayo ilihusisha vijana wa chini ya umri wa miaka kumi na saba (17), Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar *ZFA* kilifanya matayarisho ya vijana hao kwa kufuata masharti ya ushiriki kwa mujibu wa kanuni ya 4 ya *CECAFA* inayohusu uteuzi wa vijana halisi wanaotakiwa kushiriki katika mashindano hayo.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa timu ya taifa ya vijana Zanzibar iliteuliwa ilisafiri hadi nchini Burundi kwa ajili ya ushiriki wa mashindano hayo ikiwa ni pamoja na viongozi waandamizi wa *ZFA* na kiongozi wa msafara kutoka serikalini kwa matumaini ya vijana wetu wale kushindana na vijana wenzao wa Afrika Mashariki na Kati. Katika hali ya matumaini kama yale ya timu ya taifa ya wakubwa Wazanzibari wengi walikuwa na matumaini makubwa na timu hiyo kufanya vizuri katika mashindano hayo.

Vile vile, kwa kuwa muda mfupi kabla kuanza kwa mashindano hayo *CECAFA* ilitoa taarifa ya kuifuta Zanzibar katika mashindano hayo kwa madai ya kuwa Zanzibar ilikuwa na wachezaji vijana 12 wakiwa wamezidi umri sahihi waliotakiwa na wachezaji wa mashindano hayo, sambamba na kufutwa huko *CECAFA* ilikwenda mbali zaidi na kuiadhibu Zanzibar kulipa faini ya dola za Kimarekani 15,000 pamoja na kuifungia kutoshiriki mashindano ya *CECAFA* hadi hapo fedha hizo zitakapolipwa.

Kwa kuwa wahusika wengi wa soka Zanzibar ikiwemo serikali ambayo ndiyo yenye dhamana ya timu ya taifa kupokea kwa mshituko taarifa hizo, ambazo mbali na mshituko huo pia zimeleta fadhaa kubwa kwa wapenda soka wote wa Zanzibar na Tanzania kwa vile imeonekana timu yetu imetumia mbinu za udanganyifu katika kutaka kushinda mashindano hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli baada ya tukio hilo hakuna taarifa sahihi ambazo wananchi wa Zanzibar wamepatiwa ambao ndiyo wenye timu yao na walipa kodi zao kwa ajili ya timu hiyo ya taifa. Vile vile, ambao pia wana haki ya kupata na kufahamishwa nini hasa kimejiri huko Burundi mpaka timu yao kurejeshwa nyumbani kwa madai ya udanganyifu wa umri na juu ya hayo yote ikapewa adhabu ya kufungiwa na vile vile kupigwa faini, na kuwa upatikanaji wa

taarifa sahihi na kadhia hiyo kutoka *CECAFA* na *ZFA* na serikali ni muhimu sasa ili wananchi wajue nini kimejiri kwa upande upi wenye taarifa sahihi ili tujue hatua gani zimetakiwa zichukuliwe kwa wahusika wa jambo hilo lisijitokeze tena na kuitia aibu nchi yetu ambayo imeanza tena kurejesha heshima ya michezo nchini na hamasa ya uongozi wa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa umuhimu sana kwa jambo hili kujadili na hapa na serikali kuleta taarifa kutojiri ndani ya Baraza hili ambalo ndiyo chombo cha wananchi wenye timu yao ya taifa na ndiyo ambayo imetuma hapa kusema kadhia hii ya timu yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi Mohammed Said Mohammed Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa kutumia Kanuni ya 27 (1) (n), 27 (3), 49 na 50 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016 naliomba Baraza lako tukufu litowe maazimio yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed Said Mohamed samahani kidogo. Waheshimiwa Wajumbe, Kanuni ya 61(e) haturuhusiwi kuzungumza kwa sauti kwa hivyo nawaomba Waheshimiwa Wajumbe sauti zimezidi hata mtoa hoja imekuwa hasikilikani, kwa hivyo naomba tuwe taratibu sauti zisipande juu. Mhe. Mohammed Said Mohammed endelea.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana lakini pamoja na kuwa nataka kutoa maoni hapa na maazimio nina maazimio matatu, lakini Waheshimiwa Wajumbe wakati wa kuchangia Mhe. Mwenyekiti, nataka uniruhusu kuwa pamoja na michango ya Waheshimiwa wajumbe tuweze kuongeza maazimio ikiwa yapo Waheshimiwa Wajumbe kutokana na michango yao ili tuweze kuingiza na tuweze kuazimia mambo haya kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nianze kutaja moja baada ya moja maazimio haya.

1. Tume huru ya uchunguzi iundwe maalumu kwa ajili ya kuchunguza kadhia hii yote kwa ujumla tume ambayo itahusisha mihimili yote mitatu ikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama.
2. Taarifa ya tume hiyo ipelekwe serikalini na kuletwe Baraza la Wawakilishi kama Taarifa ya Serikali ambayo Waheshimiwa Wajumbe wataijadili na kutoa mapendekezo yao ya hatua zaidi za kuchukuliwa kama zitakavyopendekezwa katika taarifa hiyo.
3. Viongozi wote waliohusika wakati wa kadhia hii, Baraza la Taifa la Michezo lichukue hatua kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Baraza la Michezo kuwazuia mpaka hapo uchunguzi wa sakata lote utakapokamilika na taarifa rasmi kutolewa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusoma taarifa yangu na hoja yangu hiyo kama fasili hizo nilivyozizungumza na Kanuni zetu za 27, 49 pamoja na 50. Sasa naomba Waheshimiwa Wajumbe wako, wajadili ripoti hii na hoja hii waijadili ili tuweze kupata kitu cha pamoja na baadae basi kama patakuwa na maazimio mengine tuweze kuyatoa na tuyafikishe Baraza hili, kwa kuwa tumeshachoka na migogoro ya michezo tuweze kuweka timu yetu ya taifa sawa pamoja na chama chetu cha mpira.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo basi niseme tu naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe, kwa uwasilishaji, lakini hujatoa hoja.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, ningekuwa sikutoa hoja hii hoja yangu yote ingekuwa *fake*. Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima kubwa na taadhima na kwa niaba ya wapenzi wote wa michezo Zanzibar, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakushukuru, umetoa hoja kwa mujibu wa kanuni pale ulisema umewasilisha lakini ulilazimika utamke hilo neno na imeungwa mkono, Waheshimiwa wameunga mkono hoja. Sasa Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea kuhusiana na hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed na nina majina karibu manne mpaka hivi sasa, mchangiaji wetu wa kwanza wa hoja hii ni Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali, atafuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Nassor Ali Salim ajiandae.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, leo Zanzibar tunazungumza kihistoria na nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa hoja yake na kazi nzuri na kwa kweli amekuwa ameweka historia katika *hansard* au katika Baraza la Wawakilishi, Mwenyezi Mungu amzidishie na ampe nguvu na imani ya kuwa na uchungu na nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza hii hoja naiunga mkono na hii hoja leo haitaki kutafuna maneno maneno nataka hii hoja inahusu Wazanzibari wote bila ya itikadi ya chama. Kwa hivyo, naomba tu wahusika sote hapa tumesimama hapa kwa niaba ya Zanzibar kama wanamichezo. Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana leo Zanzibar mimi nimekuwa mdau wa michezo karibu miaka 40 lakini ubinafsi, choyo, majungu, fitna ndani ya taasisi na ndani ya Wizara ndio iliyotufikisha hapa leo michezo na hakuna hata mmoja anayeweza kushindana na mimi katika mambo ya michezo katika nchi hii, wazee wangu walionitangulia sawa katika ujana huu. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nataka tuzungumze hata wizara yenyewe inahusika, haiwezekani timu ya taifa ikaondoka ikafanya inavyotaka ikakodi ikatuletea aibu kwa Wazanzibari na wizara imekaa kimya, mpaka leo inaletwa hoja binafsi humu ndani katika Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, kama tunataka tuwe wakweli kilichokuwa moyoni mdomo utasema.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nasema leo Ligi Kuu ya Zanzibar ndugu zetu timu za mpira za Unguja na Pemba zinakwenda kushindana eti kwa kugombania ubingwa wa kikombe, leo Wazanzibari tupo lakini kwa sababu tu mtu umimi umimi ubinafsi hatuwezi kwenda ubinafsi. Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Wallahi namshukuru na nimshukuru Mhe. Makamu wake wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi, wallahi mngelikosekana hapa hata huo mchezo usingelikuwepo hapa huu ndio ukweli, fitna, majungu, choyo, umimi.

Mhe. Mwenyekiti, leo Ligi Kuu ya Zanzibar hii *ZFA*, lakini mimi nawalaumu Wazanzibari nawalaumu wale wanaopata nafasi ya kuwapigia kura viongozi, mnawapigia kura viongozi sio tafuteni viongozi wenye uchungu na nchi, leo mtu anapiga kura anapata laki nne au tano anaona yeye ndio kashafanikiwa. Kwa hivyo, naomba kufanya kosa sio kosa kurejea kosa ndio kosa *you*

learn through the mistake. Wazanzibari mliokuwa wanamichezo mnayo nafasi ya kupiga kura Zanzibar ina historia ndefu Zanzibar tunapendwa. Sisi wafadhili sisi wafanyabiashara tuna uchungu na nchi tunaona uchungu lakini basi ubinafsi tu kila mtu anataka kula tu, anataka kwenda pale *ZFA* aende *TFF* bwana hili posho laki tano basi wewe ingia kwenye msafara wa Timu ya Taifa Mhe. Mwenyekiti, *this is how we are*.

Kwa hivyo, matatizo yetu tunayo wenyewe leo. Kwa mfano, Ligi Kuu ya Zanzibar ile pale *ZFA* timu za Pemba zinashindwa hata kusafiri kule kule kutoka Chake Chake, Micheweni, Mkoani kuja Gombani pale Pemba nauli zinashindwa. Timu za Zanzibar Unguja hoi hai, halafu unaiambia timu ya Pemba ije kushiriki Kombe la Zanzibar Ligi Kuu bingwa wa Zanzibar eti zawadi kikombe, yule si anaweza kununua kikombe chake akakiweka kwenye *club* yake lazima kuwepo na motisha serikali lazima iingilie kati wizara inayohusika.

Mhe. Mwenyekiti, leo nashangaa wizara inatenga zaidi ya milioni mia mbili kwa timu ya taifa, lakini hawa timu ya taifa wanatoka *grassroot*, wanatoka huko chini sasa unaipaje hawa bila ya kutizama timu zetu za Unguja na Pemba, sasa unachezesha Ligi Kuu ya Zanzibar kwa ajili ya kikombe basi kila *club* itanunua kikombe chake kwa kuweka *club*.

Lazima tutizame mtiririko serikali, wizara lazima itizame lakini leo tunakwenda kuweka historia Mhe. Mwenyekiti, haijapata kuwekwa bajeti ya timu ya taifa timu ya taifa hii iliyoshinda iliyokwenda Nairobi imeshinda kwa nguvu za Mwenyezi Mungu na nguvu zao wachezaji huo ndio ukweli, lakini sisi timu ya taifa tunaiona pale inatafuta mbatata na nini lakini inapofanya vizuri. Mhe. Mwenyekiti, unajua unapokwenda marikiti kila mtu karoa damu mchinja ng'ombe humuoni ndio tabia zetu sisi Wazanzibari jambo lolote zuri tunakwenda kulibaka, hapo tena utamsikia Katibu Mkuu, Waziri, Mhe. Rais anapongeza mlikuwa wapi timu hii ilipoondoka. Lakini Mhe. Rais wetu wa Zanzibar huyu muungwana msikivu tena mwanamichezo lakini tatizo huku chini *grassroot*.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwanza hii hatua naona ni ndogo aliyoitoa Mhe. Mohamed Said Mohamed hii ni nchi, Dkt. Salmin Amour Juma Rais Mstaafu wa Zanzibar alinambia Raza usiwe na urafiki katika nchi hawa watu wamedanganya hii ni kesi ya jinai, sio kesi Mhe. Mohamed Said Mohamed analeta hapa kwa sababu tuwaonee huruma ni kesi ya jinai wamedanganya taasisi zilizohusika zimo ndani ya serikali mtu atapataje *certificate* ambayo amekiuka taratibu za umri au *passport*. Kwa hivyo ni taasisi mimi nina uchungu na michezo.

Marehemu Mzee Idrissa Abdul-wakil na Marehemu Dkt. Omar Ali Juma nilichaguliwa mimi Mwenyekiti wa Saidia Zanzibar Ishinde 1989 na niliichukua timu ya Taifa akina Abdullwakati wale, Zahoro, Formen Ethiopia mimi na kaka yangu Gulam kwa hivyo nina uchungu na mchezo. Leo mashindano ya majimbo yetu yale tumeyafanya Unguja na Pemba basi zawadi ilikuwa gari na mshindi wa pili milioni tano, wa tatu milioni tatu leo ligi kuu ya Zanzibar timu hizi hoi hai viatu havina Unguja na Pemba halafu tumekaa kimya tu, nani atakayekuja atakwambia mtu mimi sishiriki chukua *point* kuna timu zile za Mwenge hoi, Chipukizi, Jamhuri leo hoi timu ambayo inaongoza pale. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, lazima tutafute vile vile kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, zamani hapa kulikuwa na *Black Fighter*, *Small Simba*, Kikwajuni, Ujamaa, Shangani, Malindi na kule Pemba kulikuwa na ushindani lakini ubinafsi wetu na uchoyo wa

ubinafsi ndio uliotufikisha pale leo, halafu lazima tutatufe wanamichezo viongozi wenye uchungu na michezo. Lakini leo mimi kazi yangu mvuvi nauza samaki unanipeleka kwenye michezo ikiwa kona si atasema *goal kick* huu ndio ukweli bwana, mimi nina uchungu kwa sababu hakuna mtu anayeweza familia ya Raza ina historia katika michezo katika Tanzania nzima.

Lakini mafanikio yangu sio yangu mie ni mashirikiano na wanamichezo ni mashirikiano na Wazanzibari na mashirikiano ya serikali, mimi bila ya Serikali bila ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar nisingeli simama hapa kuwepo, lakini nashukuru serikali yangu imenisomesha na kila ninachokifanya sifanyi ihisani nairejesha neema kwa Mwenyezi Mungu serikali iliyonifundisha ikanipa elimu haya yote ni mafanikio yetu. *(Makofi)*

Lakini tufike pahala Mhe. Rais wa Zanzibar yumo ndani peke yake kule lazima tumsaidie tuwe wakweli mimi nashukuru sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi Makamu wa Pili wa Rais ana uchungu, hata kama suala la michezo kokote linamgusa yeye. Kwa hivyo, niseme ripoti hii ni ndogo sana naiunga mkono ni kosa la jinai. Lakini Ligi Kuu ya Zanzibar leo *ZFA* iko wapi. Mhe. Mwenyekiti, nahisi uchungu kwa sababu hii ni *field* yangu ni sawa sawa na kula michezo.

Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Mwenyekiti, nataka na wenzangu wengine wachangie tuiunge mkono lakini bado naona kuna haja ya kuzidisha ukali wa hili. Kwa kweli, hii ni kesi ya jinai vyombo vihusike hata wizara ikachunguzwe ndio ukitaka kumchinja nyani usimtizame usoni, kama hujafa hujaumbika haiwezekani timu ya taifa ikaondoka ikasema ni *ZFA*, lazima taasisi na wizara ibebe mzigo na wao wakahojiwe haiwezekani hili jambo likawa linapita tu tukawa tunakaa hapa tunadanganyana tunalisema. Kwa hivyo, ninachoomba sana tunapokuja kuwa-*windup* jambo lazima tuwe wakweli. Hivyo, naiomba *ZFA* nawaomba Wazanzibari wanamichezo wa Unguja na Pemba tuacheni itikadi ya siasa wakati tunazungumza nchi.

Kwa mfano, Timu ya Taifa ilitoka Nairobi pale kuja Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wote bila ya kujali itikadi za kisiasa ya vyama *Airport* ilikuwa inahema, barabara zilikuwa zinahema, lami zinahema kwa sababu watu wanapenda michezo. Kwa hivyo, naiomba na hiyo wizara ichukue juhudi ya hizi timu zetu za kuzisaidia kuzileta Unguja na Pemba kikombe Mhe. Mwenyekiti, *is nothing* sisi Mashindano yetu ya Majimbo au ya Wawakilishi kwenye majimbo yao hutoa jezi, hutoa mipira hutoa kila kitu hawa wawakilishi wote hawa Unguja na Pemba hukusanya kila kitu na mchango, mchango wa ng'ombe, farasi katika kushindana *this is how the football goes*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwa sababu ni chakula changu lakini lazima tuwe wakweli. Kwa hivyo, nasema hatujachelewa, tunaweza kufika na tutafika lakini tushikamane tuacheni mambo ya ubinafsi tusiwe na jambo ambalo la kuleta kundi haliongozi *ZFA*, wala kundi haliongozi nchi hakuna kama kuna mtu anafikiri kuna kundi linaongoza nchi au *ZFA* huyu kapotea itabidi tumuombee dua abadilike kwa Mungu. Kwa hivyo, naiomba wizara nzima isikae tu, isipokuwa inapaswa kusimamia hata ligi *ZFA* leo mnachagua hoi hai iko wapi, lazima tuwe na *determination* michezo mingi Wazanzibari wanapenda, UMISETA ile pale mchezo wa vijana imepata wadhamini wapo lakini akufukuzae hakwambii toka.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii, lakini hoja hii Mhe. Mohamed Said Mohamed namuona kama kaiweka nyepesi, lakini tuanze kwa hapo na naomba Baraza zima hili liwe fundisho si kwa hili kwa vitu vyote vinavyokuja. Lakini michezo bado tunayo nia tutasaidia mimi kama Raza na wafadhili hatutovunjika moyo na wachache tutaisaidia serikali yetu haki na mali ndio iliyotufikisha hapa. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali kwa mchango wako. sasa naomba nimuite Mhe. Suleiman Makame Ali, atafuatiwa na Mhe. Nassor Ali Salim na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajiandae.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia na mimi kidogo hoja ya Mjumbe Mhe. Mohamed Said Mohamed ambayo hoja hii ina mashiko, kusema kweli wengi ambao tunapenda michezo tunasikitika na lililotokezea kwenye suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, niseme baada ya Mapinduzi kabla ya Mapinduzi vyeti vilikuwa ni tabu vyeti vya kuzaliwa waliopungua umri huo au waliokuwa nini walikuwa wanalijua hilo, lakini yalipokuja Mapinduzi ya Zanzibar katika kitu ambacho kuwa hakina tabu mpaka leo hii kila Wilaya kila Shehiya kila Mkoa ni suala la vyeti vya kuzaliwa. Sasa mimi niulize ilikuwaje au nisikitishwe na hili kwamba hata ifike wale vijana waende kule warudishwe kisa ni sababu ya kwamba hawajulikani umri wao wamezaliwa mwaka gani.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi najua kwamba Mhe. Raza alisema kwamba ni ule umimi kuna mengine yanasikitisha, megine sawa peleka mwanao lakini mengine mpaka hili sijambo la kumchukua mtoto wako ukampeleka hata kama hawezi hata kama umri umepita mengine yanatia hasara, yako mengine mtu anabeba mwanawe anapeleka shemiji yake mkwewe, mjomba wake.

Lakini suala kama hili la nchi leo Mhe. Rais wa Zanzibar nampongeza sana na kila mwenye macho haambiwi tizama anaona jitihada za Mhe. Rais wa Zanzibar anavyozifanya, leo kila wilaya inajengwa viwanja vya kucheza mpira ili vijana wetu na wanamichezo waweze kunufaika leo mambo yanayotokezea ni kama hayo hivyo viwanja vitafanya nini vitaonda majani Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu itakuwa soka la Zanzibar tunaiua inakuwa wale vijana wenyewe na Zanzibar yenyewe tunaipunguza nguvu kwenye masuala ya michezo, itakwenda sasa hivyo viwanja vinavyojengwa kwa gharama kubwa kwa imani ya Mhe. Rais wa Zanzibar vitaota majani vifungiwe mbuzi.

Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Mohamed Said Mohamed alisema hapa kwamba wale waliofanya hivi wachukuliwe hatua na mimi naunga mkono asilimia mia, ikiwezekana hata hii gharama ya kulipa mtu auze kiwanja chake auze shamba yake, auze mgomba wake hii wailipe wao, kwa sababu wao ndio waliosababisha kuitia hasara ili sisi tusemwe vibaya Zanzibar kwenye suala la michezo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, *Zanzibar Heroes* ilipokwenda Mombasa kule kucheza mpira sote tulifurahi maji kombeni yalikuwa yanatuosha, watu walishirikiana kwa umoja na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tulichangia tulitoa mchango wetu ili kuhakikisha kwamba sekta hii ya michezo kwa vijana wetu tuko nao bega kwa bega ambapo kwamba tumeshaona njia wapi pa kuelekea,

kuna watu hawa wamesababisha hii Zanzibar tuonekane kwamba yale mambo ya kukejeliwa kudharauliwa, mimi naomba sana sana rafiki yangu Mhe. Waziri yupo pale, namuomba hili suala kama yeye au wizara inayohusika achukue hatua ambazo kwamba wale waliosababisha hili pamoja na serikali kwa ujumla waweze kuchukuliwa hatua kali ili iwe ni fundisho kwa wengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, leo Zanzibar tunataka tushiriki michezo mbali mbali na Mhe. Suleiman Sarahan Said anasema kila siku hapa kwamba Zanzibar tuna vipaji vya michezo kila aina, lakini kila kukicha tunarudishwa nyuma, kuna watu wanarudisha nyuma hawataki kuona ile jitihada ya Zanzibar, kama Zanzibar inatajitikana kwenye sekta ya michezo.

Mhe. Mwenyekiti, sina mengi ya kusema isipokuwa ni hayo, lakini naunga mkono asilimia mia, lakini pia vile vile kwamba wale waliosababisha hasara hii ikiwezekana basi faini hii ya shilingi dola 15,000 wazilipe wao ili iwe ni fundisho kwa wengi wale watakaokuja kuhakikisha kwamba na sisi Zanzibar tutajikane kwenye masuala ya michezo.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Suleiman Makame Ali kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Nassor Salim Ali, atafuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Machano Othman Said ajiandae.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii binafsi ya Mhe. Mohamed Said Mohame ya kuhusiana na kadhia hii ya timu yetu ya taifa na *ZFA* kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti kwa kweli wachangiaji walioanza kuchangia wameanza na kasi kubwa. Kwa sababu hoja hii tunaiunga mkono na ushahidi umeona kwamba Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu hili wameiunga mkono hoja hii. Sasa na mimi nataka nizungumze machache tu, kwa leo sitaki nizungumze sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa kuleta hoja hii. Kwa kweli, ni wajibu wetu kumuunga mkono Mhe. Mohamed Said Mohamed katika hoja hii kwa lengo jema, kwa dhamira njema na matumaini ya kuijenga *ZFA* mpya kama tunavyosema Tanzania mpya CCM mpya na tunataka na *ZFA* mpya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutekeleza vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kusimamia au kuleta maendeleo na mabadiliko makubwa katika sekta ya michezo, lakini hawa wachache ambao wanaturejesha nyuma nadhani sote ni wajibu wetu sisi kuwalaani na kuhakikisha kwamba tunaziunga mkono juhudi za Mhe. Rais wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Chama cha Mpira wa Miguu *ZFA* ni mwanachama wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika ya Mashariki na ya Kati, takriban zaidi ya miaka 50 tokea miaka ya 1950 mpaka leo mwaka 2018 ni mwanachama wa shirikisho hili la Mpira wa Miguu Afrika Mashariki na

waanzilishi tokea *GOSEGI Cup* Sasa Mheshimiwa tukiwa *ZFA* vile vile ni wanachama washiriki wa Chama cha Mpira wa Miguu Afrika yaani (*TF*), sasa hili ambali limetokea kwa kweli ni aibu kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla na ni jambo ambalo limewavunja moyo sana wapenzi wa mpira wa miguu Zanzibar na Tanzania. Ni jambo ambalo kwa kweli serikali lazima ilichukuliwa hatua na kutoa maelezo ambayo ya kuendeleza soka letu la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wapo wengine wanasema serikali sijui haiwezi kuingia, hapana kwa sababu ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imetoa maelekezo katika kuendeleza michezo pamoja na mpira huu wa miguu ambao tunauzungumza. Sasa hata katika nchi nyengine Mhe. Mwenyekiti, Ghana takriban kama mwezi mmoja uliyopita waliivunja Chama cha Mpira wa Miguu pale nchini Ghana kwa sababu ya kadhia ambayo ilisababisha kuzorota na kuvunja maendeleo ya mpira wa miguu pale nchini Ghana.

Nina imani kwa serikali yetu makini, yenye kiongozi makini, na waziri wake makini, nina imani kwamba waziri wetu huyu, mpiganaji, mpenda maendeleo, msikivu, mweledi pamoja na Naibu Wazi wake na Katibu Mkuu, watatupa majibu ambayo ya kuleta mabadiliko ndani ya *ZFA* kwa ajili ya kuendeleza soka letu la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika maazimio. Maazimio ya Mhe. Mohamed Said Mohamed ni matatu lakini na mimi niseme niongezee kidogo katika maazimio hasa katika azimio la kwanza ambalo nanukuu.

> "Tume huru ya uchunguzi iundwe maalum kwa ajili yakuchunguza kadhia hii yote kwa ujumla. Tume ambayo itahusisha mihimili yote mitatu ikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama"

Sasa mimi naomba kuongeza kidogo, namuomba Mhe. Mohamed Said Mohamed na Mhe. Waziri hili walichukue ili kuongeza. Pamoja na uendeshaji mzima wa *ZFA* ili waichunguze *ZFA* nzima ili tujue hasa tatizo liko wapi, kwa sababu tukichunguza tu haya ya safari ya kwenda na kadhia iliyotokea, lakini tuichunguze *ZFA* nzima ili tujue wapi tunakwenda, wapi tunarekebisha.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na taasisi wenyewe kwa kweli *ZFA* ni chombo ambacho kinatuendelezesha mpira wetu wa Zanzibar na kuna sheria zake na Kanuni zake na Katiba zake. Lakini, Katiba hii iliyopo namuomba sana Mhe. Waziri kupitia mrajisi na Baraza la Michezo la Taifa (BTMZ), ili kusimamia kuleta Katiba mpya ya *ZFA* kwa sababu migogoro yote na matatizo yote ambayo yanawakumba *ZFA* ni kutokana na Katiba waliyonayo hivi sasa, Katiba haifai, haifai kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, hii nchi ni moja, Zanzibar ni moja Unguja na Pemba ni nchi mmoja, haiwezekani leo kuna Katibu wa Kamati Tendaji Unguja na Kamati Tendaji Pemba haiwezekani, Lazima tuwe na Kamati Tendaji moja na tukiwa na Rais basi wawe na Makamo wa Rais, isiwe Makamo wa Rais Unguja, Makamo wa Rais Pemba. Hii nchi ni moja, tunajenga umoja na mshikamano, lazima tujenge umoja kupitia sekta hizi za michezo sasa tukiayaacha huku Mhe. Mwenyekiti yataendelea na kwengine. Sote ni waumini wa umoja na mshikamano na kulinda Muungano wetu na umoja wetu, kwa hivyo umoja wetu huu tuulindeni hata katika michezo.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ili kuhakikisha kwamba hiyo Kamati kunaangaliwa mikakati ya kuhakikisha kuichunguza *ZFA* yote na Katiba yake ili kuunda timu ambayo itasimamia. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri basi kwa kuanzia haya aunde Kamati angalau ya kipindi cha miesi sita anao uwezo huo kwa kupitia Mrajis, ili kusimamia yote hayo na kuchunguza na kupanga ili kufanya mikakati mzuri ya kuunda na kupata *ZFA* ambayo imara yenye kuleta maendeleo na vijana wetu kuendeleza sekta hii ya mpira wa mifuu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba Zanzibar tuna vipaji vingi pamoja na Tanzania kwa ujumla. Ukanda huu wa Afrika Mashariki katika nchi ambazo ina vipaji vya wachezaji wa mpira wa mifuu ni Zanzibar. Kwa upende wa Tanzania Bara, Dar-es-Salaam, Tanga kuna vipaji vingi. Juzi tu kuna mchezaji mmoja anachezea timu ya Denmark asili yake ni Tanzania. Kwa hivyo inaonesha wazi kwamba Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kuna vijana ambao wanavipaji vikubwa wanaweza kuleta sifa kubwa na faida kubwa sana kwa taifa letu. Sasa hayo yote yanatakiwa yawe na usimamizi mzuri ambao unalenga katika kuinua Sekta yetu ya Michezo. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono tena hoja kwa asilimia mia moja hoja hii. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Nassor Salim Ali kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi atafuatiwa na Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Ali Suleiman Ali ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ndogo ya kuweza kuichangia hoja hii ya Mhe. Mohamed Said Mohamed Mwakilishi makini wa Jimbo la Mpendae, lakini ni Mwakilishi ambaye anaongoza katika kutoa hoja katika Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya kufutwa kwa timu yetu katika Mashindano haya ya *CECAFA*, Waheshimiwa Wajumbe wamechangia mengi na wamechangia kwa hisia tofauti. Mimi niseme tu kwamba ni mtu ambaye ninafahamu sana masuala ya michezo, taaluma ya uongozi wa michezo, usuluhishi wa migogoro ya michezo ni vitu ambavyo kwangu mimi ni taaluma.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiria tusikurupuke, Mhe. Mohamed Said Mohamed ameleta hoja lakini inataka busara kubwa sana na mimi naunga mkono hoja yake, lakini kwa mazingatia makubwa. Unapotaka kusuluhisha jambo na kulipatia ufumbuzi unatakiwa uwe na hadidu rejea mbali mbali. Wenzetu wamekwisha kuzungumza kwamba Zanzibar ni mwanachama wa shirikisho hili tokea miaka ya 50 na haijawahi kutokea kadhia ya namna hii. Sasa kunatakiwa umakini kidogo au mkubwa katika kuweza kuliona jambo hili chanzo chake, sababu zake na vipi tunaweza tukaleta suluhisho lake. Tusikazie tu kuweza kuwashutumu wenzetu au kukishutumu chama kwa sababu sosi ya hili jambo hatujalijua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimpongeze sana Mhe. Mohamed Said Mohamed Kamati Huru inahitajika na Kamati Huru hiyo ndiyo ambayo itaweza kuona chanzo, sababu mpaka tukafikia hapa. Kwa kweli, nakiri kwamba hili limeitia doa sana Zanzibar, hili limeiletea aibu sana Zanzibar, kwa sababu miaka ni

mingi halijawahi kutokea. Lakini kuanza kuwashutumu wenzetu nafikiri ni mapema mno kama hakuna tume huru iliyoundwa na kuweza kujua hasa kiini cha tatizo hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nina usoefu mkubwa sana masuala ya michezo, nina elewa sana. Shirikisho au Chama chotote cha mchezo ulimwenguni kinakuwa na sheria zake, kinakuwa na kanuni zake, kinakuwa na miongozo yake. Mimi nina imani kwamba Shirikisho hili ni pevu lina viongozi mahiri wenye uzoefu, nina imani sheria ipo, nina imani Kanuni zipo, nina imani taratibu na miongozo ipo. Sasa tujiulize kwa nini likatokea hili.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya mashindano yoyote ambayo yapo kirasmi lazima kunakuwa na vikao mbali mbali vya maandalizi, vikao ambavyo vinakuwa vinapitia sheria, kanuni zake pamoja na taratibu zake. Ndio maana tukasema kuna *under seventeen*, lazima itolewe *definition* na hii inatolewa katika vikao vya awali vya kabla ya mashindano hayo. Sasa leo inashangaza sana timu mpaka inafika kwenye mashindano, inafika kiwanjani, halafu linatoka tamko kwamba Zanzibar imefutiwa kuingia katika mashindano. Lazima tujiulize inawezekana vile vile kuna kidudu mtu ndani hapa hatujui. *(Makofi)*

Kwa nini kama serikali tuingie harama tokea maandalizi ya mashindano kuwatafuta wachezaji, paspoti, kuwasafirisha mpaka wanaingia kwenye uwanja ndio kauli hii inatoka. Lazima tujiulize, sio kitu cha kawaida kabisa, kwa sababu kama ni kosa maana yake usisubiri mpaka timu imeingia uwanjani.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni aibu kubwa kwa sababu imetuletea hasara sana, imetuletea hasara za maandalizi, imetuletea hasara za vijana wetu na viongozi wetu kuweza kutumia muda wao katika kuziandaa timu. Vile vile, imetuletea hasara katika fedha za maandalizi, imetuletea hasara kama hii faini ambayo tumepigwa na tukapaleka maana yake ni hasara ya fedha. Lakini, kwa upande mwengine tunawananchi wazalendo ambao wameiyunga mkono timu hii aidha kwa kuipa vifaa au fedha taslim lakini wameichangia, hii nayo ni hasara kwa upande mwengine. Lakini hasara nyengine ya kuonesha kwamba Zanzibar haiaminiki, sasa hasara hizi tutazifuta vipi.

Hasara hizi tutazifuta baada ya kuundwa Tume Huru ya kuweza kuchunguza kiini cha tatizo. Mimi sitaki niilaumu *ZFA*, sitaki nilaumu Kanuni au Katiba ya *ZFA* ni mapema mno kulaumu, utakapofanya uchunguzi ndio baadae unaweza ukajua kama Chama chetu cha Mpira kina matatizo au viongozi wetu wana matatizo au *CECAFA* yenyewe inamatatizo katika maandalizi na hatimae katika mawasiliano na vile vyama au wale nchi wanachama.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohamed Said Mohamed ambaye ndiye aliyewasilisha hoja hii aliomba kama kunamaazimia mengine aongezewe. Nichukue fursa hii kuweza na mimi kutaja maazimia mawili. Kwa kuwa kadhia hii ni ya mwanzo kwa nchi yetu. lakini imeitia aibu nchi yetu, Tume Huru iundwe, ichunguze ili kujua chanzo na sababu ya kadhia hii ili tatizo la aina hii lisiendelee kutokea katika nchi yetu. Hilo ni azimio langu la kwanza la kumuongezea Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Azimio langu la pili baada ya uchunguzi kukamilika na ripoti kuwashilishwa basi chama kinachohusika lakini na wizara inayohusika ikae na wadau wa michezo kuweza kuwaelezea kwa uwazi kadhia hii na kuweza vile vile kuomba radhi kwa wale wote ambao walikuwa na

matumaini na nchi hii pamoja na wale ambao wameichangia timu hii kwa njia moja au nyengine, iwe kwa mawazo, fikra, fedha au vifaa ili kuwapa moyo kwa mwakani au mwaka mwengine tunapoandaa timu zetu wawe na moyo wa kuweza kuzisaidia timu zetu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia hoja hii, lakini naomba tuwe na busara katika kuchangia ili kuweza kufahamu hasa mzizi wa tatizo hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Rashid Makame Shamsi. Sasa naomba nimwite Mhe. Machano Othman Said, akifuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia nafasi hii ya kuchangia hoja hii ya Mhe. Mohamed Said Mohamed Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae. Pia nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia na mimi nitachangia kwa ufupi kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kadhia hii ilikuwa ni mbaya sana na imeleta doa sana katika maendeleo ya mpira kwa Zanzibar. Lakini kama walivyosema baadhi ya wenzangu kwamba kadhia hii mimi nahisi imerejesha pia ile ari na moyo ya vijana wetu katika kujiendeleza kimpira.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba yanakuwepo mabadiliko ya kimpira Zanzibar, na wengine humu wamefikia wafadhili wa michezo walikuwa nani wengine wataalamu wa kucheza mchezo lakini na mimi nilikuwa Mwenyekiti wa *ZFA* Wilaya ya Mjini, kuchaguliwa Mwakilishi wakanishawishi wenzangu niendelee nikawaambia hapana wacha nitumikie uwakilishi kwenye mpira waendelee watu wengine tusichanganye mambo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi mpira ni ajira kubwa sana na tuna bahati Zanzibar kwa vijana wetu wa *Under Seventeen* na mpaka *twenty* hata wale wa Zanzibar *heroes* kupata ajira yao kutokana na mpira, na kama tukijipanga vizuri yawezekana kila mwaka tukawauza wachezaji Bara kama kuanzia 20 mpaka 30 na wachezaji wa Zanzibar wanachukuliwa kwa shilingi milioni 20,000,000 au 30,000,000 mpaka shilingi milioni 40,000,000. Kwa hivyo, ni vijana ambao wanaweza kuingia katika soko kwa sababu bara kuna timu nyingi kubwa na zina uwezo kuna kama timu saba za ligi kuu Bara zinaweza zikanunua hata wachezaji wanne wanne wa Zanzibar na wakacheza na wakapa ajira na wakapata fedha nyingi.

Lakini, yanapotokezea mambo kama haya ambayo yametokezea yanavunja moyo hata kuchukuliwa katika timu kubwa naungana na mapendekezo ya Mhe. Mohamed Said Mohamed, lakini mambo mengine yako wazi sana kwa sababu kesi ya mwanzo ya ugomvi je *ZFA* waliarifiwa hawakuarifiwa mwanzo wao wakakataa wakasema hawakuarifiwa lakini baadae wakakiri kwamba waliletewa *email* lakini hawakuisoma sasa huo si ndio uzembe wenyewe utaletewa *email* masharti ya kushiriki mashindano ya vijana hukuisoma mpaka muda unapita timu unapeleka wachezaji wanarejeshwa Zanzibar inaadhibiwa hili ni kosa.

Lakini kama kwa sababu *ZFA* tunafanya kazi kwa mazoea, *ZFA* Chama cha Mpira, yaani kipo kama *club* maalum kwa watu maalum na mambo yao maalum, kama watu wakawaida tu hawaweze kuingia kwenye *ZFA* na ndio tumefikia hapa tulipofikishwa leo. Kwanza mimi nina

ushauri ambao utakuja baadae pendekezo hatuwezi kwenda tupate mafanikio kwa kutumia Katiba ya sasa ya *ZFA* hatuwezi kabisa, kwa sababu katiba yenye ikifanywa marekebisho inafanyiwa marekebisho na viongozi ambao wako madarakani. Kwa hivyo, wanafanya marekebisho kwa kuangalia maslahi yao yatakuwa yepi hatuwezi kwenda mbele.

Lakini tulitaka kuwatupia mpira *CECAF* sasa hapa hawanakosa wameziarifu timu zote 8 masharti ya kushiriki mashindano wenzetu wameyaweza, kuna mjumbe alisema kwamba labda kuna makosa hapa tunafanya makosa wachezaji tunawarejesha umri, wachezaji *passport* tunawafanyia sizo, wachezaji hapa vyeti vya kuzaliwa wanadanganya, ili waende katika *under seventeen*. Kwa hivyo, tujisahihishe.

Kwa mfano, wenzetu Ghana juzi Rais wa Chama cha Mpira Ghana ambae pia ni kiongozi wa *FIFA* kafukuzwa kaonekana kachukua dola kama $25,000/- za rushwa kaondolewa na utaratibu sio kuivunja *ZFA* mimi sipendekezi kuvunjwa *ZFA* utaratibu na haiwezekani Rais kajiuzulu, Makamu wote wawili wamejiuzulu, kamati tendaji inakaa kwa misingi gani. Sasa kama wale manahodha watatu wameshaondoka kamati tendaji nao yote iondoke ipishe iundwe kamati katika *Committee* ya muda iandae marekebisho ya katiba na mimi sipendelee sasa hivi tufanye uchaguzi mpaka tumalize marekebisho ya katiba ya *ZFA* halafu ndio tuchague viongozi sio sasa tukajaze nafasi ya mwenyekiti na makamo zake wawili tutakuwa hatujafanya la maana.

Lazima Mrajis wetu wa Michezo atumie nafasi ambayo anayo kufanya marekebisho ya Katiba ya *ZFA* hatuhitaji kuwa na *ZFA* mbili sasa hivi kama zilivyo sasa, sasa tuna *ZFA* Pemba, tuna *ZFA* Zanzibar hiyo haiwezekani, Kamati tendaji Pemba inakutana inafanya maamuzi ya mpira kamati tendaji ya Unguja inafanya maamuzi ya mpira sijui utaratibu gani wa vyama hivi hatuhitaji kuwa na makamo wawili tunahitaji kuwa na makamo mmoja wa Rais. Hatuhitaji kuwa na ligi ambayo inatimu 38 duniani hakuna Zanzibar ipo hii ligi gani.

Sasa Mhe. Mohammedraaza Hassanaali Mohamedali pale anaposema timu hazina ufadhili kweli, hakuna duniani nchi ambayo inatimu 38 kwenye ligi hata hizo *Premium* Ligi za Uingereza, Spain, German mwisho timu 20 sisi 38 huu mpira au tunafanya nini, lazima tuondoke katika mazoea kwamba tunacheza mpira tu, tucheze mpira kwa idadi maalum na haliwezekani hili kama Katiba haikurekebishwa vizuri. Katiba ya sasa inawaruhusu kuwafanya wanalolitaka wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo nashukuru wala silaumu wizara naona wizara wanajitahidi sana na wametumia labda maarifa kutoka kwa wale viongozi kujiuzulu nawashauri wizara wakae na hao wajumbe waliobakia wa Kamati Tendaji za *ZFA* kwa kutumia njia zao nao wawaagize nao wajiuzulu iundwe kamati ya mpito ya kuendeleza mpira Zanzibar.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mohamed Said Mohamed mtoa mada katika maazimio ambayo tuyapendekeze niongeze kwamba na *ZFA* sasa wizara iwatake wajumbe wa kamati ya utekelezaji walobakia wajiuzulu, ili kupisha halafu wizara iunde kamati ya muda ya uendeshaji wa mpira Zanzibar kwa kipindi kisichozidi miezi sita hilo la kwanza. Pili Katiba ya *ZFA* nayo ifanyiwe mapitio na kurekebishwa kwa kupitia wataalamu ambao watateuliwa na serikali, ili kuhakikisha kwamba na wadau wa mpira washirikishwe ili *ZFA* tuwe na *ZFA* mpya. Hayo ndio ambayo mapendekezo yangu katika Katiba.

Hili la faini la dola $15,000 sijui tumepewa muda gani maana yake nalo lisije likapita muda halafu ikawa badala ya 15 tukafungiwa kushiriki mashindano ikawa adhabu kubwa zaidi, nafikiri hili serikali waliangalie watalimaliza vipi katika kuweka sawa katika ukanda wetu huu wa Afrika Mashariki. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja hii (*makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: ahsante nakushuru Mhe. Machano Othman Said kwa mchango wako, Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa kanuni zetu muda tulionao utakuwa hauturuhusu kuwaita wachangiaji wengine na katika orodha ya wachangiaji nina wachangiaji karibu 4 waliobaki lakini pia tupate tumpe fursa ya Mheshimiwa mtoa hoja sasa niombe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais atumie Kanuni ya Kutengua muda, ili tuendelee na shughuli zetu, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushuru kwa kunipa fursa hii kwa kuwa shughuli iliyo mbele yetu haitohitaji muda mrefu sana na kwa kuwa tokea asubuhi Waheshimiwa Wajumbe wamekuwa wanashughuli mbali mbali. Kwa hivyo, tuweke kando Kanuni ya 23 (1), ya muda ili tupate nafasi zaidi ya kumalizia shughuli ilo mbele yetu na tuweze kupumzika jioni hii. Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo, wanaokataa, inavyoonekena Waheshimiwa Wajumbe waliokubali wameshinda tunaendelea. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali atafutiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Panya Ali Abdalla ajiandae.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kupata fursa hii kuchangia hoja hii ya Mhe. Mohamed Said Mohammed kwa umuhimu wake tulokuwa nao katika nchi yetu.

Lakini pili Mhe. Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati kabisa kwa kutuletea hoja hii ambayo ni maendeleo katika nchi yetu kuhusu vijana wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, leo tumesimama hapa lakini muda wananchi Watanzani na ulimwengu kwa jumla masikio yote yanaelekezwa Urusi kuangalia vipaji vya wanasoka mbali mbali ambao vijana hao wameanzia katika *under seventeen* mpaka kufikia walikofikia.

Kwa hivyo, niseme tu kwamba hoja hii ni muhimu hasa tukizingatia umuhimu wa vijana wetu kama wengine walivyodiriki kusema kwamba michezo ni ajira na hasa mchezo wa mpira wa miguu hakuna alokuwa halielewi hilo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba tatizo la timu ya taifa la vijana wetu chini ya umri wa miaka kumi na saba (17), kama nilivyosema kwamba limetuletea aibu na fedheha na jambo ambalo limetusikitisha wengi. Lakini pia nchi yoyote duniani huwa inakwenda katika vita katika mashindano kama haya tunashuhudia wenzetu nje huko katika mashindano ya ulimwengu, timu inasimama na timu ambayo ina matarajio wao hawana kama wataingia yaani washatoka lakini wanasema pamoja na huyo anaekwenda anataka kuingia katika maeneo hayo ana mdhibiti haingii tumeshuhudia katika *final* hii inoendela Urusi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti makosa yamefanyika mengi kwanza la kudanganya lakini pia la kusikitisha kwamba chombo kinachohusika kipo na kimekwenda katika taratibu ambazo kinasema kwamba kimefikia, lakini hakikufikia kunakotakiwa ndio mana tukakosa wanamichezo wetu hawa kushiriki katika mashindano hayo.

Mhe. Mwenyekiti, baya zaidi kitendo hichi kimeturejesha nyuma kwa sababu vijana wetu katika mashindano kama haya walikuwa waonekane vipaji vinapatikana pale pale wenye uwezo wao katika vilabu vyao wanasema tu kwamba kijana huyu atanifaa mimi kuingia katika timu yangu baadae, lakini baada ya kwende mbele tumerudi nyuma. Lakini bahati mbaya zaidi inaonesha dhahiri Mhe. Mwenyekiti ubinafsi ulitawala katika uteuzi wa wachezaji. (*Makofi*)

Kwa mfano, kama mimi Shihata, mimi nafasi yoyote katika *ZFA* nikaseme aa! Mimi mwanangu lazima aende ndio haya yaliotufika, lakini hili suala limetusikitisha sana. Kwa hivyo, naomba tu kwamba hatua kama zilivyoelekezwa za kisheria zichukuliwe na wale walengwa ambao wameleta matatizo haya basi mimi ushauri nitautoa baadae katika kuengeza katika changamoto hizi.

Mhe. Mwenyekiti, timu yetu hii ni chimbuko na timu kubwa zinazokuja baadae kwa sababu mchezaji akishafikia kucheza timu ya taifa ya vijana anategemewa na vilabu vikubwa ambavyo vinakwenda kushiriki katika ligi kuu ya nchi, lakini leo bahati mbaya tumekosa kabisa. Kwa hivyo, naomba sana hili suala likaangaliwa na kusema tu kwamba kubwa zaidi liangaliwe juu ya kuhakikisha kwamba tunaweka sheria, tunaweka taratibu zetu kupata maamuzi mazuri juu ya hatima ya vijana wetu hawa.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya tunazungumza haya masuala tupo hapa, Mhe. Waziri nasikitika katoka nje hayupo na vijana wale, japo Naibu Waziri yupo lakini Mhe. Waziri mwenyewe angebakia hapa akasikiliza kauli hizi zinazotolewa. (*Makofi*)

Sisi tumesimama hapa kuishauri serikali na serikali ni Mawaziri na sisi pamoja, lakini Mawaziri ndio tunaotegemea kwa hali na mali kwa sababu vyombo hivi viko katika nafasi zao lakini bahati mbaya katoka labda kakutwa na dharura nyengine sina la kusema.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote waliyozungumza wenzangu naunga nao mkono, lakini naushauri wangu kwa bahati nzuri au mbaya tunasikia mtu kafanya tatizo katika eneo fulani, basi

mtu yule hutakiwa akae pembeni ili upite uchunguzi tuendelee na mengine. Kwa hivyo, ushauri wangu wa kuongeza kwa Mhe. Mohamed Said Mohamed pamoja na maazimio aliyotoa nasema tu viongozi wa *ZFA* wote wajiuzulu, kuanzia Rais Kajiuzulu, Makamo wa Rais Pemba kajiuzulu, lakini hawa waliobakia wajiuzulu ili iundwe tume ya muda mfupi ifanye uchunguzi na kujua nani aliyehusika na matatizo haya baada ya kupatikana matatizo yao haya sheria ifate mkondo wake. (*Makofi*)

Lakini pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa lazima tubadilike hakuna Pemba katoka Pemba ligi inaachwa Unguja hapana tuwe kitu kimoja ligi iende kwa maeneo yote mawili na hii itatupa maelekezo mazuri. Kwa hivyo, naishauri serikali *ZFA* ifanyiwe mapitio tena na katika Katiba itayokuja tuwe na kitu ambacho kitatusaidia huko mbele tunakokwenda ombi langu ikiwa Rais wa *ZFA* katoka Pemba, Makamu wa *ZFA* atoke Unguja, ikiwa Rais katoka Unguja, Makamu wa Rais atoke Pemba hakuna *ZFA* Pemba wala Unguja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hii ndio inoturudisha nyuma soko letu baada ya kwenda mbele linarudi nyuma. Naomba sana hili tulizingatie katika maazimio hayo au katika utaratibu wa baadae uwe hivyo.

Lakini la mwisho Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote yalotokea tuamini kwamba *ZFA* ni chombo ambacho kimewekwa na *ZFA* ni chombo ambao kimechaguliwa tulikuwa tunaingojea taarifa hiyo iletwe, lakini hadi leo haijafika. Kutokana na hali hiyo, wizara itupe taarifa angalau tujue nini kimefikiwa hadi hapa tunasimama hapa ili tujue na sisi muelekeo wetu. Lakini kwa asilimia mia moja naunga mkono hoja hii na namuunga mkono sana Mhe. Mohamed Said Miohamed atafute hili na jengine kwa maslahi ya nchi yetu. Nashukuru ashsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Ali Suleiman Ali kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma atafutiwa na Mhe. Panya Ali Abdalla na pia Mhe. Ali Salum na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii lakini sijui kanuni zetu zinatuongoza vipi katika suala zima la kuongeza muda kwa sababu naona orodha bado inakuja na tunahitaji kuchangia hii hoja.

Sasa naomba Mhe. Mwenyekiti, pia uangalie kanuni zetu muda gani ambao tunaruhusiwa kuongeza baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naendelea kukushukuru tena kunipa hii nafasi lakini mimi katika hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed kwanza namuunga mkono hoja yake kwa asilimia zote. *(Makofi)*

Lakini, kitu ambacho ninachotaka kukisema kwamba Zanzibar sisi sasa hivi hapa kwa hii *style* tunokwenda nayo hapa kutakuwa hakuna mpira, hapa kutakuwa kuna watu tu wanacheza mpira lakini kutakuwa hakuna mpira.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Katiba ya *ZFA* tumelizungumza kwa muda mrefu sana Katiba ya *ZFA* tuliyokuwa nayo tukiendelea kuwa nayo hapa tutakuwa hatuna mpira. Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo *style* tunayokwenda tunakuwa kama jongoo anakwenda mpaka agonge ukuta akeshagonga

anajua kumbe huku hakuna njia anageuka anakwenda upande mwengine sasa hapa tumeshagonga tumeshagonga ukuta tunafuta njia nyengine ya kutokea.

Mhe. Mwenyekiti, leo asubuhi tulisoma hapa ripoti ya *ZAECA*, na Wajumbe wakasema hapa mbona hatusikii kesi zinokwenda mahakamani, zinohukumiwa zikatolewa maamuzi, lakini ukija ukiangalia kuna mambo ndani ya hii *ZFA* yenyewe yametokezea watu wamekiuka mpaka hiyo Katiba yao ya *ZFA*, leo kuna *clip* zimevuja kila pahala watu wanasikiwa Rais wa *ZFA* anasema, anasema hapa kama haujavunjika Muungano hakuna mpira bado yupo mpaka leo wewe utegemee kuna mpira hapo. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hawa ndio viongozi tuliokuwa nao wewe utegemee nini. Sasa Mhe. Mwenyekiti, Urais watu wanautaka sana na wengine labda walipoona katika *channel* nyengine hawaupati wakaamua kukimbilia *ZFA* ili na wao waitwe maraisi, lakini huo wa *ZFA* pia watu ushawashinda. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, huwezi ukawa na *ZFA* Unguja, *ZFA* Pemba hiyo ndio Katiba sasa kama haujaondoa katiba hii ukatengeneza katiba ambayo itaimarisha mpira Zanzibar Mhe. Mwenyekiti tutakuwa tunapiga blabla sasa hivi Zanzibar kwa bahati mbaya tunauwa vipaji vya vijana wetu. Kwa kweli, Zanzibar Mwenyezi Mungu katujaalia tuna vipaji vizuri sana vya mpira, lakini kama huna uongozi hata uwe na vitu vizuri vipi kama uongozi wako sio bora, sio imara, sio weledi hamuwezi mkafika pahala.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika hayo mapendekezo na mimi naongeza la nne kwamba *ZFA* hao waliokwishajiuzulu ndio wameshajiuzulu na hiyo Kamati Tendaji iliyobakia na wao wajiuzulu, lakini vile vile iundwe kamati ya mpito kuipitia katiba na kuifanyia marekebisho ili hao viongozi wa *ZFA* watakaochaguliwa wachaguliwe kwa katiba mpya ambayo itakuwa ni katiba *strong* sio katiba tuliyokuwa nayo sasa hivi. Mhe. Mwenyekiti, Waswahili wanasema nyumba choo kama nyumba haina choo si nyumba ndio sawa sawa na *ZFA*, sasa tunaposema choo tunakusudia katiba, ule msingi wa chama.

Kwa mfano, mwenzangu kasema hapa leo Zanzibar tuna timu thelathini na sita sijui thelathini na nane ligi hiyo wakati huko duniani ligi zote unazozisikia timu utakuta kumi na sita mpaka timu ishirini leo Pemba kuna watu kwa mujibu wa takwimu ya mwaka nafikiri kama sikosei ya mwaka 2007 kuna watu wanakaribia laki tano kuna timu kumi na nane ligi.

Unguja kuna watu karibia milioni moja timu kumi na nane sijui ishirini wakati bara kuna watu karibu milioni arubaini na tano kuna timu kumi na sita, sijui kumi na nane sasa leo hapa tuna utitiri mkubwa lakini matokezeo yake hatuna ligi. Sasa kitu ambacho ninachokisema na sasa hivi labda waziri atatuambia sasa hivi sehemu zote dunia ligi ishamaliza ligi iliyobakia sasa hivi kombe la duni lakini Zanzibar ligi bado inaendelea sasa sijui huyu bingwa atakuja kushiriki wapi, sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, narejea tena kusema tumashindwa katika utawala *ZFA* hakuna utawala, uliopo ni utawala mbovu na bila utawala huwezi ukaenda. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naona kila nikisema naona aidha nitakuwa naanza kurejea ya wenzangu lakini hapa kitu cha msingi tunataka maamuzi ya haraka na Mhe. Mwenyekiti, amesema pale kwamba iundwe tume sasa hii tume kwa kawaida tukishaipitisha hapa azimio serikali inatakiwa iifanyie

kazi isichukuwe zaidi ya mwezi mmoja wale waliokuwepo na wao *wa-sign off* wakae pembeni, ili iundwe hiyo tume ifanye uchunguzi halafu baadaye tupate wajumbe ambao kamati ya muda inakayoendesha mpira mpaka hapo tutakapopata uongozi mpya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo baada ya hayo machache lakini la kukazia la mwisho pendekezo la tano deni ambalo *ZFA* au Zanzibar tumepigwa maana lile deni linapigwa nchi *ZFA* tumepigwa adhabu dola elfu kumi na tano kama sikosei faini.

Mhe. Mwenyekiti, kosa haikufanya serikali, kosa wamefanya watu kwa hiyo deli lile walilipe waliofanya makosa kwa hiyo *ZFA* walipe deni lile, ili Zanzibar iendelee kushiriki katika mashindano. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namna ya kupata wapi fedha nafikiri kuna taasisi najua tukiwashika wale kila mmoja alipe au auziwe mali yake.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa aibu kubwa iliyojitokeza timu yetu ya *Zanzibar Heroes* leo timu yetu kwa bahati mbaya timu ya taifa sio klabu, timu ya taifa ingekuwa klabu hata wangekwenda kwa baskeli wala nisingeshughulika kwa sababu klabu wameangalia wakajipima wakaona wanaweza, lakini leo timu ya taifa inaendeshwa kwa kodi ya wananchi wote.

Mhe. Mwenyekiti, tuliwapeleka kwenye mashindano kwa basi lakini baada ya kuja kufuatilia kumbe serikali ilitenga fedha Mhe. Mwenyekiti, fedha zilikuwepo kwa kuwasafirisha kwa ndege kwenda na kurudi lakini kwa kuwa uongozi wa *ZFA* hawajui mpira, hawajui nini maana ya mpira wakaamua kwamba baada ya kwenda wachezaji ishirini na tano wakenda watu arubaini sijui ndio wakasema maana yake pesa hii tukenda kwa ndege haitoshi, bora twende kwa basi ili kila mtu aende kwa hiyo naona watu walikwenda pikiniki kule, watu walikwenda pikiniki wakaachwa wachezaji mpira kwenda kwa ndege ili wapate kupumzika matokezeo yake wakenda kwa basi kwa sababu gani pale hakuna utawala wabovu wote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo yote jee kuna haja ya kuwepo *ZFA* mpaka sasa hivi uongozi huu uliokuwepo. Kwa hiyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, haya maazimio mawili na mimi nimeongeza, moja ya kutengeneza katiba mpya, lakini vile na wale kuwaondoa, lakini vile vile kuweza kulipa hilo deni ambalo tunadaiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako, lakini kabla kuanza mchango wako ulitaka kujua muda gani utakaotumia naona unataka kujua vipi hii kanuni inatumika ya kuongeza muda. Naomba tu, nikujibu nitamka kuwa nina wachangiaji watatu na kulingana na kanuni zetu za muda wa asubuhi ulikuwa unakaribia kuisha na ndio maana nikamuomba Mhe. Waziri wa Nchi tutengua hiyo kanuni ya muda, ili tuwape nafasi hao wachangiaji waliobaki wachangie lakini pia shughuli zetu ziko mpaka jioni. Lakini, ndio tukaona hiki kiti kitumie busara ili tumalize baadaye Waheshimiwa Wajumbe waendee na shughuli nyengine. Mhe. Hamza Hassan Juma nakushukuru sana, nadhani umeridhika na ufafanuzi huu.

Vile vile, niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe tusirejee yale kwa yale kanuni zinatukataza Mhe. Hamza Hassan Juma umerejea pia ile maazimio ambayo tayari yameshatolewa na mchangiaji mwengine. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wataochangia tena wasirejee zile zile kwa mujibu wa kanuni zetu zinatukataza jambo lile kurejea kwa mara mbili au tatu nawashukuru sana.

Sasa naomba nimwite Mhe. Panya Ali Abdalla atafuatiwa na Mhe. Ali Salum Haji na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Suleiman Sarahan Said ambaye ameniomba dakika tano. Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana hapa lakini pia nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia na mimi fursa hii kuweza kuunga mkono hoja ya mwanangu Mhe. Mohamed Said Mohamed Mheshimiwa makini sana mheshimiwa mchakarikaji wa akutafuta kero za wananchi au kero za taifa lake na kuziwasilisha hapa, Mhe. Mohamed Said Mohamed hongera sana.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaendelea kwanza naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyoelewa michezo ni ajira, michezo ni afya ambayo inasaidia nchi kuwa na vijana bora wenye afya ambao wataweza kulisaidia taifa lao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa ambayo yameonyesha katika hoja hii mimi sitaki niende mbele sana nataka nisema tunaomba tupatiwe maelezo yenye ukweli ambayo yataweza kuondosha dharau na fedheha hii kwa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, kidogo hapa hawa vijana ambao tunawahamasisha Mhe. Rais nichukuwe fursa hii kumpongeza Rais wetu wa Zanzibar kwa jitihada kubwa ambayo anaichukua katika kundaa vijana katika mawilaya yetu, mikoa yetu ili vijana hawa waje waweze kujitegemea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu hawa wangepata fursa ya kufika katika Afrika ya Mashariki na wakacheza wangeweza kujitangaza na kutafuta soko na baadaye tungeweza kuwa na vijana wazuri ambao wangeweza kujitegemea wao wenyewe na kulitangaza taifa lao.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu hapa wamesema mimi naomba niunge mkono lile azimio namba moja ambalo linataka tume huru iundwe ili iweze kuchunguza kadhia hii, tunaweza tukatoa hukumu sisi hapa lakini pengine ikawa ndivyo sivyo, lakini itakapoundwa tume ndipo itakapoonesha bayana moja moja ambalo limejitokeza. Kwa hiyo, maoni yangu naomba hii tume napongeza hili azimia namba moja ni muhimu sana tume hii huru iundwe ili kadhia hii iweze kufanyiwa kazi na baadae mchawi wetu tuweze kumjua ambaye anarejesha nyuma maendeleo ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Panya Ali Abdalla kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Ali Salum Haji (Mnadhimu) na mchangiaji wetu wa mwisho kwa hoja hii atakuwa Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii yakuweza kuchangia hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed juu ya kadhia ya vijana wetu *under seventeen* katika kadhia hii iliyojitokeaza. Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema tukianza kuchangia kwa sababu wengi tunaweza kurejea humo kwa humo tunajaribu kadiri ya uwezo wetu ili tuzungumza yale machache ambayo na sisi tunaweza kupata kutowa mawazo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naunga mkono uwasilishaji wa hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed ni jambo jema pamoja kwamba tumechelewa kwa muda mrefu kwa sababu tayari kuna baadhi ya wahusika wameshaanza kujitathmini kama kauli ya Mhe. Waziri aliyoitoa katika kuchangia bajeti yake kwamba watu wajitathimini na tayari washajitathmini. Lakini, niseme tu pamoja na yote ambayo yamejitokeza pamoja na kutathmini mimi nilikuwa na maeneo mawili matatu nilitaka nishauri na ni ya msingi ambayo pia wenzangu wamejaribi kuzungumza, wao wamezungumzia katiba mpya mimi nitazungumzia labda mapungufu ya katiba zao katika baadhi ya maeneo ambayo yanaonekana pasipo na kuyarekebisha haraka haya yatatuathiri na athari kubwa ambayo inaonekana katika Katiba yetu *ZFA* ni kifugu ambacho imanmpa mamlaka wajumbe kuweza kuchangu Rais wa *ZFA* .

Rais *ZFA* kwa mujibu wa katika yao anachaguliwa karibuni na watu 18 lakini ukiangalia washiriki na wadau hususan ya wana michezo ni vilabu. Sasa ni jambo basi tukaangalia haya mantiki katika namna nzima ya kufumua katiba katika yale maeneo ambayo yana umuhimu wa hali ya juu ili tuweze kuboresha michezo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ambalo wenzangu hawakuligusa mimi nataka nimpongeze tu Katibu wa *ZFA* Taifa kaka yetu Teddy kwa umahiri wake na utendaji ulitukuta, kwa sababu wengi tulishutuka baada ya kusikia vikao vimekaa vya kutengua maamuzi ya waliojiuzulu lakini kwa umahiri wake mkubwa na yeye kama katibu alipaswa andike barua ya kuwarejesha viongozi ambao wameamua kujiuzulu basi wamesimamia taratibu zake hakuandika barua mpaka leo na mpaka leo kikao kile kimekuwa batili na hakieleweiki kabisa, kwa hiyo naoomba mimi kwa fursa yangu nimpongeze hilo suala zima la kuamua kuto- *oxygen*.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu mimi nimemuomba Mhe. Waziri afanye jitihada za kutosha akishauriana na Baraza la Michezo sababu sisi tunayuemkamata ni Baraza la Michezo sababu chama kinajitegemea na kinashauriana na Baraza la Michezo kufanya uharakishaji wa kuchukua hatua katika yale maeneo ambayo yanaturejeshea nyuma michezo yetu, kwa sababu kuchelewa kwao kunatuathiri sisi wadau wa michezo na nimpongeze sana kwa sababu wanaosimama hapa karibuni wote hawa ni wachezaji. Mhe. Mohamed Said Mohamed mleta hoja alikuwa mchezaji wa timu ya taifa ya Zanzibar, Mhe. Hamza Hassan Juma amechezea timu ya daraja la kwanza Sebleni, Mhe. Nassor Salim Ali alikuwa Katibu wa *ZFA* wa Wilaya, mimi mwenyewe Rais wa Timu ya Mpira ya Zanzibar sasa tunaosimama hapa tunazungumza kwa uchungu tukifahamu misingi na umuhimu wa michezo katika nchi yetu, tukiangalia namna ya vipaji vya Wazanzibar vilivyokuwa vina uwezo katika mazingira mazuri ya kuweza kujiajiri katika sekta binafsi baadhi ya watu wanavyovi-*demote* na kuvurejesha nyuma kwa uongozi ulikuwa sio mzuri.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri karibuni nimeanza mashindano hapa yameanza mashindano ya *FA* ya kumpata mtu wa kuweza kushiriki katika mashindano ya klabu bingwa sasa haya mashindano pia yameanza kutuvuruga huko chini, yameanza kuruvuruga kwa saababu lile la mwanzo halijamalizika yanakuja mengine na haya yameanza kutuvuruga watu wamekwenda kuchukua vilabu vyao, vilabu vya masahiba zao wameacha vilabu vyenye uwezo wa kuweza kuishiriki, ili kumpata mshindi wa kuja kushiriki mashindano ya kimataifa na wanachukua vilabu kwa sababu ya msingi yao tu wanayojua wenyewe, sasa hili tusipolichukulia hatua za haraka linaweza kutufikisha pahala ambapo si pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tunachelewa tuna mambo ya muhimu ambayo yanahitaji kurejekebishwa ili mpira wetu uendelee. Mhe. Hamza Hassan Juma kanifilisi hapa dunia nzima hakuna pahala ambapo mashindano yanaendelea mashindano yashamaliza tangu mwezi wa tano dunia nzima yanamalizika, lakini hivi sasa hivi Zanzibar hatua ya pili ya *premium* haijachezwa imechezwa hatua ya mwanzo, hatua ya pili ni kuzishirikisha timu nne za Unguja, timu nne za Pemba hawa watu hawajaanza hata ligi kisingizio wanasema Ramadhani dunia inaenda na kalenda watu wanataka waelewe Ramadhani inakuja mwezi gani na sikukuu mwezi gani, ukiwauliza leo wanakwambia tumekubwa na Ramadhani mashindano yamesimama Ramadhani mwezi mmoja.

Daraja la pili timu bora zile bingwa wa mjini hajapatikana yule bingwa wa Wilaya ya Mjini daraja la pili hajapatikana anatakiwa apatikana bingwa wa daraja la pili wende katika hatua ya timu nne bora wakitoka hapo timu mbili kila Wilaya wanatakiwa washindane kwa Wilaya zote za Zanzibar, hizo hatua bado refu hatujii ligi itamaliza mwaka gani unampata bingwa ambaye hata ladha hana ukiachilia hayo mengine, zawadi hakuna, mambo mengine hakuna yanatusononosha na sisi ndio wadau.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri tumesema hapa hatua za haraka zichukuliwe kwa kushirikiana na Baraza la Michezo kuona hatua za dharura zinachukuliwa kusaidia michezo kwa sababu katika kipengele cha katiba hiyo hiyo ya *ZFA* Taifa, kwamba pindipo uongozi unapoondoka madarakani kwa namna yoyote wamejiwekea mwaka mmoja na nusu ndio kufanya mabadiliko, mwaka mmoja na nusu kuweka kamati za dharura kuongoza mchezo ni muda mrefu maana yake umejipangia makusudi kama wataondoka madarakani maana yake tusiweke uongozi wa dharura mpaka muda wa kuchaguliwa wa kikatiba ufike.

Sasa hayo ni mapungufu muda wa mwaka mmoja na nusu unasubiri uunde viongozi wa dharura wa kuongoza soka yaani tukae mwaka mmoja na nusu sisi tukae kimya ni tatizo hasa hilo maana yake tukifanya vyengine tunaingilia katiba. Kutokana na hali hiyo, hatua za dharura zinahitajika katika kunusuru michezo katika nchi ya Zanzibar, viongozi wetu wanajitahidi tunaona namna wanavyojitahidi katika kutoa mazawadi mbali mbali motisha mkubwa kwa vijana wetu, lakini mashaka yanabakia kwa watendaji muangalie katiba zinakavyokuja.

Tatizo kubwa linavyojitokeza nasema tena katika kipengele kikubwa cha kuhakikisha katiba inawekwa sawa tutowe fursa kwa vilabu ama makatibu wote vilabu vilivyokuwa *registration* kwa msajili ndivyo vimchague Rais wa *ZFA* Zanzibar sio kikundi cha watu kumi na nane, sasa

hivi wamejiweka watu kumi na nane ndio wenye mamlaka wa kuteuwa Rais wa nchi nzima akateuliwe na watu kumi na nane huyu wa nchi hawi hivyo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naunga mkono hoja na ninaridhia mapendekezo yote yalotolewa na mtoa hoja. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Ali Salum Haji. Sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwisho wa hoja hii Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja yetu hii ambayo iko mbele yetu. Kwanza naunga mkono hoja kama wenzangu walivyounga mkono. Lakini hili jengine ulisema tusirudie rudie Mhe. Mwenyekiti nakuomba kwa sababu ya kumpongeza Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika jitihada zake za kujuza michezo ikiwemo kujenga viwanja katika kila Wilaya na pia kutupa zawadi katika timu yetu iliyofanya vizuri *Zanzibar Heroes*. (*Makofi*)

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hili nilizungumze kwamba kwa kweli *speed* iliyotoka kwenye *Zanzibar Heroes* ambapo ilianguka Zanzibar ikaja zake Zanzibar, basi vijana walibadilika na Zanzibar ilibadilika katika michezo. Kwa kweli, suala hili limeiletea ile timu yetu ya *under seventeen* na wao walikuwa na uhakika wanakuja na zawadi na Mhe. Rais wa Zanzibar atawapongeza tena. Sasa imepinguza ari ya michezo lakini hata Mhe. Rais wa Zanzibar ile kasi yake aliyokuwa nayo basi nayo nina uhakika imepungua kutokana na sababu zilizojitokeza. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niulize swali mmoja sisi ni wepesi sisi kama tuseme ndio tuna uongozi, sisi timu yetu ya *Zanzibar Heroes* iliyokwenda kule Kenya katika mashindano ilifanyiwa *disturbance* katika hali ya *final* ikatolewa damu wachezaji wale waliwaona wanacheza vizuri wakaonekana kama wanatumia madawa ya kulevya na vitu vyengine. Lakini sisi hatukudai chochote kilichotupa *disturbance* na pengine ubingwa tungeupata lakini sababu zile hata kupeleka malalamiko yetu katika *CECAFA* hatukupeleka na timu yetu ikarudi. Na mara hii wametuchezea tena sijui ni wale wale au ni wengine kuitoa *Zanzibar under seventeen* katika sababu zilizokuwa si za msingi.

Mhe. Mwenyekiti, hizi sababu zina matatizo sana mtu anapokwenda nchi za nje anaangaliwa kuanzia kwenye *passport* na kila kitu chake na mpaka kule anakokwenda na kuna mambo mengi yanayofanyika, inakuwaje mpaka tunafika *final* katika masuala haya ndio yanajitokeza matatizo. Kwa hivyo, baada ya kuonekana timu ya Zanzibar iliyokwenda pale kwamba inaonesha tochi hii timu itachukua ubingwa, ndio imeanzishwa na *problem* nyengine ya *under seventeen* hawafai. Sasa hapo tunataka tujiulize kutokana na matatizo yetu hayo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala jengine linalozungumzwa, mheshimiwa katika miaka hii ya 1990, 1980 huko Zanzibar ilikuwa imechenguka kweli kweli katika masuala ya michezo. Watu walikwa ikichezwa michezo Amani, watu hawapandi gari tena wanatoka Amani mpaka Malindi, Amani mpaka Mlandege, Amani mpaka wapi lakini timu yetu hii ya Mlandege imeshachukua kombe la Tanzania Mwanza, hamasa zilikuwa kubwa. Sasa hivi hakuna hata mmoja anayetizama mpira Zanzibar anatizama mpira wa Uingereza hata habari leo anacheza nani hakuna, kaangalie

Amani pale utakuta kivuli cha watu watatu tu wanatizama mpira Ligi Kuu, *final* hapana, sasa tuangalie tatizo liko wapi.

Kwa hivyo, tuangalie kwamba upande huu wa *ZFA* haujajipanga kimataifa, umejipanga kama wanavyosema wenzangu kombe la ndani tu la kwamba nani na nani, nani na nani lakini hatujajipanga wachezaji wetu kuwatoa nje. Kwa kweli, jambo hili tunalitizama tu suala dogo la michezo Mhe. Mwenyekiti hapa tungetengeneza ajira, tungetengeneza pesa za kuleta humu nchini na wachezaji wengi tu wangepata faida kubwa sana. Lakini bado kila siku tunaututika mzigo wa vijana matokeo yetu ndio haya yanayotokea sasa hivi kubakana tu, kwa sababu hata hizi kazi hazifanyiki tena yote imekuwa ni matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wakiingia kwenye michezo kazi hizo wanazisahau kabisa wanaelekea kwenye michezo, lakini sasa kwa sababu hizi *ZFA* na shughuli nyengine za Baraza la Michezo hazishughuliki itakiwavyo, basi wachezaji na vijana wanapotea vibaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini malalamiko mengi kwa *ZFA* si ya leo ni miaka mingi, wachezaji wanalalamika, timu zinalalamika lakini hata ukitizama kusimamia haki zinavunja moyo timu. Kwa hivyo, hili ni la kimataifa lakini zinaanza ndani hawawatendei haki wachezaji, hawawatendei haki timu na hata rufaa haziendi zinakwenda kwa mtu ndani ya mkoba wake anaamua rufaa anavyotaka yeye na wala haiingiliwi. Kwa kweli, kama tunavyosikia hapa majibu yetu serikali inaacha nafasi kwamba hawaingiliwi wajitawale wenyewe, hawawezi kujitawala kwa hivyo lazima serikali iingilie kati *otherwise* itakuwa tumekosa kila jambo.

Mhe. Mwenyekiti, uongozi una miaka yake lakini licha ya miaka una *final* zake katika masuala, lazima viongozi tunaowapa jukumu hili tujitathmini. Wenzetu anaichukua timu ya taifa akienda kule akirudi na kitu kibovu anachukua *briefcase* yake hata harudi kule nchini kwa watu. Sio sisi hata akirudi anakuja kucheka tena utasikia sio rizki Mwenyezi Mungu hajatujaalia, Mwenyezi Mungu hajatujaalia mpaka lini. Kila jambo sisi tunakaa Mwenyezi Mungu hakutujaalia kwa sababu mheshimiwa maelekezo lazima tutizame. Mtu anajitasmini kocha amefanya vibaya, uongozi umefanya vibaya ukirudi tu hapa hakuna habari ya kanuni wala nini, ondoka tuanze na kitu kingine.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie juzi tu timu ya Argentina ilifanya vibaya ikawa inatoka toka nje, Maradona alimwambia kocha usije ukarudi tena Argentina ikitolewa, na juzi imecheza kufa na kupona mpaka imeingia. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti lazima kitu hiki kiwepo.

Mhe. Mwenyekiti, *ZFA* pamoja na michezo lakini hasa *ZFA* katika suala la mpira haijajiendesha kisasa, haina historia, haina vitu vyovyote vya wana michezo. Inajiendesha mtu kapuni, inajiendesha mtu hivi hakuna chochote. Kwa hivyo, hilo lilikuwa ni jambo ambalo hatuna la kuangalia zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini uongozi wa mpira ni tofauti na taasisi nyengine, huwezi kumchukua mtu Barazani ukenda ukampa mpira au ukampa uongozi wa mpira. Mpira una fani yake tofauti na hata hao wenzetu lazima rikodi ya dunia ichukue, huyu alikuwa wapi, alifanya nini. Sio leo tu mtu akifika na wewe jaza fomu, na wewe jaza fomu hili sio kumbwaya kwamba kila mmoja anaingia, huu ni mpira uliokuwa unajuilikana dunia nzima na fani yake inajuulikana.

Kwa mfano, sasa hivi mchezaji wa mpira ana pesa, ana thamani kuliko hata mawaziri, kuliko hata maeneo mengine, kuliko mchezaji wa mpira. Kwa hivyo, mchezaji wa mpira ana thamani kubwa sana ulimwenguni, hivyo sisi hatuna hata mmoja humu ndani, hatuna mchezaji hata wa kupita wa kumpa mkono. Wachezaji huko mtu anatia saini mpira au anatia saini pahala anambusu mtu anaona fahari kukataa hapa tuna mchezaji gani. Hatuna mchezaji hata mmoja humu tuliyemtuza wala tuliyenaye katika masuala kama hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu muda umeshakwenda sana mimi ningesema tu kutokana na kadhia hii iliyotupata, Mhe. Mwenyekiti lazima tukae chini nasema tena kwa lugha yangu ile nyengine tupige mstari mwekundu tunaanza mwanzo tuache matatizo yote Waswahili wanasema "yaliyopita si ndwele tugange yajayo". Lakini ninachokizungumza Mhe. Mwenyekiti sasa tuwe makini na suala hili, pia tusitizame upande mmoja, tuna tabia ya kutizama hapa kwetu tu makosa yetu na kule nje wale wanaotufanyia *sabotage* tunawatizama.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja, nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Suleiman Sarahan Said kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite mtoa hoja Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu imechukua muda mrefu na mimi nitajaribu kujumuisha kwa kifupi sana ili wajumbe wako wapate muda wa kupumzika lakini hili ni suala muhimu sana ambalo lilikuwa liko mbele yetu. Vile vile, nishukuru kwa dhati kabisa kutokana na ndugu yangu, kaka yangu Omar Hassan King, Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kuwa amewasili pamoja na Mkurugenzi wake Kilangi ili kusikia kadhia nzima ya timu yetu ya taifa, hongereni sana.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hii imechangiwa na takriban wajumbe 15 na wajumbe 10 wamechangia moja kwa moja lakini wajumbe 5 wamechangia kwa maandishi na nitaomba kwa heshima kubwa sana niweze kuwataja wajumbe hawa.

1. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali
2. Mhe. Suleiman Makame Ali
3. Mhe. Nassor Salim Ali
4. Mhe. Rashid Makame Shamsi
5. Mhe. Machano Othman Said
6. Mhe. Ali Suleiman Ali
7. Mhe. Hamza Hassan Juma
8. Mhe. Panya Ali Abdalla
9. Mhe. Ali Salum Haji
10. Mhe. Suleiman Sarahan Said

Hawa ndio wajumbe ambao walichangia moja kwa moja, lakini kuna wajumbe 5 wamechangia kwa maandishi nao ni.

1. Mhe. Bahati Khamis Kombo
2. Mhe. Maryam Thani Juma
3. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
4. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
5. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame

Mhe. Mwenyekiti, wengi wao kwanza niseme katika moja ya maadhimio yetu nimeyapata mengi ambayo kila mtu alikuwa akitia labda kionjo chake katika kuhitimisha maadhimio hayo. Lakini moja katika yote ambayo tutaadhimia ni iundwe kamati ya mpito ya *ZFA* ambayo ndio itaiongoza. Sasa hili ndio moja ambalo nitaiongoza iundwe kamati ya mpito ambayo itaongoza *ZFA*. Lakini nisisahau suala zima la Mhe. Ali Salum Haji nikubaliane na hoja yake ambayo yeye alitaka kusema Katibu huyu wa *ZFA* Taifa aliyekuwepo sasa hivi aweze kuendelea angalau kwa sababu yeye ndiye muajiriwa wa serikali, angalau aweze kumaliza mashindano au kimeo kile cha mashindano yaliyobaki. Kwa sababu tunaita kimeo hakuna *league* kubwa duniani kama *league* ya Zanzibar inachukua muda mrefu, lakini vile vile inachukua timu nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajunmbe wamesema maneno mengi kwanza Katiba ya *ZFA* ni kweli tukiitizama Katiba ya *ZFA* ina matatizo. Matatizo yenyewe tayari Kamati Tekelezaji mbili, lakini kuna Makamu wa Rais wawili, Rais awe mmoja nchi hii moja kuwa na Kamati Tekelezaji mbili, Makamu wa Rais wawili haipendezi sana. Sasa tuwaambie wenzetu *ZFA* na serikali kwa jumla tukisema ifanyiwe mapitio Katiba ya *ZFA* angalau kuwe na Kamati Tekelezaji moja na Makamu wa Rais mmoja. Na inanishawishi sana kusema Makamu wa Rais, Rais akitoka Unguja Makamu wa Rais atoke Pemba. Lakini Rais akitoka Pemba Makamu wa Rais aweze kutoka Unguja. Hii inanishawishi sana kuliko kusema Kamati Tekelezaji hizi tutazigawa mbali mbali haitupi sifa nzuri na kwa sababu chama chetu kimoja.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli waheshimiwa wengi wametoa michango yao moja kwa moja na wengi wametoa katika kujenga sana *ZFA* tuione *ZFA* ya mpito lakini tuone sasa hata hizi pesa ambazo ni za kulipwa mimi niungane nao kabisa. Hii serikali sio iliyofanya kosa, iliyofanya kosa ni ile baada ya tume yetu kuchunguza na kubaini nani hasa aliyefanya kosa, basi pesa zile zilipwe na watendaji wenyewe. Niungane sana na Mhe. Hamza Hassan Juma hata wale watendaji waliohusika na hili kama kuna mali zao ziuzwe, basi ziweze kuuzwa kufidia deni hili sio kutoa pesa za wananchi walipa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, wengi wamezungumza mambo mengine, gharama lakini Mhe.Nassor Salim Ali amezungumza kuwa Ghana imevunja chombo chake cha mpira kutokana na kufanya vibaya. Tuwapongeze sana Waheshimiwa Wawakilishi angalau kwa kufatilia jambo hili, na jambo hili linauma sana na tuseme tu pamoja na michango yenu mbali mbali naichukua yote tutayafanyia kazi lakini vile vile na haya maoni yaliyotolewa pamoja na maoni matatu niliyoyatoa na hili la nne tunaliongeza hapa.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya kupoteza muda niseme tu michango ya Waheshimiwa Wawakilishi yote ilikuwa mizuri na yenye kujenga chama chetu, na wote walikuwa wanalia sana kupunguza migogoro katika Chama cha Mpira, lakini vile vile kuweka Chama cha Mpira kiwe *strong*, ili kuunda na kuweza kuviimarisha vipaji vyetu vya wana michezo wetu. Zanzibar tuna vipaji vizuri tumeiona *Zanzibar Heroes* ilivyofanya kazi vizuri lakini tulitegemea sana na hii *under seventeen*

itafanya vizuri, lakini bahati mbaya sana kutokana na uzembe uliofanyika hapa haikuweza. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, niseme baada ya kuongeza hilo azimio moja pamoja na yale ya mwanzo niseme tu naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Machano Othman Said, kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe ambaye ametoa hoja alikuja maazimio matatu lakini na sisi tuliongezea maazimio, yeye kazungumzia kamati ya mpito sawa tunalikubali azimio lake, lakini pia tulikuwa tuna azimio kwamba na Katiba ya *ZFA* nayo ifanyiwe marekebisho iwemo katika maazimio.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yangu mafupi sana na kuchukua michango mingi ya Waheshimiwa Wajumbe, nilisema iundwe Tume Huru, ile Tume Huru ndio itafanya vitu vyote na baadae nikasema hainishawishi kuweza kuwa na Kamati Tekelezaji mbili labda Makamu wa Rais wawili kutoka katika pande zote. Sasa hii Tume Huru ndio itakayochunguza na kufanyiwa marekebisho ili tuazimie hii Tume Huru iifanyie marekebisho ya Katiba ile, ili Katiba itakayotungwa sasa iwe sawa.

Kwa hivyo, hapa Mhe. Waziri aunde Kamati ya Mpito ya kuongoza *ZFA* ili baada ya kutengenezwa Katiba Mpya ndio uchaguzi uendelee. Kwa hivyo, ningeomba tu Mhe. Machano Othman Said, Mwenyekiti Mstaafu wa *ZFA* Wilaya ya Mjini anikubalie hili ili hiyo Tume Huru ndio itakayopitia Katiba na baada ya Katiba ndio ufanyike uchaguzi. Mhe. Mwenyekiti, baada ya *concern* ya Mhe. Mwenyekiti Mstaafu naomba sasa nitoe hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohamed Said Mohamed, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa ili kupitisha maazimio ya mtoa hoja. Sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na maazimio hayo wanyooshe mkono, wanaokataa, inavyoonekana wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa hoja yake, lakini naomba niwakumbushe au niikumbushe serikali kwamba Mhe. Mohamed Said Mohamed ametumia Kanuni hizi za Baraza 27(3) ambayo inamruhusu kufanya hili jambo, lakini pia Kanuni hizi hizi zimeiamuru Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Kanuni ya 58(9) naomba niisome.

"Serikali itawasilisha katika Baraza, ndani ya miezi mitatu baada ya maazimio ya Baraza juu ya mjadala wa hoja ya mjumbe, taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo; italetwa katika kipindi cha miezi mitatu".

Kwa hiyo, nawaomba sana serikali ichukue maazimio hayo na muda ukifika kwa mujibu wa Kanuni zetu basi walete maazimio hayo yaliyoletwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, niseme nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yenu lakini pia kwa utulivu wenu na nina imani Serikali ya Mapinduzi chini ya Mawaziri wake ikiongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi basi maazimio hayo yataletwa ndani ya kipindi hicho kwa mujibu wa Kanuni zetu. Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe, naomba niakhirishe kikao hiki mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 7:32 Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe
29/06/2018 saa 3:00 asubuhi)